

11 APRILI, 2013

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tatoo - Tarehe 11 Aprili, 2013

*(Mkutano Ulianze Saa Tatoo Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. [The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Local Government Authorities for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012].

11 APRILI, 2013

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Maendeleo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwezi Machi, 2013. [*The Report of the Controller and Auditor General on Contract Management of Development Projects in Local Government Authorities in Tanzania, March, 2013*].

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. [*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of the Central Government for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*].

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. [*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of Donor Funded Projects for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*].

Ripoti ya Jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi na Maalum kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2013. [*The General Report of the Performance and Specialized Audits for the Period ended 31<sup>st</sup> March, 2013*].

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. [*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the Financial Year 2011/2012*].

11 APRIL, 2013

*The Report of the Controller and Auditor General on the Performance of ICT Equipment in Public Sector, March, 2013.*

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji wa Soko la Bima nchini kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2011. [The Annual Report on Insurance Market Performance report for the year ended 31<sup>st</sup> December, 2011].

#### **NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:**

Taarifa ya Madhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Utendaji wa Masuala ya Afya na Usalama Maeneo ya Kazi nchini Tanzania, ya Januari, 2013. [The Report of the Controller and Auditor General on the Performance Audit Report on the Management of Occupational Health and Safety in Tanzania in January, 2013].

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa Shughuli za Uvuvu katika Ziwa Viktoria ya Januari, 2013. [The Report of the Controller and Auditor General on the performance Audit Report on the Management of Fisheries Activities in Lake Victoria in January, 2013].

#### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Sukari Tanzania kwa Mwaka wa Fedha Ulloishia tarehe 30 Juni, 2012. [The Annual Report of Audited Accounts of Sugar Board of Tanzania for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012].

11 APRILI, 2013

**SPIKA:** Katibu tuendelee!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita tulipitisha hapa Sheria ambayo ilikuwa inaleta marekebisho kwa Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ilisema wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali analeta ripoti hapa, Serikali pia *concurrently* kiingereza lazima pia waweke mezani majibu ya ripoti ya CAG. Leo tumekaa hapa tumepeata ripoti, hatujapata majibu ya Serikali.

Hii ndiyo kusema tunavunja sheria siku ya kwanza ambapo sheria hii inapaswa kuanza. Naomba mwongozo wako. (*Makofit*)

**SPIKA:** Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inatosha tutajibu baadaye. Katibu!

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 20

### **Tatizo la Ajira Nchini**

**MHE. VINCENT J. NYERERE** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la Wahitimu wa Vyuo mbalimbali hapa nchini lakini hakuna ajira kwa wahitimu hao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusitisha kutoa mikataba kwa wastaafu ili wahitimu wanaotoka vyuoni wapate ajira na kujenga nchi yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wako wataalam wengi wanaohitimu katika vyuo mbalimbali hapa nchini. Wahitimu hao hupatiwa ajira kulingana na mahitaji ya nchi na pia kwa kuzingatia uwezo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mikataba hutolewa na Serikali inapoonekana ni kwa manufaa ya Umma kufanya hivyo kutokana na mahitaji makubwa katika sekta husika. Kifungu 12.2 cha Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998 kinatamka wazi kwamba endapo Utaalam wa Mtumishi unahitajika sana, Serikali inawajibika kumuomba mtumishi kuendelea kufanya kazi na siyo mstaafu mwenyewe kuomba. Kwa sasa Serikali inawapa mikataba wataalam wastaafu ambaio sio rahisi kuwapata katika soko la ajira, hususan wataalam wa kada muhimu kama vile Walimu, Waganga, Wahandisi na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuhitajika kwao, wataalam hawa wanapostaafu wanaendelea kutumiwa kwa kuwapa mikataba ya muda mfupi sambamba na kuajiri wahitimu wa vyuo mbalimbali. Kwa mantiki hiyo Serikali itaendelea kuajiri wastaafu katika kada hizo muhimu hadi hapo soko la ajira litakapojitosheleza.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa kulinda muda naomba maswali yenu ya nyongeza yawe mafupi na Mawaziri majibu yenu ya nyongeza yawe mafupi kwa sababu *by* saa Nne Kamili lazima nifunge mazungumzo na nikifunga hakuna msamaha kwa mtu ye yote. Mheshimiwa Nyerere swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa kazi za Wakuu wa Mikoa siyo za kitaalam na wengi ni wastaafu kutoka maeneo mengine, nini tamko la Serikali kuhusu ajira zao.

11 APRILLI, 2013

**SPIKA:** Hayo ndiyo maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mheshimiwa Vincent Nyerere, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa siyo watumishi wa Umma, wako kwenye upande wa watumishi wa kisiasa kama mlivyo Wabunge.

**MHE. LAIZER M. LEKULE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wafanyakazi wengi wamestaafu na wengine wamefariki na Serikali kuwaacha watumishi wote wakiwa kaimu, kaimu, kaimu kwa kila Idara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziba nafasi hizo?

**SPIKA:** Safi kabisa, haya ndiyo maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule M. Laizer kama ifuatavyo:-

Nafasi mbadala huwa hazina matatizo yoyote, ni pale tu mtu anapostaaafu Halmshauri husika inaleta taarifa kwetu Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma. Tukiishapata tunatoa vibali mara moja ili nafasi kwa watumishi waliostaafu wawewe kuajiri mara moja. Kwa hiyo, tatizo la nafasi mbadala huwa siyo kubwa sana kama ilivyo kwa watumishi ambaao ni wa ajira mpya.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ajira ni chache na ndio maana vijana wanakosa ajira na vijana kwa sasa wamefunguka kiakili wamekuwa wakijijiri wenyewe lakini kikwazo ni mtaji.

Je, Serikali iko tayari kuzungumza na benki ili kupunguza vigezo na riba ili vijana hawa waweze kupata mikopo na waweze kufanya kazi zao? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa Niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, analolitaka Mheshimiwa Mbunge ndivyo hivyo Serikali inajitahidi kufanya kuititia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi. Serikali imeweka dhamana ya shilingi bilioni 2.1 lakini benki zinatoa mara tatu na pengine hata zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, tutajitahidi sana kwa wale ambao wanaleta andiko ambalo linalidhisha basi tutawaelekeza kwenye benki. Tukifanya hivyo nina hakika suala la ajira ya vijana pengine tatizo litakuwepo lakini litapungua kila tunavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Walimu ni mionganini mwa kada muhimu za utumishi na hivi karibuni Serikali imetoe ajira kwa kada hii ya walimu isipokuwa wanafunzi waliosoma *BED(Psychology)* pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine suala la kuajiriwa limekuwa ni tatizo.

11 APRILI, 2013

Nini kauli ya Serikali kuhusiana na watu hawa ambao wamesoma kada ya ualimu, *Especilly BED (Psychology)*, nini hatima yao katika suala zima la kuajiriwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses J. Machali, kama ifuatavyo:-

Ni kweli mwanzoni wakati tunawapangia ualimu wale ambao wamechukua BED tulikuwa hatujawapangia, lakini sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, inafanya mpango wa kuwapangia nafasi ambazo zinawahusu watumishi hawa ambao wamechukua *Education* pamoja na *Psychology*.

**SPIKA:** Ahsante. Kwa dakika tano tumepata maswali ya nyongeza manne, kitu ambacho ndicho tunachotaka kiwepo.(Makofi)

Na. 21

### **Biashara Haramu**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Hivi karibuni kumezuka wimbi la biashara haramu ya binadamu na wanaohushishwa kwenye biashara hiyo ni wasichana na wavulana ambao wengi wao wako chini ya umri wa miaka 18.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu za msingi za kushamiri kwa biashara hiyo haramu kwa miaka hii ya karibuni?

(b) Je, ni wasichana na wavulana wangapi ambao wameishasafirishwa huko ughaibuni katika kipindi cha miaka miwili 2010/2011 – 2011/2012?

(c) Je, vijana hao wanauzwa kwenye nchi zipi hasa ambako wanatumikishwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ziko sababu mbalimbali zinazofanya kushamiri kwa biashara haramu ya wanadamu hapa nchini. Mionganoni mwa sababu hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Kuwepo kwa mtandao haramu wa watu waovu ambao wanafanya mikakati ya kujipatia pesa.

2. Vijana wengi kutafuta ajira na nafasi za masomo nje ya mfumo rasmi.

3. Baadhi ya vijana kudhani kuwa ughaibuni kuna maisha bora na hivyo kudanganywa kwa urahisi na kuchukuliwa na watu waovu.

(b) Mheshimiwa Spika, biashara hii haramu ya binadamu, hufanywa kwa siri na hivyo kufanya taarifa za matukio hayo kutopatikana au kupatikana kwa shida. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 na 2011/2012 hakuna matukio yoyote yaliyori potiwa ya kuwepo kwa biashara haramu ya binadamu dhidi ya wavulana au wasichana wenye umri chini ya miaka 18 kuchukuliwa kwenda nje ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye sehemu (b) ya swalii hili, hakuna taarifa ya kuuzwa kwa vijana wa Kitanzania katika nchi yoyote.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

11 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kwamba kuna baadhi ya watu hutaka kuoa lakini mahari wanakuwa wamechangishana watu wengi, na yule mama anapoolewa anakuwa ameolewa na waume wote waliochangia mahari.

Je, Serikali inaeleza nini kuhusu hili?

Je, tetesi hizi nazo Serikali nayo haijazisikia? (*Makof*)

Swali la pili, Serikali imekiri kuwa kuna watu waovu wanaofanya biashara hii ovu.

Je, Serikali sasa haioni sasa kama kuna haja ya kuandaa utaratibu rasmi kutoka nchi wanazohitaji ajira na huku kwetu tukaandaa utaratibu rasmi ili tujue watu wetu wanaenda wapi na wanafanyishwa kazi zipi?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, maana ni mabomu kweli kweli hayo. (*Kicheko*)

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la ndoa, mara nyingi ndoa linakuwa ni jambo la watu wawili. Lakini linapokuwa ni la mchango kwa kweli ni mtihani. (*Kicheko*)

Taarifa hizi kwa kweli hata kama zitatokea ni tabu kuzipata kama Serikali, lakini tukizipata tutasaidiana na balozi zetu ili tuweze kuona ni vipi tunaweza tukasaidia lisitokee kwa kuzungumza na wenzetu kwa kusaidiana na *foreign affairs*.

Swali la pili, ni kweli kwamba kuna mitandao ambayo ni ya siri na *informal* ambayo inachukua watoto na vijana kwa ajili ya kuwatumikisha. Hata hivyo Serikali si kwamba haina taasisi ambayo pengine ingesaidia kufanya kazi hii. Watoto ambao wanachukuliwa pengine kinyume na utaratibu hawajafikia umri kushughulikiwa na chombo hicho. Lakini kuna chombo kinaitwa *Tanzania Employment Service Agent TAESA* ambacho Serikali iliukiunda kutafuta kazi ughaibuni kwa ajili ya Watanzania. (*Makof!*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, nina ushahidi wapo wasichana wanaoenda nchi za Ughaibuni kwenda kufanya kazi za ndani na nina ushahidi msichana mmoja alikaa miaka miwili hata kurudi ikawa kazi alikaa ndani na alinyang'anywa simu na kufanya kazi masaa 24 nimeingilia kama Mbunge nimetumia jitihada zangu huyo msichana amerudi ana wiki sasa na anasema wenzake wapo kule.

Je, yupo tayari kufuatilia hapa hata kumtumia huyu msichana ninayemfahamu kumwuliza ili awape taarifa muwasaidie hao vijana? (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, chombo chetu ambacho Naibu Waziri alikitaja cha *TAESA* kinafuatilia mambo haya na kama taarifa hizo zipo mimi ningefurahi sana Mheshimiwa Diana Chilolo anipe na Mtanzania mwingine yoyote ambaye ana taarifa za Watanzania kunyanyaswa huko kwa kigezo kwamba wanapata kazi ili tuzifanyie kazi tuwasiliane na Ubalozi kule ili tukomeshe tatizo hili.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Swali moja dogo la nyongeza. Siyo kwa Watanzania wanaopelekwa nje ya nchi peke yake. Lakini wapo pia watu kutoka nchi jirani kama Wasomali ambao wamekuwa wakiingia au kupita kwenye mipaka yetu kinyume na sheria.

11 APRILI, 2013

Mfano mzuri ni wale waliokutwa Dodoma kwenye lori zaidi ya watu 40 wakiwa wamekufa na wengine walikuwa wameishavuka *bordertayari* kwa maana ya *borderya* kwetu na ya Kenya walienda kukutwa kwenye *border ya* pili labda Zambia au Malawi. Sasa nini kauli lya Serikali kwa sababu wakati mwagine tunaweza kujikuta kwamba tumeingiliwa na tunatekwa hapa Bungeni bila kufahamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa wimbi la watu kutoka pembe ya Afrika kupita ndani ya nchi kwa nchi za huko na jitihada nyingi zinafanywa za ndani na za Kitaifa. Lakini pia tunafanya jitihada za Kimataifa pamoja na wenzetu na Kikanda kuhakikisha kwamba mtandao ambaou unahusika tunaupata na tunaudhibiti kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa. Lakini mbinu siku zote zinabadilika, mwanadamu ndiye anayeuzwa na mwanadamu ndiye anayenunua na mwanadamu ndiye anayefanya mbinu. Tutaendelea kulifanya kazi lakini tutahakikisha kwamba tunalikomesha kwa nguvu zote.

Na. 22

**Fidia Kwa Madhara Yatokanayo na Uvunjifu wa Amani**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Inapotokea hali ya uvunjifu wa amani kwa bahati mbaya humlenga mwananchi aliyekuwepo na asiyekuwepo. Pia athari mbalimbali za mali au mtu binafsi zinaweza kutokea:-

Je, kwa yule mwananchi ambaye alikuwa nyumbani kwake, kwa bahati mbaya akapata athari ya mali yake au kuumia yeye binafsi, Serikali ina utaratibu gani wa kumsaidia au kumlipa fidia mwathirika huyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)  
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vitendo au hali ya uvunjifu wa amani vinavyofanywa na watu au makundi ya watu wasiozingatia utii wa sheria vinaweza mara nyingi, husababisha madhara kwa watu wengine wasiohusika na wasiounga mkono vurugu za aina hizo. Kwa mwananchi yeьте anayepata madhara ya kuharibiwa kwa mali zake au kuumia anayo haki ya kufungua mashtaka ya madai katika Mahakama kudai fidia ya hasara aliyopata au uchungu aliongopata kutoka kwa aliyesababisha madhara hayo. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa sheria zinazoongoza madai dhidi ya madhara ambayo mtu anayapata (*Law of Torts*) kutokana na vitendo vya mtu au watu wengine.

Aidha, sheria ya mwenendo wa kesi za jinai katika kifungu cha 348 inaruhusu Mahakama kutoa fidia kama itakavyoona inafaa pale ambapo mtuhumiwa ametiwa hatiani.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa sheria zilizopo, Serikali haina utaratibu wa kumlipa fidia mwathirika yeьте wa madhara ya uvunjifu wa amani pale inapothibitika kusababishwa na mtu au watu binafsi.

Endapo itathibitika kuwa mtumishi au chombo cha Serikali kimehusika na kusababisha uharibifu wa mali au kuumia kwa mtu, sheria zetu zinaruhusu mtu huyo kulipwa fidia pale inapothibitika kuwa madhara hayo yanatokana na uzembe au matumizi ya nguvu zinazopita kiwango kinachokubalika.

11 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali mara zote umekuwa unahimiza kudumishwa kwa amani na utulivu nchini kutokana na hilo, Serikali huchukua hatua kali za kisheria kwa kuwafikisha Mahakamani wale wote wanaosababisha uvunjaji huo. Hatua hizo ni kama zilizowekwa na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura 16 ya Sheria za Tanzania kwa kuititia Bunge lako Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwahimiza wananchi kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu. (*Makofii*)

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa inapotokea vurugu unakuwa humjui nani aliyeanza au nani aliyesababisha vurugu hizo na wewe mhusika uliyefikwa na madhara yale humjui nani wa kwenda kumshtaki.

Je, kwa nini Serikali isiweke kitengo maalum ambacho mwathirika yule anaweza kwenda kuonana na kitengo kile?

(b) Kutokana na maelezo yake ameeleza kwamba ikiwa kitatokea kitendo kile, chombo cha Serikali kimefanya kwa uzembe.

Je, mhusika yule anatakiwa aende akamwone nani ili fidia ile aweze kuipata kutokana kitendo kile cha uzembe kilichofanywa na chombo cha Serikali? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli inapotokea vurugu mara nyingi huwezi ukafahamu nani aliyeanzisha lakini tuna vyombo vyetu nya dola huwa vinashughulikia masuala hayo.

Kwa hiyo, Polisi ni chombo kimojawapo ambacho kinashughulikia masuala hayo na kinafanya uchunguzi na kuangalia kwamba ni nani aliyesababisha madhara hayo.

Chombo kingine ambacho kinashughulikia ni chombo cha Haki za Binadamu, tunacho kitengo chetu Haki za Binadamu ambacho kipo chini cha Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria kinashughulika na Haki za Binadamu. Kwa hiyo, mwathirika anaweza akaenda kwenye Tume ya Haki za Binadamu na akapewa msaada ili aweze kupata haki zake. (*Makof!*)

**SPIKA:** Tuendelea Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa. Naona yanafanana kwa sababu alikwambia atakwenda kwa nani si ndiko ulikosema.

**MHE. ENG. MOHAMMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa, katika vurugu zinazotokea wapo wale waliosababisha au wengine hawakusababisha lakini wapo ndani; na kwa kuwa, Polisi mpaka sasa hivi haijawa na taratibu za kufanya upelelezi kwanza halafu ndiyo mtu wakamweka ndani kwa kuwa wana ushahidi tayari.

Sasa watu wengi wanaathirika na matukio ya kuwekwa ndani wakavunjiwa kazi zao, wakaharibiwa utaratibu wao wa maisha halafu baadaye wanaachiliwa wanasema hawana hatia.

Je, Serikali sasa ipo tayari kufanya utaratibu wa kwamba yule ambaye amewekwa ndani bila hatia wanapomtoa ndani wakamlipe fidia ya muda wote ambao wamemweka ndani? (*Makof!*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli watu wengi wanachukuliwa kama alikuwa eneo la tukio au kama vyombo vya dola vinaona kwamba anahuksika kwa njia moja au nyininge lazima awekwe ndani, akishawekwa ndani wanachekechwa wale ambao wana makosa watabaki ndani na wale ambao hawana makosa watatolewa.

11 APRILI, 2013

Lakini kwa kweli Serikali haina utaratibu wowote wa kusema kwamba yule aliyewekwa ndani kwa muda au sheria yoyote inayosema kwamba yule aliyewekwa ndani kwa muda aweze kufidiwa na Serikali kwa kweli utaratibu huo wa kisheria haupo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na malalamiko kwa wananchi kwamba baadhi ya wanajeshi wamekuwa wakijihuisha katika vitendo vya uvunjifu wa amani kwa maana ya kuwapiga wananchi, lakini pia hapo hapo kumekuwa na malalamiko kwa wanajeshi wamekuwa wakitumia nguo zile kwa ajili ya kulichafulia jina Jeshi la Wananchi wa Taifa.

Je, Serikali imefanya utafiti wa kutosha katika suala hili ambalo mwisho wa siku linaleta uchonganishi kati ya rala na Wanajeshi ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana na nzuri katika ulinzi wa nchi yetu? Nini kauli ya Serikali katika hili? (*Makof!*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna raia ambao wanajifanya kwamba wao ni wanajeshi na kutumia nguo za Jeshi ili kufanya uhalifu na mambo mengine mbalimbali. Lakini mara nyingi au kisheria Mwanajeshi yeoyote akistaafu anatakiwa arudishe kila kitu pale Jeshini. Kwa hiyo, zile nguo zinazotumika mara nyingi ni wale wananchi ambao wanatumia nembo ya Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Ulinzi ili kufanya uhalifu.

Serikali mara zote inafuatilia masuala haya na inahakikisha kwamba yule ambaye anafanya udanganyifu wa aina hiyo mara nyingi tunachukua hatua za kisheria. Lakini tuwaase tu wenzetu wanajeshi kuhakikisha kwamba pale inapotokea vurugu wasitumie nguvu za ziada kuwadhuru wananchi. (*Makof!*)

11 APRILI, 2013

Na. 23

**Kutoa Elimu ya Tamko la Ulimwengu la  
Haki za Binadamu**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. JAMES F.  
MBATIA)** aliuliza:-

Tanzania imeridhia Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu (*Universal Declaration of Human Rights*) na kukubali kusambaza na kufundisha Tamko hilo katika shule na Taasisi zote za elimu:-

Je, Serikali imetekeleza kwa kiasi gani makubaliano hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)**  
alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, kama ifuatavyo:-

Serikali kwa kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikitoa elimu ya Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu ((*Universal Declaration of Human Rights*) katika shule na Taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Katika Maadhimisho ya siku ya Haki za Binadamu ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 10 mwezi Disemba.

- Kutembelea shule za Sekondari: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikifanya ziara za kutembelea shule za sekondari na kutoa Elimu kuhusu Haki za Binadamu.

11 APRILI, 2013

Pia kupitia siku hiyo ya Haki za Binadamu Tume ya Haki za Binadamu imekuwa ikiwashirikisha wanafunzi wa shule za Sekondari na kutoa elimu ya Haki za Binadamu.

Aidha, Tume imechapisha vijitabu vyatamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Tume iliweza kuchapisha nakala 3,000 za Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu (kwa lugha ya Kiswahili) na kuzigawa katika shule na taasisi mbalimbali nchini.

Aidha, upo mchakato unaosimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo na kushirikisha wadau mbalimbali ambao unapitla mitaala ya Elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari ambao umelenga kuboresha somo la elimu ya Haki za Binadamu mashulenii.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, wanafunzi wanaosoma Sheria Tanzania siyo lazima kusoma somo la Haki za Binadamu. Sas Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha somo hili la Haki za Binadamu linakuwa *compulsory* kwenye Vyuo ili waweze *to compete* kwenye Mahakama za Kimataifa ambazo zinashughulika na Haki za Binadamu?

La pili, la swali msingi linaliliza kuhusu kusambaza. Sasa Serikali ipo tayari kuingiza kwenye mtaala tamko nzima siyo Haki za Binadamu kama zilivyo kwenye Katiba, kwa sababu tamko linaeleza haki nyingi kuliko haki zilizopo kwenye Katiba?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, tamko la Haki za Binadamu ukilisoma kwa undani mambo mengi yapo kwenye Katiba yetu ya nchi.

Kwa hiyo, anayesoma Katiba ya Nchi mara nyingi ukiangalia na lile Tamko la Haki za Binadamu nayo imejirudia, na hiyo anayosema kwamba ni vyema tukaangalia hizo Haki za Binadamu zikaingia kwenye mitaala moja kwa moja hilo tutaliangalia na tutalifanyia kazi, tutaona umuhimu wa hilo tamko kuingia kwenye mitaala. Lakini ukisoma Katiba ya nchi vipengele vingi vinakidhi mahitaji ya tamko la haki za binadamu. *Makofii*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kati ya haki zinazotajwa kwenye tamko la Haki za Binadamu ni haki ya kupata elimu pamoja na haki ya malezi kwa watoto. Sasa Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine katika nchi yetu wamezagaa watoto wengi wakiwa wanaomba ombo; na kwa kweli wanalitia aibu Taifa letu. Sasa Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba watoto hao wanapata haki ya elimu na wanapata haki ya malezi bora?

**WAZIRI WA MAENDELEO WA JAMII, JINISIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, haki ya msingi ya elimu ya watoto inayotolewa katika nchi yetu kwa kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu ya msingi. Hivyo hivyo, tunaendelea katika shule za Kata.

Mheshimiwa Spika, pia ameuliza kuhusu watoto wanaozagaa nchi nzima. Suala la watoto waliozagaa nchi nzima ni kwamba wale watoto wanatakiwa wakae kwa wazazi wao na kila Halmashauri nchi hii inatakiwa ihakikisha watoto wake wanalelewa ipasavyo na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kulea mtoto kwanza ni la mzazi mwenyewe. Tunachokifanya Serikali ni kuhamasisha na kutoa elimu kuhakikisha kwamba wazazi wanakaa na hawa watoto na sasa tumetengeneza mkakati wa Wizara Mbalimbali kuhakikisha tunashirkiana kuhakikisha watoto hawa wanabaki katika malezi, kwa sababu suala la watoto linashughulikiwa na Serikali na wazazi wenyewe.

Kwa hiyo, kwa kupitia Bunge hili ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda kwenye Halmashauri Idara ya Maendeleo ya Jamii inapewa fungu la kutosha ili wafanye kazi hiyo kikamilifu. (*Makofii*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, haki za binadamu ni haki ya Kikatiba na maeneo mengi hapa nchini haki za binadamu zimekuwa zinakiukwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo mengi vijijini, Wilayani na kwenye Kata, na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inakabiliwa na tatizo kubwa la kutokuwa na ofisi kwenye ngazi ya Wilaya, ngazi ya Tarafa hadi ngazi ya Kata, hawana vyombo vya usafiri, hawana watalaaam maeneo ya vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba Tume hii ambayo inabidi ifanye uchunguzi ili haki ipatikane inasambaa maeneo yote ya nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Tume ya Haki za Binadamu haijasambaa katika Mikoa na Wilaya. Lakini kuanzia mwaka uliopita Tume ya Haki za Binadamu imeongezewa Bajeti kidogo ili iweze kukidhi mahitaji ya kuwasaidia wananchi katika sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, kukiwa na tukio lolote, Tume ya Haki za Binadamu sasa hivi angalau wana uwezo wa kufika katika sehemu mbalimbali na hili suala la Tume ya Haki za Binadamu tusiachie Tume peke yake kuna *NGO's* nyingi ambazo zina deal na masuala ya Haki za Binadamu kwa hiyo pia zishirikiane na Serikali kuhakikisha kwamba haki zinatendeka katika sehemu mbalimbali.

Lakini kwa sasa ukilinganisha na hapo zamani kwa kweli Tume ya Haki za Binadamu zinafanya kazi zake vizuri na Serikali inawawezesha kwa kiasi kikubwa ili waweze kufanya kazi zake vizuri.

Na. 24

**Wananchi Kuzuiwa Kuvua Samaki Ziwa Victoria**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Wananchi waishio kandokando ya Ziwa Victoria hawaruhuswi kuvua samaki wa kitoweo wala wa biashara hadi watumie vikubwa kama vile nyavu zenyenye matundu ya ukubwa wa inchi 8. Katika ziwa hilo kuna samaki wa asili wenye ukubwa wa inchi 1 hadi 3 kama vile obufulufulu au Obukeije (Kihaya) na sato na kadhalika ambao wana ukubwa wa inchi 5 hadi 6.

(a) Je, kwa kuwazuia wananchi kuvua samaki katika Ziwa hilo Serikali haioni kuwa ni kuwanyima haki ya kuvua samaki ambao kwa maumbile yao kamwe hawawezi kukua zaidi ya inchi 1, 3, 5 au 6?

(b) Kwa kuwa mazalio ya samaki wanaolindwa aina ya sangara yanafahamika. Kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi wavue maeneo au kwa wakati usiokuwa wa mazalio ya samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba wananchi waishio kandokando mwa Ziwa Victoria hawajawahi kuzuiwa kuvua samaki wa kitoweo wala wa biashara, bali wamehimizwa

kuzingatia uvuvi endelevu kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997, Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake Namba 3008 za mwaka 2009. Kanuni husika zinazosimamiwa na Serikali na Serikali zimeanisha aina ya zana zinazoruhusiwa kutumika kuvua aina mbali mbali za samaki kwa mfano samaki aina ya sangara, sato, dagaa na kadhalika.

Kanuni ya 58(1)(a) inakataza kuvua ama kumiliki au kuchakata kusafirisha nje ya nchi au kufanya biashara sangara wenyе urefu chini ya sentimita 50 na zaidi ya sentimita 85. Aidha Kanuni namba 58(1) (b) inakataza kuvua ama kushusha, kumiliki, kuchakata kusafirisha nje ya nchi au kufanya biashara ya sato wenyе urefu chini ya sentimita 25 na Kanuni 66(1) (k) kinakataza kumiliki kutumia ama kusababisha mtu kutumia kwa uvuvi wa dagaa nyavu zenye macho chini ya millimita nane.

Kanuni namba 66(3) kinakataza kumiliki kuingiza nchini, kuuza, kutumia au kusababisha mtu mwagine kutumia kwa uvuvi nyavu za makila (*gill nets*) zenye ukubwa wa nchi sita ama milimita 152.4 katika Ziwa Victoria isipokuwa hizi zinaruhusiwa kutumika kwa shughuli maalum.

(b) Mheshimiwa Spika, Sera, Sheria na Kanuni za uvuvi zinatamka waziwazi kwamba, aina zote za samaki, wakubwa wa wadogo, wavuliwe kwa namna endelevu. Kanuni namba 54 (1, 2) inataka maeneo maalum (*critical habitats*) kama *Rubafo Bay*, Ruiga, Mto Kagera na kadhalika wanakotagia au kuzalia na kukulia samaki yalindwe na kuhifadhiwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa samaki watakuwepo kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Hata hivyo, Kanuni husika zinaruhusu watu kuvua kwa kutumia ndoano za ukubwa namba 8,9,10 na 11 bila ya kutumia vyombo vya uvuvi hasa maboti ambayo yangeweza kuharibu maeneo ya mazalia ya samaki. Hivyo Serikali inawahimiza wananchi kutumia zana halali kama Sheria na Kanuni za Uvuvi zinavyo eelekeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri sikuyaelewa; hayaeleweki na ninaamini wananchi huko Ziwa Victoria hawakuelewa kabisa na hawakuambulia chochote.

Lakini pamoja na hayo napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kama ndivyo hivyo alivyosema kwamba hajjawahi kuzuia kuvua bado wanahimizwa kutumia uvuvi endelevu; inakuwa vipi wananchi wanapokamatwa wakivua mitumbwi yao na nyavu zao zinakamatwa, zinataifishwa na kuharibiwa kama hawazuiwi?

Swali la pili, kwamba wananchi wanazuiwa kuvua kwa vifaa hivi ambavyo vinasemekana kwamba haviruhusiwi kwanini Serikali inapenda kuzuia tu bila kuwapa njia mbadala, hakuna mafunzo, hakuna misaada hakuna mikopo. Je, wanapenda wananchi waendelee kuteseka na umaskini?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, moja kama nilivyosema kila sekta hasa iliyo muhimu katika uchumi kama hii ya uvuvi ina sera yake inayoongoza na kuelekeza, ina Sheria na Kanuni zake. Kama nilivyosema kwenye majibu ya swali la msingi ni kwamba vitu vilivyokatazwa hasa zana ambazo zaidi zitaharibu na kumaliza samaki kwa kipindi kifupi hivi vimekatazwa na Sheria na Kanuni na Serikali ipo kusimamia Sheria na Kanuni. Kwa kinachofanyika zaidi ni kuwashughulikia wale wanaovunja Sheria na Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ni kwamba Serikali imekuwa inatoa mafunzo na tuna wataalam wavuvi maafisa wa uvuvi katika ngazi ya Halmashauri na semina zinakuwa zikitolewa na hawa maafisa ugani na njia mbadala zinakuwa zinapendekezwa hasa zile za kuvua kwa sababu hakuna mtu angependa kuvua na sandihiki. Tuna jukumu la kutumia sie na kuhakikisha kwamba vizazi vingine vitatumia pia. (*Makof!*)

11 APRILI, 2013

Lakini kumekuwepo na dirisha katika Benki ya Rasilimali inayotoa mikopo kwa watu mmojammoja na katika vikundi kwa hiyo njia nzuri zaidi na Kagera hasa Mjini Bukoba watu wameanza kufuga kwa kuwa na madimbwi yao na wameweka samaki. Hii ni njia nzuri ya kuhakikisha watu wanaongezewa uwezo zaidi kwa kushikamana kuwa katika makundi kutafuta mikopo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri katika jitihada zako za kuhakikisha kwamba samaki hawaharibi au ufugaji au uvuvi endelevu Sheria za Tanzania zinawalazimisha wavuvi wa Tanzania katika Ziwa Victoria kutumia nyavu zenye macho makubwa kuliko milimita nane kwa sita. Waganda wanatumia macho madogo na hili ziwa letu halina mipaka hatimaye waganda wanakuwa wanakuwa na *advantage* katika uvuvi. Kwanini Serikali sasa isiweze ku-harmonize na kuhakikisha kwamba viwango vinavyotumika Uganda vilevile vinatumika Tanzania kusudi wote wavuvi wafaidi?

#### **WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, katika Ziwa Victoria chini ya Utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Sheria zinazotumika Kenya zimekuwa *harmonized* na tumekuwa na *programs* za pamoja. Kwa hiyo *advantage* ya waliokuwa nayo wenzetu wa Uganda labda ni kuwa na vyombo zaidi lakini kwa uhakika Sheria ni zilezile na mwaka huu tu mwanzoni mwa mwaka kulikuwepo na operesheni ya pamoja katika ya Tanzania Kenya na Uganda na watu waliokamatwa wakitumia nyavu kama nilivyoeleza wamekamatwa katika maeneo haya yote iwe ni upande wa Kenya Uganda na upande wa kwetu. Kwa hiyo, Sheria zimeoanishwa na kuhuishwa lakini labda katika zana zinazotumika huenda wenzetu wanabahati ya kuwa na vyombo vizuri na vinavyotumia teknolojia ya kisasa zaidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha dakika kumi na tano tulizozichukua ni zile zilizotumika kuwasilisha nyaraka. Kwa hiyo tunaendelea na kazi.

Tangazo la Kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Jerome Bwanausi anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Pius Msekwa C. Katibu tuendelee.

### HOJA ZA SERIKALI

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alimaliza kutoa hotuba yake kwa hiyo asubuhi hii kutakuwa na wawasilishaji hotuba wengi kiasi, kwa hiyo inaweza kutuchukua muda wa kutosha.

Kwa hiyo, naanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala au Mwakilishi wake dakika thelathini. Naomba wahusika wasogee kupunguza muda wa kutembea. Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine.

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za 99 (7) na 114 (11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Fungu 25 –

11 APRILI, 2013

Waziri Mkuu; Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 42 – Mfuko wa Bunge na Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata muda wa kutosha wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Utekelezaji huu ni wa manufaa kwa uhai na ustawi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Kamati ilipokea maelezo ya kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Taasisi zake yaliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Uratibu na Bunge. Katika maelezo yake, Pamoja na mambo mengine, Waziri alieleza Kamati kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi kufikia mwezi Juni, 2013 na matumizi kwa Mafungu yote. Aidha alieleza changamoto zinazoikabili Ofisi hii na Taasisi zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2012/2013 ilitengewa jumla ya kiasi cha sh, 175,948,033,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi Februari 2013 kiasi cha sh 102,851,194,348.86 zilipokelewa kutoka hazina. Kiasi hicho cha fedha kilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha katika kupitisha bajeti ya Mwaka 2012/2013 Kamati ilitoa ushauri, maoni na mapendekezo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Utaratibu wa kuleta vitabu vya bajeti Ofisi ya Bunge kwa mujibu wa kanuni ya 96(1) uzingatiwe. Kamati iliridhika kwamba utaratibu uliowekwa na kanuni ulizingatiwa ipasavyo kwa maelekezo yaliyotolewa kwa mawaziri wote kwamba ifikapo Marchi 23, 2013 vitabu viwe vimewasilishwa kwa Katibu wa Bunge.

(ii) Katika Idara ya Maafa serikali iliagizwa ipeleke chakula kwenye maeneo yenyе upungufu. Kamati ilielezwa kwamba Serikali imekuwa ikisambaza chakula kutumia Reli kwenye maeneo ambayo reli zinapita, aidha malori ya jeshi la ulinzi yamekuwa yaktumika kusafirisha chakula kwenye sehemu ambazo hazina reli, na wasafirishaji binafsi nao hutumika wakati reli inapokuwa mbovu na jeshi linapokuwa na shughuli nyingine.

(iii) Wafanyakazi wa kitengo cha maafa wajitahidi kufanya utafiti kubaini maeneo yenyе matatizo ya chakula. Tathmini ya hali ya chakula na lishe imekuwa ikifanywa na Idara ya Menejimenti ya Maafa ikishirikiana na Wizara ya kilimo chakula na ushirika, iwapo kuna sehemu zimeonyesha kuna upungufu mkubwa wa chakula serikali huwa inasafirisha chakula kwenda kwenye maeneo hayo.

Serikali kuongeza bajeti iliyotengwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili kutoa elimu ya vyama vya siasa kwa wananchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, kiasi cha sh. 63,550,000 kimetengwa kwa ajili ya kugharamia kuelimisha vyama vya siasa na umma wa watanzania.

(iv) Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta eneo la ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa. Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa inaendelea na juhudzi za kupata jengo jipya na kubwa zaidi katika kiwanja kilichopo au sehemu nyingine kubwa zaidi kukidhi ongezeko kubwa la watumishi walipo.

(v) Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha shughuli za kanda za uratibu wa shughuli za vyama vya siasa. Kwa sasa Ofisi ya Msajili ina kanda nne zinzoratibu shughuli za vyama vya siasa kanda ya Arusha, Dodoma, Mbeya na Mwanza. Aidha Ofisi imepanga kufungua Ofisi za kanda katika mkoa wa Tabora na Lindi katika Mwaka wa Fedha 2013/2014.

11 APRILI, 2013

(vi) Mfuko wa Bunge-Kuangalia uwezekano wa kuongeza muda wa wabunge kuitia na kujadili Bajeti za Wizara kwa ufanisi zaidi. Kamati itakayoshughulika na bajeti imeanzishwa, na muda wa Bunge la bajeti umebadilika na kuanza mwezi Aprili hadi Juni ili Mwaka wa Fedha unapoanza Julai bajeti ya kila Wizara iwe imepitishwa tayari kwa kuanza matumizi.

(vii) Ofisi ya Bunge kuweka utaratibu utakaowawezesha wabunge kuuliza maswali yakiwemo maswali kwa Waziri Mkuu badala ya utaratibu wa kuwahi mapema na kujiandikisha majina.

Marekebisho mbalimbali ya kanuni za Bunge yanaendelea ili kuweka utaratibu mzuri wa kila mheshimiwa Mmbunge kupata fursa ya kuuliza swali la papo kwa hapo kwa Mh, Waziri Mkuu.

(viii) Kuharakisha mchakato wakuwawezesha wabunge kuijunga na matibabu kwa njia ya Bima ya Afya ili kupunguza gharama za matibabu nje ya nchi.

Zabuni imetangazwa ili kumpata mshauri muelekezi atakaye ratibu zoezi la kupata mtoa huduma ili wabunge wapate huduma ya Bima ya Afya.

(ix) Ofisi ya Bunge iangalie uwezekano wa kununua mabasi mengine badala ya kukodisha.

Mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi haijapata fedha kwa ajili ya ununuzi wa mabasi hayo kwa kuwa bajeti imerudi kwenye ukomo wa bajeti ya Mwaka 2012/2013. Ofisi inatarajia kutenga fedha hizo tena katika bajeti ijayo.

(x) Tume ya taifa ya uchaguzi ieandae Bajeti kwa ajili ya uandikishaji wa wapiga kura kwenye Daftari la kudumu la wapiga kura. Serikali inashughulikia kupata fedha kwa ajili ya jukumu hilo.

(xi) Serikali kwa kushirikiana na Tume ya uchaguzi

kutoa elimu zaidi kwa wapiga kura na vyama vya siasa ili kupunguza vitendo vya uvunjaji wa sheria. Mapendekezo yamekubaliwa, elimu ya mpiga kura itatolewa na itakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge. Pamoja na utekelezaji wa majukumu yake Ofisi ya waziri Mkuu na Taasisi zake imekabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikikabiliwa na tatizo la ufinyu wa bajeti unaotokana na ukomo wa kibajeti. Changamoto hii imekuwa ni kikwazo katika kuleta ufanisi kwani majukumu mbalimbali yanashindwa kutekelezwa kutokana na kukosekana fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa; Kutotengwa kwa fedha za kushiriki chaguzi ndogo kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni changamoto kubwa katika ofisi hii kwani kunapotokea chaguzi ndogo ofisi hulazimika kutafuta fedha nje ya bajeti za ziada ili iweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutokuwa na jengo ambalo ni mali ya serikali na kulazimika kulipa gharama kubwa za pango na hivyo kuathiri utendaji wake wa kazi. Kwa mfano kiasi cha shilingi 234,387,648 hutengwa na Tume kulipia pango la nyumba kwa kila mwaka, Aidha Tume imekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi jambo ambalo huilazimu Tume ya Taifa ya uchaguzi kutumia watumishi wa muda nyakati za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kutokontaktewa kwa wakati fedha zilizopangwa kwa ajili ya kurekebisha daftari la Mpiga kura kunasabaisha daftari hilo kutoboreshwa kwa wakati. Hata hivyo, pale Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapopata fursa ya kuboresha daftari la wapiga kura kumekuwepo na mwiliitikio mdogo sana wa wananchi kujitokeza kuhakiki na kukagua majina katika vituo wanavyokuwa wamepangiwa.

11 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali; Katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali, mtambo pekee uliopo una uwemo wa kuchapa rangi nne tu, hivyo kuhitajika mashine nyingine ndogo sita au nane ili kusaidia kuchapa pande zote (*full colour on both sides*) ili kuwezesha kutoa kazi kwa muda mfupi.

Hata hivyo, japokuwa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkoo wa serikali inatengewa bajeti ndogo lakini imekuwa ikitoza asilimia 26 ya mapato yanayotokana na shughuli za upigaji chapa ambayo hutakiwa kupelekwa hazina. Kamati inashauri kwamba kwa kuwa bajeti inayotolewa kwa Ofisi hii ni ndogo ni vyema tozo la asilimia 26 lipunguzwe hadi kufikia 5% au kuondolewa kabisa kwa lengo la kuiwezesha Ofisi ya Mpiga Chapa ijitegemee yenye kutokana na mapato inayojingizia.

Mheshimiwa Spika, Aidha kamati inapendekeza Mpiga Chapa asijikite kwenye kuchapisha machapisho ya Serikali peke yake bali achukue tenda za machapisho yoyote yatakayostahili kuchapishwa kwenye Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali, kwani kwa kufanya hivyo taasisi hii itajiongezea kipato na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkoo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 imetengewa jumla ya sh, 233,664,757,000. Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo; Fungu 25-Waziri Mkoo, sh 6,386,889,000 zinaombwa kwa matumizi ya kawaida. Fungu 27-Msajili wa Vyama vya Siasa kiasi cha sh, 19,388,739,000 kwa matumizi ya kawaida, Fungu 37-Ofisi ya Waziri Mkoo kiasi cha sh 35,085,191,000 kinaombwa kwa matumizi ya kawaida na sh 43,871,152,000 kwa miradi ya maendeleo, Fungu 42-Mfuko wa Bunge kiasi cha sh. 123,401,059,000 ambapo kiasi cha sh, 100,000,000,000.000 zinaombwa kwa ajili ya kuendesha Mikutano ya Bunge na Kamati pamoja na shughuli nyingine za kiutawala. Na sh, 8,899,600,000 zitatumika kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, kufuatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014,kama yalivyotajwa kwa kila fungu, yafuatayo ni maoni na mapendekezo ya kamati:-

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu na Ofisi Ya Waziri Mkuu; fungu 25 na 37.

(i) Kutokana na ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa mara kwa mara na Waziri Mkuu anapokuwa ziarani katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kumekuwa na ugumu wa ufatilaji wa utekelezaji wa ahadi hizo.Hivyo basi Kamati inashauri kwamba idara inayoshughulikia ahadi za Waziri Mkuu ifatilie utekelezaji wa ahadi hizo mara zinapotolewa.

(ii) Kutokana na maafa mbalimbali ambayo yamekuwa yakijitekeza mara kwa mara, Kamati inashauri kuwa ni vyema kitengo cha Maafa kikaanzishwa katika kila Wilaya hapa nchini kwani ni vigumu kuratibu shughuli za maafa kutoka makao makuu. Aidha, wakati umefika kwa Kitengo cha maafa kujengewa uwezo wa fedha na rasilimali watu, ujuzi na vifaa, kwa lengo la kuisaidia nchi yetu kukabiliana na maafa ya aina mbalimbali yatakayoweza kujitekeza.

(iii) Serikali inatakiwa kusimamia ipasavyo na kuhakikisha kwamba jamii haijengi kwenye mikondo ya maji, kwa kufanya hivyo itapunguza madhara ya mafuriko yanayoweza kuleta maafa kwa jamii kwa kiwango kikubwa. Aidha Serikali ielimishe jamii ipasavyo ili ifuate taratibu za mipango miji wakati wa ujenzi wa makazi yao. Lengo ni kuweza kuacha nafasi pale inapotokea maafa kama moto magari ya uokoaji na ya kuzima moto yaweze kupita kwa urahisi kutoa huduma za uokoaji.

(iv) Kamati inashauri kwamba serikali inunue magari ya kuzima moto kwa kila wilaya hapa nchini. Ili kurahisisha shughuli za uokoaji na uzimaji wa moto pale maafa yanapotokea.

11 APRILI, 2013

(v) Serikali iharakishe ulipaji wa fedha za wenyeviti wa vijiji na vitongoji ambao walishiriki katika zoezi la sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2012, kwani pamoja na ahadi ya Waziri Mkuu kwamba wangalipwa mapema, lakini hadi leo hii hawajalipwa stahiki zao kama walivyoahidiwa.

(vi) Serikali iboreshe Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa lengo la kudhibiti taarifa na siri za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa Fungu 27 Kutokana na ufinyu wa Bajeti kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali kuongeza Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ili aweze kumudu majukumu yake lkiwa ni pamoja na kutafsiri Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992 pamoja na sheria ya uchaguzi ya Mwaka 2010, kushiriki kikamilifu katika chaguzi mbalimbali zikiwemo chaguzi ndogo za madiwani na kufuatilia kwa karibu kampeni za vyama vya siasa na kuhakikisha kuwa wagombea wanafuata sheria zote zinazoweka haki na wajibu kwa wagombea na vyama vyao vya siasa.

(ii) Kamati imepata taarifa kwamba serikali inakusudia kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa- *The political parties Act, CAP 258 R.E 2002*. Kamati inashauri kwamba pamoja na lengo zuri la serikali kutaka kuifanya marekebisho sheria hiyo, serikali isubiri hadi Katiba mpya itakapokuwa imeanza kutumika.

Mheshimiwa Spika Mfuko wa Bunge - Fungu 42. Kamati inashauri na kupendekeza ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Bunge iwaelimishe wabunge utaratibu unaotumika kuwapatia Wabunge matibabu pamoja na familia zao pale wanapokuwa wanahitaji huduma hiyo.

(ii) Ofisi ya Bunge iweke utaratibu unaohusu ziara za wabunge za ndani na nje ya nchi. Aidha, kamati inashauri kwamba ni vyema utaratibu uliokuwepo zamani kuhusu ziara za wabunge za ndani na nje ya nchi ukarejeshwa.

(iii) Kutokana na jukumu zito linaloikabili nchi kwa sasa ambalo ni uundwaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotazamiwa kukamilika ifikapo 26 Aprili 2014, Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ipewe nafasi ya kufuatilia mchakato mzima unavyofanyika.

(iv) Katika fedha iliyotengwa na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya ununuzi wa magari na vifaa vingine vyta usafirishaji, kamati inashauri kwamba ni vyema tathmini ya kina ifanyike ili kuweza kujua ni njia gani bora katika kununua au kukodi magari kwa ajili ya kuwashudumia wabunge.

(v) Ofisi ya Bunge ijitahidi jjenge Ofisi za Wabunge kwa kila jimbo na ziwekewe samani kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi wa Wabunge wakiwa majimboni.

Mheshimiwa Spika, Tume Ya Taifa Ya Uchaguzi - Fungu  
61. Kamati inapendekeza na kushauri ifuatavyo:-

(i) Serikali iongeze fedha za Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili iweze kulipa deni la sh 2,254,323,693 lilitokana gharama mbalimbali wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

(ii) Serikali iwawezeshe kifedha Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili waweze kuboresha Daftari la Kudumu la Mpiga Kura ambalo limekuwa likikabiliwa na changamoto nydingi, zikiwemo baadhi ya majina ya wapiga kura kutoonekana katika daftari, majina ya baadhi ya wapiga kura waliofariki kuendelea kuwemo kwenye daftari hilo, baadhi ya wapiga kura kujitokeza zaidi ya mara moja na kuwepo uwezekano wa kughushi kadi ya mpiga kura.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iandae daftari la orodha ya wapiga kura litakalotumika katika uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Jamhuri la Muungano kutoka Zanzibar, kwa kuwa utumiaji wa daftari la Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) unaelekeza sifa za ziada tofauti na zile zilizopo kwenye daftari la kudumu la *NEC*. Hivyo basi, tofauti hizo huwanyima wananchi haki ya kikatiba ya kuchagua/kuchaguliwa kuwa wabunge.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo limeendelea kuwa na changamoto nydingi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa jinsi anavyosimamia na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelawa na Wizara zote na pili kuwa msikivu na kuwa tayari kuyashughulikia matatizo ya Kamati za Bunge wakati zinapotekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Uongozi wake umesaidia kuweka mambo mbalimbali katika hali iliyo sawa na kulingana na uwezo wa Serikali. Pili, namshukuru kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati yangu wakati wa uchambuzi wa Bajeti kutuwezesha kufikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa William Lukvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na , Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wote, kwa maelezo na ufanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii.

Kipekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya sheria, utawala na sekta nydingine mbalimbali ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti na Mheshimiwa Mheshimiwa William M. Ngeleja ambaye ni Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wengine wa Kamati ni ni Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee na Mheshimiwa Fakharia K. Shomar.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza, Mheshimiwa Nyambari C.M.Nyangwine na Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh. (*Makofii*)

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Theonest Ruhilabake, Ndugu Haika Mtui na Tumaini Fungo, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, umejitahidi kutokutaja majina wala kumshukuru Katibu wa Bunge, Kwa hiyo nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

11 APRILI, 2013

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Utangulizi; kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Kamati mpya na kwa mara ya kwanza Wajumbe wake waliteuliwa na Spika tarehe 14 Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa mujibu wa ibara ya 63 (2) na 63 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, uwepo wa Kamati kama hii ni muhimu kwa madhumuni ya ufuutiliaji na usimamizi thabiti wa shughuli mbalimbali zinazotekelizwa na Serikali katika ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya matumizi ya fedha, kwa mujibu wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa miaka mitatu iliyopita, inakadiriwa kuwa wastani wa asilimia ishirini na tano (25%) ya Bajeti Kuu ya Serikali kila mwaka huenda kutumika katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri nchini hivyo usimamizi wa Bunge katika matumizi ya fedha za umma, hususan katika kuleta maendeleo kwa Wananchi, ni jambo ambalo Kamati hii inalipa uzito mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuanza utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeamua kujivekea vipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

(a) Menejimenti ya Huduma za Afya katika Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Mikoa kwa sababu Kamati inaanmini kuwa ustawii wa wananchi unaanza kwa kuwa na taifa lenye watu wenye afya; Menejimenti ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari.

(b) Huduma za maji na umwagiliaji chini ya Tawala za Mikoa na Halmashauri.

(c) Miundombinu inayosimamiwa na kuendelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kama vile barabara na miradi mingine.

(d) Masuala ya ardhi, maliasili, mazingira, mifugo, maendeleo ya Jamii na mengineyo chini ya Halmashauri.

(e) Kuhamasisha ubunifu wa mbini za kukuza uchumi na kupunguza umaskini; pamoja na mikakati ya kupanua fursa za ajira hususan kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza baadhi ya vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Kamati, itafanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri (*By-laws*) na Kanuni (*Regulations*) pamoja na Sheria Ndogo nyingine chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu. Zoezi hili litaenda sanjari na kuhamasisha Halmashauri zote nchini kutunga na kuboresha Sheria Ndogo zinazotekelzeza na kusimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati wanatambua imani uliyo nayo kwao na kwamba ufanisi wa Kamati utalisaidia Bunge kuwa chombo halisi cha uwakilishi wa Wananchi kwa kukidhi matarajio yao hasa kwa kuzingatia kuwa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii unahusika moja kwa moja na masuala na huduma muhimu zinazohitajika na kufuatiliwa na Wananchi. Kwa msingi huo, Wajumbe wa Kamati wamedhamiria kuhakikisha kuwa kazi yao inakidhi matarajio ya Wananchi, na si vinginevyo.

11 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Wa Majukumu Ya Ofisi Ya Waziri Mkuu, Tawala Za Mikoa Na Serikali Za Mitaa Kwa Mwaka Wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika Vikao vya Kamati za Bunge vilivyoanza tarehe 18 Machi, 2013 hadi tarehe 06 Aprili, 2013 Kamati ilianza kutekeleza majukumu yake kwa kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ni ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Dodoma pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, uamuza wa kutembelea miradi hii, ulitokana na nia madhubuti ya Kamati kupata picha halisi ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; lakini pia kuwa na maono halisi juu ya namna ya kuishauri Serikali katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 hususan katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 26 Machi, 2013 hadi tarehe 06 Aprili, 2013 Kamati ilipokea na kujadili, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 56 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Aidha, katika kipindi hicho, Kamati pia ilipitia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara kama ifuatavyo:-

1. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
2. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
3. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
4. Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
5. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
6. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
7. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
8. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;

9. Fungu 75 – Mkao wa Kilimanjaro;
10. Fungu 76 – Mkao wa Lindi;
11. Fungu 95 – Mkao wa Manyara;
12. Fungu 77 – Mkao wa Mara;
13. Fungu 78 – Mkao wa Mbeya;
14. Fungu 79 – Mkao wa Morogoro;
15. Fungu 80 – Mkao wa Mtwara;
16. Fungu 81 – Mkao wa Mwanza;
17. Fungu 54 – Mkao wa Njombe;
18. Fungu 71 – Mkao wa Pwani;
19. Fungu 89 – Mkao wa Rukwa;
20. Fungu 82 – Mkao wa Ruvuma;
21. Fungu 83 – Mkao wa Shinyanga;
22. Fungu 47 – Mkao wa Simiyu;
23. Fungu 84 – Mkao wa Singida;
24. Fungu 85 – Mkao wa Tabora; na
25. Fungu 86 – Mkao wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa umakini na kwa kujitolea kufanya kazi kwa masaa mengi, Wajumbe wa Kamati walichambua Taarifa na Bajeti za Mikoa yote ya Tanzania Bara na kutoa maoni na maagizo mahsus kwa kila Mkao. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa maoni, ushauri na maagizo hayo yatafanyiwa kazi katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Makusanyo; katika Mwaka wa Fedha 2012/203 Kamati ilielezwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiriwa kukusanya Jumla ya Shilingi 362,635,616,479/=.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2012, makusanyo yalikuwa wastani wa Shilingi 117,806,757,658/= sawa na asilimia thelathini na mbili nukta tano (32.5%) ya malengo yaliyowekwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI – 38%;

11 APRILI, 2013

- (b) TAWALA ZA MIKOA – 120%; na
- (c) MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA - 32%.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, makusanyo haya kwa upande wa Wizara na Mikoa, yalitokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, na kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yalitokana na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka hizo kutokana na vyanzo nya mapato viliviyokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, Changamoto; Kamati ilielezwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutimiza malengo waliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta kulikosababisha gharama za uendeshaji kuongezeka.

(ii) Upungufu wa Watumishi katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan katika Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Sheria na Ugavi.

(iii) Miundombinu duni ikiwemo, barabara, reli, mawasiliano, nishati ya umeme na uhaba wa maji safi na salama.

(iv) Ufinyu wa ukomo wa Bajeti (*ceiling*).

(v) Kukosekana kwa mwongozo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Ada za Leseni za Biashara.

(vi) Kukosekana kwa hospitali za mikoa na wilaya katika maeneno mbalimbali ya nchi yetu.

(vii) Tatizo la ulinzi na usalama hasa katika mikoa ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mapato na Matumizi, Kamati ilielezwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, illidhinishiwa jumla ya Shilingi Triliioni 3,639,968,434,000; ambapo Shilingi Bilioni 186,891,598,000 zilitengwa kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kugharamia Mishahara, Matumizi Mengineyo na Ruzuku za Taasisi zilizo chini yake, Mfuko wa Barabara na Mpango wa Maendeleo; Shilingi Bilioni 173,276,761,000 zilitengwa kwa ajili Tawala za Mikoa kugharamia Mishahara, Matumizi Mengineyo na Mpango wa Maendeleo; na Shilingi Triliioni 3,279,800,075,000 zilitengwa kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kugharamia Mishahara, Matumizi Mengineyo na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mapato katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ulikuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) – 58% (kufikia Februari, 2013);
- (b) Tawala za Mikoa – 54% (kufikia Desemba, 2012); na
- (c) Mamlaka za Serikali za Mitaa – 50% (kufikia Desemba, 2012).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika eneo la Mapato na Matumizi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto hizo:-

- (i) Upatikanaji usioridhisha wa fedha za Matumizi Mengineyo na hasa zile za Miradi ya Maendeleo;
- (ii) Matatizo katika usimamizi na udhibiti wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Kutowasilishwa kwa wakati fedha za wahisani, jambo linalosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(iv) Ukosefu wa ofisi na nyumba za Viongozi kwa baadhi ya Mikoa na Halmashauri kunakosababisha Serikali kuingia gherama za kupanga katika majengo ya taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji halisi wa Bajeti hiyo kati ya Julai, 2012 hadi Februari, 2013 ulijelekeza katika maeneo yafuatayo:-

(a) Utawala Bora hususan katika uratibu na uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala, ushiriki katika ushirikiano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, uhakiki na kuidhinishwa kwa Sheria Ndogo za Halmashauri, migogoro ya mipaka na masuala mengineyo;

(b) Ufuatiliaji na Uthamini hususan katika kaguzi za ndani, kaguzi za Miradi ya Maendeleo, mahudhurio katika kujibu hoja za Kamati za Bunge, masuala yanayohusu elimu na masuala mengineyo;

(c) Kujenga Uwezo hususan katika kutoa mafunzo mbalimbali na vikao vya kubadilishana uzoefu na taasisi nyingine za Serikali;

(d) Upelekaji wa Madaraka ya Maendeleo kwa Umma hususan katika upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mikoa, vikao vya mrejesho wa matokeo ya tathmini ya miradi na masuala mengineyo;

(e) Mifumo ya Habari, Teknolojia na Mawasiliano hususan katika ufungaji mfumo wa usimamizi Rasilimali Watu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, marekebisho ya Mfumo wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa (*LOG/N Tanzania*), Halmashauri mbalimbali kuunganishwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (*EPICOR*) na masuala mengineyo; na

(f) Uwezeshaji wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hususan katika ujazaji wa nafasi wazi za Wakuu wa

Idara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ukamilishaji wa ujenzi wa shule mbili kwa kila Halmashauri ili ziwe kamili (*Full Functional Secondary Schools*) na masuala mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu/Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa mapato kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri. Aidha, kumekuwepo na udanganyifu katika makusanyo, ambao kwa kiasi kikubwa umechangia kupotea kwa fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudzi za Wizara katika kuwawajibisha Watendaji wasio waaminifu katika matumizi ya fedha na inazitaka Tawala za Mikoa kufuata nyayo hizo. Kamati inatambua mamlaka hizo zina uwezo wa kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi ili kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Halmashauri zote nchini, kubadili mfumo wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo, kwa kuweka kiwango kikubwa cha fedha katika makusanyo ya ndani (*own source*) badala ya mfumo wa sasa unaotegemea zaidi fedha za wahisani (*foreign source*).

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi, Halmashauri zitajiwekea malengo halisi ya makusanyo na kutoa vipaumbele kwa miradi michache. Hali hii itasaidia pia kupunguza utegemezi kwa wafadhili ambao kwa sehemu fulani wamekuwa wakisita kutoa fedha kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa sababu ya kutowasilishwa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha mapema mazungumzo (*negotiations*) kuhusu Mfuko wa Barabara ili Mfuko huu uanze kufanya kazi na kuzsaidia Halmashauri zetu kujenga barabara zenye ubora.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi Triliioni 4,107,009,288,802 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) (Makao Makuu), Tawala za Mikoa na katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida, Shilingi Bilioni 194,359,133,000 zinaombwa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) (Makao Makuu) na Taasisi zilizo chini yake pamoja na Fedha za Mfuko wa Barabara; Shilingi Bilioni 143,790,302,000 zinaombwa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo katika Tawala za Mikoa; na Shilingi Triliioni 2,989,902,776,000 zinaombwa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, kiasi cha Shilingi Bilioni 778,957,077,802 zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kwa mchanganuo ufuataao:-

- (i) Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) – Shilingi Bilioni 84,326,931,802 (10.82%);
- (ii) Tawala za Mikoa – Shilingi Bilioni 54,031,618,000 (6.93%);
- (iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa – Shilingi Bilioni 640,598,528,000 (82.23%);

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, fedha inayoombwa imepangiwa kutekeleza kazi mbalimbali. Katika ngazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), mathalani, kiasi cha shilingi bilioni 128.9 kinategemewa kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuzifanya matengenezo barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Tawala za Mikoa,

fedha inayoombwa inategemewa kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya Mikoa na Wilaya mpya pamoja na kukamilisha Miradi ya Ujenzi na ukarabati wa Ofisi, Nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, fedha inayoombwa inategemewa kukamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hosteli, maabara na kupanua baadhi ya shule kwa ajili ya kuongeza kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 inakadirwa kufikia Shilingi Trillioni 17.3 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Waziri Fedha, katika Kikao cha *Briefing* kwa Wabunge kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 25 Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, Shilingi Trillioni 4.1 (sawa na 23.7%), zimetengwa kwa ajili ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Kwa msingi huo, Ofisi hii ina mchango mkubwa katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo zilizotengwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), 81% ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (ikiwa 58% ni Mishahara na 23% ni Matumizi Mengineyo) na hivyo basi, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kubaki na 19% tu. Jambo hili halikubaliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuja na maboresho ya Muundo wa Bajeti yake ili angalau fedha itakayotengwa kisheria kutekeleza Miradi ya Maendeleo isipungue 40%. Nitarudia, fedha itakayotengwa kisheria kutekeleza Miradi ya Maendeleo isipungue angalau asilimia 40 ya Bajeti Kuu ya TAMISEMI; na mahususi kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, isipungue 60% ya bajeti za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa husika, ili kutosheleza mahitaji halisi ya kuleta tija na ustawi kwa Wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kubajeti kwa muktadha huo, Serikali italazimika kufanya tathmini ili kuongeza vyanzo vya mapato na pia itakuwa makini kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa Bajeti yenyeye Muundo huu wa sasa, malengo ya kitaifa hususan katika kuwaletea Wananchi maendeleo kama huduma muhimu za afya, ujenzi wa zahanati na hospitali, miundombinu ya maji na barabara, ufgajji bora na wa kisasa na elimu bora, hayatafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukomo wa Bajeti (*ceiling*); wakati Kamati ikifanya uchambuzi wa Bajeti hii, ilibaini kuwepo kwa malalamiko mbalimbali kwamba baadhi ya Mikoa na Halmashauri zimewekewa kiwango cha juu cha makusanyo kisichowenza kufikiwa au kuwekewa kiwango kidogo ambacho kinaathili bajeti husika kimapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na HAZINA, wadau wa maendeleo, Mikoa pamoja na Halmashauri, ifanye tathmini juu ya uwezo wa kukusanya mapato ili malengo ya makusanyo yanapowekwa, mamlaka hizo ziweze kufikia malengo hayo kwa ufanisi ili kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imojiwekea malengo mbalimbali katika ngazi ya Wizara, Tawala za Mikoa na Halmashauri ili kukusanya mapato. Kamati inapendekeza kuwepo kwa ubunifu wa njia mpya za ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza pia kwamba, Serikali iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo (*property tax*) katika Majiji, Manispaa, Miji na Miji Midogo kwani fedha nyingi zinapotea kwa kutokusanywa kwa kodi hii. Kwa yale maeneo ambayo tathmini bado haijakamilika kuhusu thamani halisi ya majengo hayo ili kuweza kuweka viwango stahiki, Kamati inapendekeza kuwa fedha maalum itengwe ili kuwezesha

tathmini hiyo kukamilika kwa haraka ikiwa sahihi ili kodi hiyo ikusanywe katika Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Halmashauri nyingi zinakosa mapato kwa kutokusanya kisheria Kodi ya Ushuru wa Huduma (*Service Levy*) kwa sababu ya kutopigania haki zao za msingi, au kuyumbishwa na taarifa ama nyaraka za Wizara za Sekta husika, kuzuia kampuni kutolipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri husika kwa madai kuwa ushuru huo unalipwa katika makao makuu ya kampuni hizo ambayo huwa katika miji mikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) - (z) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, (*The Local Government Finances Act, CAP 290, R.E 2002*), Halmashauri zinastahili kutoza asilimia 0.3 ya mapato ghafi (*gross turnover*) ya kampuni zinazoendesha biashara katika eneo la Halmashauri kama kodi ya ushuru wa huduma (*service levy*).

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa, fedha inayotozwa hapa, ni kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa kampuni ambazo zinafanya biashara katika mipaka ya kisheria ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na Watendaji wa Wizara za Kisekta ambao kwa namna moja au nyingine wamehusika katika kuzikosisha Serikali za Mitaa mapato kwa kutoa nyaraka au na maagizo ya kuzizua Halmashauri kukusanya mapato kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili siyo geni masikioni mwa Uongozi wa Ofisi wa Waziri Mkuu (TAMISEMI), Kamati inaagiza kufanyike uchunguzi wa kina, hasa kwa kurejea Halmashauri ambazo zilipokea makatazo hayo kwa maandishi, na kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, ili kubaini watu hao na kisha hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi yao. Aidha, kwa makampuni ambayo yametumia mwanya huu kukwepa ushuru, yalipe malimbikizo ya ushuru

huo pamoja na adhabu ya kuchelewesha malipo ya ushuru husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa maelekezo yanayokinzana (*double standards*) katika utekelezaji wa Sheria ya Bunge, iliyotungwa kwa madhumuni ya kuzisaidia Halmashauri zetu kukusanya mapato ili kuweza kutoa huduma bora, ambapo sasa inahitajika juhudhi maalum za Halmashauri fulani ili kupatikana kwa haki hiyo kisheria. Jambo hili halikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri ambazo zimenufaika na ukusanyaji wa ushuru wa huduma (*Service Levy*) ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa Mgodi wa *Resolute*, na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa Kampuni zinazoendesha utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi Wilayani humo. Kamati inaziagiza Halmashauri zote nchini, kujifunza kutoka kwao na kuanza mara moja kukusanya ushuru huo. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) itoe Waraka kwa Halmashauri zote nchini kwamba zikusanye kikamilifu ushuru wa huduma (*Service Levy*) kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa suala la ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vilivyopo ni jambo ambalo Halmashauri zote nchini zinapaswa kufanya juhudhi za makusudi kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, zitumike vizuri na kwa uaminifu na hasa katika yale masuala ambayo yanaleta tija kama ufuatiliaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iongeze fedha kwa ajili ya uendeshaji na ununuzi wa vifaa vya tiba kwa ajili ya Hospitali ya Tumbi Kibaha, ambayo inakabiliwa na changamoto ya kupokea Wagonjwa wengi na majeruhi kutokana na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mikoa yote ambayo ina mifugo kwa wingi kuboresha majosho, kutenga maeneo ya malisho na kupanda nyasi ili wafugaji wasihami kutoka Mkoa mmoja kwenda mkoa mwine kutafuta malisho ili kuepuka migogoro kati yao na wakulima. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), zije na mpango wa pamoja wa kuisaidia Mikoa kuwa na ufugaji bora na wa kisasa ambao utaepusha uharibifu wa mazingira lakini pia kuboresha uchumi kwa Wafugaji hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Utumishi na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, isaidie Mikoa na Halmashauri kwa ajili ya kupanga mikakati na kuajiri Watumishi wenye sifa katika fani mbalimbali hususan katika Sekta za Afya na Elimu ili kuzijengea uwezo Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kutambua changamoto ya kukosekana kwa makazi kwa Watumishi hao, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, zifanye jitihada za makusudi kwa kushirikikiana na Taasisi za Fedha na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), katika kujenga nyumba za kutosha ili kujenga mazingira bora ya kuishi na kiutendaji kwa Watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kushirikiana na wadau wengine, kuandaa mfumo wa uratibu, ufuatilaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo. Mfumo kama huu, utapaswa kuzingatia vipaumbele vichache na vya haraka vyenye kutoa matokeo makubwa na ya haraka. Kwa utaratibu huu, Halmashauri zitawenza kugharamia utekelezaji wa miradi husika kutokana makusanyo ya ndani (*own source*), bila kutegemea sana kutokea Serikali Kuu na ufadhilli kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati ingependa kutoa mapendekezo yake mahususi ni katika tatizo la msongamano wa magari linaloikabili miji mikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudni ambazo zimeoneshwa na Jiji la Dar es Salaam kwa kuanzisha Mradi wa Mabasi yaendayo kwa kasi (*DART*). Hata hivyo, kuna haja ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, kutafuta mbinu za kupata fedha, hata kwa mikopo ya nje, ili kuweza kujenga barabara za juu (*fly-overs*) katika makutano makubwa ya barabara. Aidha, kuwepo na umakini katika kumpata Mshauri Mwelekezi (*Transaction Advisor*) mwenye uzoefu na uelewa katika udhibiti wa hasara za mfumo wa uendeshaji kisoko (*market risk management*) katika ubia (*Public Private Partnership*).

Mheshimiwa Spika, aidha, katika jitihada za kupambana na msongamano wa magari, Kamati inaishauri Serikali ije na Mpango Mkakati kwa Miji inayokua kwa kasi kama Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa tamko ni lini Serikali itahamia Mkoa wa Dodoma ili kuenzi juhudni za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere za kufanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Mpango wa kuhamishia shughuli za Serikali mkoani Dodoma utasaldia kupunguza tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nchini zimepewa mamlaka kisheria kutunga sheria ndogo kwa madhumuni yanayofana na yale ya kutungwa kwa Sheria za Bunge. Sheria hizi ni muhimu katika masuala ya utawala lakini pia ni muhimu katika kusaidia ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, Kamati imebaini kutohana na changamoto ambazo zimeainishwa na Mikoa na Halmashauri kwamba Halmashauri nyingi nchini zina sheria ndogo chache zinazohusu makusanyo, au zilizopitwa na wakati au kutohuwepo kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto zilizopo katika mchakato wa utungwaji wa Sheria Ndogo hizo, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuwekeza katika Idara ya Sheria na Wanasheria katika Halmashauri ili Sheria Ndogo zitakazotungwa au kufanyiwa mapitio, zikidhi hali halisi ya kiuchumi ya eneo husika. Aidha, Idara za Maendeleo ya Jamii zitumike ipasavyo kuhamasisha na kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali katika kuajiri Watumishi wapya, hususan katika Sekta ya Elimu. Aidha, Kamati inaitaka Serikali iboreshe maslahi na mazingira ya kufanya kazi kwa Walimu ili kuwapa motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Utumishi na Hazina iunde Kikosi Kazi Maalumu (*Special Task Force*) ili kuja na Mpango wa Dharura wa Ajira Katika Sekta ya Afya ili kuweza kutengeneza ajira mpya katika kada mbalimbali za Sekta ya Afya hususan katika Mikoa, Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo unapaswa kutoa majibu ya kina na yanayotekelezeka juu ya njia zitakazotumika kuwajengea mazingira bora (*incentives*) ya utendaji kazi Watumishi hao ikiwa ni pamoja na kuboresha maslahi yao kulingana na maeneo wanayokwenda kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, kutoa Mwongozo kuhusu Ada ya Leseni za Biashara inayopaswa kukusanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kuangalia upya na kuboresha maslahi ya Madiwani na Maafisa Tarafa kwa kuzingatia kuwa wao ndiyo wanaoishi na Wananchi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, ili kuleta maendeleo ya kweli na ya haraka kwa Wananchi, ni lazima yafanyike mageuzi makubwa katika maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kifikra (*change of mind set*) kwa Watendaji wa Serikali waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu amewabariki Watanzania. Hatuwezi kuendelea kufanya kazi kwa kuendelea kuamini kuwa mabadiliko yanaanza juu, na kuwa kila mtu atekelze wajibu wake, asiamini kuwa kuna mwingine atakuja kumfanya kazi yake. Mfumo wa namna hii, unasababisha Watendaji waliopewa dhamana hii, kufanya kazi kwa mazoea hivyo kusababisha urasimu, kukosekana kwa uwajibikaji na kukosekana kwa ubunifu. Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri wafungue vichwa vyao, wabuni Miradi ya Maendeleo yenye tija kwa Wananchi, na Viongozi wenye dhamana ya kufanya maamuzi wawaunge mkono.

(ii) Mheshimiwa Spika, Madiwani na Wabunge, wanao uwezo na dhamana ya kuwasimamia Watendaji wasiotekeliza majukumu yao kwa maendeleo ya Wananchi kwa kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika vikao vyote na hasa vile vya Kamati za Fedha (*Finance Committees*) na Baraza la Madiwani (*Full Council*).

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, wasiache kutekeleza jukumu la usimamizi unaochochaea maendeleo. Kamati hii kwa niaba ya Bunge, haitasita kufika eneo lolote ambalo lina harufu ya kutowajibika ili kufanya uchunguzi na kupendekeza hatua za kinidhamu kuchukuliwa kwa wale watakaobainika kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuleta ustawi wa Taifa letu bila uwajibikaji, na uwajibikaji unakuja pamoja na maumivu. Aidha, maumivu yatokanayo na kufanya kazi kwa bidii na kwa kujitolea ili kutimiza majukumu yako kwa ufanisi au maumivu yatokanayo na kuwajibishwa kwa kutotekeliza

majukumu yako kikamilifu. Maumivu yote haya mawili ni lazima ili maendeleo yapatikane.

Mheshimiwa Spika, Kamati haitasita kuwapongeza wale wote ambao wameonesha mfano kuwa maendeleo yanaweza kuletwa na sisi wenyewe. Nachukua fursa hii, kwa mfano, kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Singida na Sekretarieti ya Mkoa huo, kwa jitihada za kuleta maendeleo tunayoyazungumzia katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Singida.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali iangilie uwezekano wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali za Rufaa kwa kuzingatia Kanda za Kiutawala ili kutengwe fedha za kutosha kukamilisha miradi michache kwa muda mfupi.

(iii) Mheshimiwa Spika, Wananchi washirikishwe kikamilifu katika kutambua fursa walizo nazo ambazo zitachochaea ustawi na maendeleo ili kukabiliana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia kuhusu Azimio la Bunge Kuhusu Mfuko wa Ajira kwa Vijana. Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) itoe tamko la namna ambavyo wamejipanga kwa ajili ya kuratibu na kutenga maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa Azimio hili. Aidha, TAMISEMI, ishirikiane na Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo katika kuhakikisha Azimio liliopitishwa na Bunge linatekelezwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kutenga pesa kwa ajili ya kukamilisha Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Mfano, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma, Hospitali ya Mkoa wa Singida pamoja na Miradi mingine iliyopo katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kufanya jitihada za makusudi ili kukaa meza moja ya mazungumzo na Walimu ili kutatua matatizo yanayowakabili Walimu na

Sekta ya Elimu kwa ujumla ikiwa ni sehemu ya kutatua tatizo la kuporomoka kwa kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, ninamshukuru Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa; Naibu Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo, wakiongozwa na Ndugu Jumanne A. Sagini, Kaimu Katibu Mkuu na Ndugu Alphayo J. Kidata, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa John Paul Lwanji, Makamu Mwenyekiti, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu mengine ya Kitaifa. Aidha, kwa umuhimu mkubwa nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa uzalendo wao, maoni, busara, mahudhurio, utayari wao wa kufanya kazi bila kuchoka na ushauri uliosaidia kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, na kwa kutambua mchango wao katika kuipitia na kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dokta Hamisi Andrea Kigwangalla – Mwenyekiti, Mheshimiwa John Paul Lwanji – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Eugen Elishininga

11 APRILI, 2013

Mwaiposa, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Injinia Athumani Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza na Mheshimiwa Dokta Hadji Hussein Mponda.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge, Dokta Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati; Ndugu Yona Kirumbi na Ndugu Mossy Lukuvi, wakisaidiwa na Ndugu Abdallah Selemani, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati. Pia, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, jumla ya Shilingi 4,107, 009, 288,802.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa kutambua mchango wa Wajumbe wa Kamati yangu, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Muda umekwisha. (*Kicheko*)

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea. Kuna Mwenyezekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

Hayo Mafungu mnayoyataja yako kwenye Wizara zinazohusika, mnapoteza muda wenu bure. (*Makof*)

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 – Uwekezaji na Uwezeshaji kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupitia majukumu, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji pamoja na kupokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Uendelezaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2012/13 na Makadirio ya Bajeti 2013/14. Kamati ilijadili taarifa hizo kwa kina na hatimaye kuishauri Ofisi hiyo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji inatekeleza majukumu yake kwa kuratibu shughuli za Maendeleo ya Sekta Binafsi ikiwemo Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Kuwezesha Maendeleo ya Sekta Binafsi; Shughuli za Uwekezaji; Kanuni bora na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Sambamba na haya, ofisi hii inaratibu na kusimamia Taasisi zinazotekeleza majukumu mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Taasisi hizo ni pamoja na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*); Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*NEEC*); Baraza la Taifa la Biashara (*TNBC*) na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*TPSF*).

Mheshimiwa Spika, bado Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inakuwa mhimili wa Uchumi wa Taifa. Jitihada za kukuza uwekezaji, kuendeleza sekta binafsi na kuwezesha Wananchi kiuchumi ni masuala muhimu yanayohitaji msukumo wa kipekee kwa Taifa kuwa na uchumi imara. Katika kufanikisha haya, Serikali iliweza kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi Tanzania pamoja na kuratibu majadiliano na mashauriano baina ya wadau na makundi mbalimbali ya sekta binafsi kwa lengo la kuwa na sauti moja ya sekta binafsi nchini;
- Kukamilisha maandalizi ya Mkakati pamoja na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*National PPP Policy Implementation Strategy and Action Plan*);
- Kuratibu uainishaji wa baadhi ya Miradi inayokidhi vigezo vyta kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*;
- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004;
- Kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Government Roadmap for Improvement of Business Environment and Investment Climate in Tanzania*);
- Kuratibu utekelezaji wa Azma ya KILIMO KWANZA na Mpango wa kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini (*SAGCOT*);
- Kuendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kuititia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*); na
- Kuendelea kuratibu na kusimamia Programu na Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi tu ya majukumu yanayotekeliza na Ofisi hii. Hata hivyo, jitihada na msukumo mkubwa unahitajika hasa katika upande wa uwajibikaji wa watendaji na fedha zinazotolewa kufanikisha majukumu haya ili kuhakikisha tunafikia malengo tunayojojiwekea kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, Ofisi

ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji ilieeleza Kamati kuwa inakabiliwa na changamoto kadhaa zifutazo:-

- Kiwango cha Bajeti kinachotengwa hakikidhi utekelezaji wa majukumu ya uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi, jukumu ambalo ni muhimu katika kukuza uchumi;
- Uwezo wa Serikali katika kutunisha Mifuko ya Uwezeshaji ni mdogo sana kuwawezesha Wananchi kiuchumi na pia kumekuwa na utitiri wa Mifuko mingi ya uwezeshaji ambayo haijaweza toa tija;
- Kuwepo kwa Sera, Sheria na Mifumo ya Kitaasisi inayokinzana na mazingira wezeshi kwa sekta binafsi;
- Urasimu katika baadhi ya Taasisi za Serikali katika kuwashudumia wawekezaji ili kutoa huduma bora na za haraka bado ni changamoto kubwa;
- Miundombinu hafifu ya kiuchumi na kijamii inafanya jitihada za kuendeleza sekta binafsi, uwekezaji na uwezeshaji kuwa ngumu;
- Uhaba mkubwa wa miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme, barabara, reli na bandari, hali inayoongeza kwa kiasi kikubwa gharama za kufanya biashara na kuwekeza nchini;
- Ufanisi mdogo wa Mahakama katika kutoa hukumu za kesi zinazohusu masuala ya biashara na uwekezaji nchini;
- Ushindani mkubwa wa upatikanaji wa mitaji kutoka nje. Kila nchi inajitahidi kuvutia wawekezaji ili kuweza kukuza uchumi wa nchi zao; na
- Mikoa mingi nchini bado haijaweza kuandaa mikakati ya kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Mikoa yao. Aidha, bado kuna miundombinu hafifu na hivyo kusababisha Miradi mingi ya Maendeleo kuwekezwa

katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Pwani na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yamelenga kuimarisha sera na mifumo mizuri ya kufanya biashara, uwekezaji na uwezeshaji wa Wananchi wenyе kipato cha chini ambao utachochea ukuaji wa uchumi jumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na misingi na shabaha ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika utekelezaji wa Bajeti kwenye Fungu la 37 ambazo kimsingi zinalenga kutatua changamoto zinazopaswa kuangaliwa na Serikali kwa kipindi cha Mwaka huu wa Fedha wa 2013/2014 katika masuala ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ndiyo yatakayosaidia katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa inayoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji ni upungufu wa bajeti na fedha kuchelewa kufika kwa wakati na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. Kamati inashauri Serikali kuongeza kiwango cha Bajeti kinachotengwa kwenye Fungu hili liweze kukidhi utekelezaji wa majukumu ya uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi, jukumu ambalo ni muhimu katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Msingi Mkuu wa Serikali katika masuala ya uwekezaji na uwezeshaji ni kuongeza jitihada za kukuza uwekezaji hasa kwa kuititia Sekta Binafsi pamoja na kuwawezesha Wananchi kiuchumi. Jukumu hili lazima liambatane na kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi ili kuhakikisha kuwa inakuwa mhimili mkuu wa ukuaji wa uchumi. Hatua hizi zitatusaidia kufikia malengo yetu ya kujenga uchumi imara utakaohimili ushindani wa ndani na nje ya nchi na hivyo kufikia lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati kama inavyoelekezwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/

2016) na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misamaha ya kodi tunayotoa kila mwaka kwa wawekezaji wa ndani na wale wa nje ya nchi, bado nchi yetu haifanyi vizuri katika kuhakikisha inajenga mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji nchini. Kwa mujibu wa taarifa inayoandaliwa na Benki ya Dunia '*Doing Business 2013*'; kati ya nchi 185 Duniani, Tanzania ni nchi ya 134 katika kurahisisha mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara (*Ease of doing business*). Ni dhahiri kuwa, hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza ili kuongeza kasi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kamati bado inaishauri Serikali kuhakikisha inapitia na kufanya marekebisho ya Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazokinzana na kuleta urasimu mkubwa katika kufanya shughuli za biashara na uwekezaji, kufanya tathmini Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji nchini pamoja na kuondoa tatizo la ucheleweshaji au kutokutoa maamuzi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, Serikali inajitahidi katika kukabiliana na tatizo la ajira hasa kwa vijana, kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza fursa za ajira, Kamati inaona bado hatua hizo hazitoshii na hazijawekewa msukumo na usimamizi wa kutosha hasa katika upande wa kuboresha mazingira ya kisera na kisheria kuwezesha sekta binafsi kukua; kupanua huduma za kibenki hasa vijiji, kutoa mikopo ya muda mrefu kwa Wananchi wenyewe kipato cha chini hasa ya biashara na ujenzi wa nyumba na makazi pamoja na kuwezesha Wananchi kupitia programu mbalimbali za uwezeshaji.

Kamati inatoa msisitizo kwamba, Serikali iongeze juhudii katika maeneo hayo pamoja na kusimamia ipasavyo taasisi mbalimbali zinazosaidia kuongeza ajira hasa kwa vijana kama vile *VETA*, *TASAF*, *SELF*, Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*), Taasisi ndogo za Fedha, *VICOBA*, Benki za Kijamii na Mifuko ya Udhagini wa Mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inafurahishwa na jitihada za Serikali za kukuza uchumi. Hata hivyo, ukuaaji huu bado haujaweza kumsaidia mwananchi wa kawaida kupunguza umaskini wa kipato. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa jitihada za kupunguza umaskini zinawezekana tu pale ambapo rasilimali za Taifa zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yanawagusa Wananchi wengi katika shughuli zao za kila siku hasa Sekta ya Kilimo, Uvuvi, Ufugaji na uzalishaji viwandani, ambazo zinaajiri Wananchi wengi. Uwekezaji kwenye maeneo haya utalisaidia Taifa kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo na kuongeza uwezo wa Serikali katika uendelezaji na uboreshaji wa huduma za jamii hasa afya, elimu na maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inashauri Serikali kuweka msisitizo kwenye eneo la Sekta ya Fedha hasa katika kuendeleza upatikanaji wa mikopo na hatua nyingine za uwezeshaji. Pamoja na kuongezeka kwa mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi, sehemu kubwa ya mikopo hiyo bado haiwafikii walengwa na hivyo *impact* yake kutoonekana katika kukuza uchumi na hivyo kumwezesha mwananchi wa kawaida. Utitiri wa Benki nchini takriban 51 bado hautoi nafuu ya riba za mikopo na hivyo kuwa kikwazo kikubwa katika kumkwamua Mwananachi kiuchumi. Wananchi wengi vijiji ni hawana elimu ya kutosha kuhusu upatikanaji wa mikopo pamoja na uwekaji wa akiba. Hii inatokana na kwamba, benki nyingi zipo mijini badala ya vijiji na kwamba Serikali kuititia *BOT* hajjaweza kutoa elimu ya kutosha pamoja na kusimamia ipasavyo suala hili. Kamati inaona kuwa ni wajibu sasa Serikali kuhakikisha inaweka msukumo zaidi katika kukuza na kuimarisha mfumo wa huduma za kifedha vijiji; mfumo ambao utazingatia Taasisi za Kati za Kifedha na Mabenki (*Linkage Financing*) ili kuboresha upatikanaji endelevu wa huduma za kifedha vijiji.

Mheshimiwa Spika, bado hali ya uzalishaji wa umeme nchini hajakidhi mahitaji ya eneo la uwekezaji kwa upande wa viwanda na biashara, hali inayopelekea baadhi ya viwanda nchini kutumia magogo kama nishati mbadala wa upatikanaji wau meme na hivyo kuathiri mazingira. Mahitaji

ya umeme ni makubwa kuliko upatikanaji wa umeme kwenye Gridi ya Taifa. Hali hii ya ukosefu wa umeme wa uhakika inasababisha kukosa wawekezaji. Aidha, hali hii inasababisha hasara kubwa kwa wenye viwanda kutokana na gharama kubwa za uzalishaji na pia kupunguza fursa za ajira. Tatizo la umeme wa uhakika lisipotatuliwa ipasavyo litapunguza kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo kupunguza ukuaji halisi wa Pato la Taifa kwenye sekta za uzalishaji viwanda, ujenzi na biashara. Tafiti zinaonesha kuwa gharama za upungufu wa umeme viwandani zinaongeza gharama ya uzalishaji kwa asilimia 2 hadi 15.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijaonesha nia ya kweli ya kutatua tatizo hili la umeme kwa kutumia vyanzo vya uhakika kama vile makaa ya mawe, jua, upepo na gesi asilia. Kama Serikali itaamua kuwekeza kwenye vyanzo vya uhakika vya makaa ya mawe yallyopo Ngaka (Mbinga), umeme wa upepo (Singida) au umeme wa gesi (Mtwara) itakuwa imeokoa kiasi kikubwa cha fedha ukilinganisha na chanzo cha umeme wa mafuta kinachotegemewa sasa kuzalisha umeme ambacho ni gharama kubwa kwa Serikali. Uwekezaji huu uendane na ujenzi wa njia mpya za umeme (*Transmission line*) za uhakika kwa mfano kutoka Makambako mpaka Songea ambayo inategemewa kugharimu kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 64 na hivyo kupeleka Megawati 120 – 400 kwenye Gridi ya Taifa. Hii itasaidia kupunguza gharama za uzalishaji viwandani na hivyo kuwapa nafuu wazalishaji na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, bado idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha Wananchi wenye kipato. Programu mbalimbali za kuondoa umaskini na zile za kuwawezesha Wananchi kiuchumi kama vile MKUKUTA, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali (*NEDF*); Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*YDF*); Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*); Mfuko wa Rais wa Kusaidia Wananchi (*PTF*); Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo (*SELF*); Mpango wa Udhamini wa

Mikopo kwa Mauzo ya Nje (*Export Credit Guarantee Scheme*); Mpango wa Kudhamini Mikopo kwa Miradi Midogo na ya Kati (*Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme – SME-CGS*) na mingine mingi, yenyе lengo sahihi la kuwasaidia na kuwawezesha Wananchi wengi wenye kipato cha chini, bado hazijaweza kuwanufaisha Wananchi kwa kuwa utekelezaji wake hausimamiwi ipasavyo, hivyo kutowafikia walengwa. Aidha, baadhi ya Mifuko hii mitaji yake ni midogo kuweza kutosheleza mahitaji yote. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufuatilia na kuhakikisha malengo ya Mifuko hii yanafikiwa ikiwemo kusaidia kuongeza mitaji ya mikopo hiyo pamoja na kuhakikisha kuwa inaongozwa na watu wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, elimu bora itolewe kwa wadau mbalimbali wanaoshiriki kwenye shughuli za uwekezaji kuititia utekelezaji wa Miradi chini ya utaratibu wa *PPP* katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Elimu inahitajika ili waelewe namna ya kutayarisha Miradi inayokidhi vigezo na hivyo kutekelezwa kwa kuzingatia utaratibu na muundo wa *PPP*. Takwimu zinaonesha kuwa, jumla ya Miradi 125 yaliyowasilishwa kwa kuzingatia utaratibu wa *PPPI* meshindwa kukidhi vigezo. Aidha, Miradi minne ndiyo imekidhi vigezo na sasa inafanyiwa uchambuzi. Kamati inaona kuwa hali hii inaashiria kuwa bado wadau wengi hawajaelimika vyta kutosha kuhusiana dhana nzima ya utaratibu wa Miradi ya *PPP* pamoja na sheria yake. Kamati inashauri kuwa, jitihada za makusudi zifanyike katika kuelimisha Wananchi ili Miradi hii iweze kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kuiondolea Serikali mzigo wa kufanya kila kitu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kituo cha Utoaji Huduma kwa Pamoja (*One Stop Centre*) katika Bandari ya Dar es Salaam, ambacho kinahusisha Taasisi, Wakala na Wizara zinazohusika na utoaji wa vibali na leseni kwa mizigo inayopitia bandarini. Dhumuni kubwa la kituo hiki ni kupunguza urasimu na ucheleweshaji wa uondoaji mizigo bandarini ambaao umekuwa kikwazo kikubwa cha biashara nchini na kwa nchi jirani zinazopitishia

mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Pamoja na umuhimu wa uanzishwaji wa kituo hiki, Kamati hajjaridhi na maandalizi yaliyopo sasa kwa sababu kuu zifuatazo:-

(i) Ofisi inayotumiwa sasa kama One Stop Centre ni ndogo na haikidhi mahitaji na utoaji wa huduma unavyostahili;

(ii) Kuwa kuna baadhi ya Taasisi au Wakala hawashirikiani vizuri au wanasuasua kufanya kazi kwenye kituo hiki;

(iii) Bado kuna ugumu wa kisheria kuziunganisha Taasisi zote kufanya kazi pamoja na kwa ufanisi; na

(iv) Serikali bado hajatoa msukumo wa kutosha kusimamia Kituo hiki kufanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaondoa vikwazo vyote hivi na kusimamia ipasavyo shughuli zote za Kituo hiki ili kuweka mazingira wezeshi ya biashara kupitia bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Utekelezaji wa KILIMO KWANZA umeweza kuainisha kwa ufasaha utekelezaji wa nguzo kumi kama msingi mkuu amba Serikali pamoja na Wadau wa KILIMO KWANZA wanapaswa kufuata na kuhakikisha nguzo hizo zinatekelezwa kwa ufanisi. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa nguzo ya pili ya utekelezaji wa shughuli za KILIMO KWANZA ihakikishe kuwa inatekeleza azma yake ya kuimarisha msingi wa Mabenki ya Wananchi katika mikoa kama ilivyokusudia. Aidha, Kamati inatoa msisitizo kwa sekta binafsi kupitia *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* kuendelea kuhamasisha sekta binafsi iongeze juhudzi za uwekezaji katika Sekta ya Kilimo kuanzia ngazi za chini kwa kuwa Sekta hii ndiyo mkombozi wa Wananchi wengi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Uwekezaji na Uvezeshaji, Mheshimiwa Dkt.

Mary Michael Nagu (Mb), Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa, ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstun Luka Kitandula - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengyea Kamani, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa David Zakaria Kafulila, Mheshimiwa Shawana Bukhet Hassan, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Vick Pascal Kamata, Mheshimiwa Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Josephine Jonson Genzabuke, Mheshimiwa Eng. Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa Mohamed Hamis Misanga.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Katibu wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Ndugu Michael Kadebe, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 – Uwekezaji na Uvezeshaji, kama alivyowasilisha mto hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, umezamia kwenye *issues*. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI au mwakilishi wake. Tulisema wanaowasilisha wakae karibu mbona huwa wanakaa *front bench*; kwa nini wanafanya hivi?

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) na (11), Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevy - Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kuidhinisha maombi ya fedha kama yalivyowasilishwa na mto hoja.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii mpya yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge za mwaka 2007 kuwa ni kuchambua Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara na Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevy nchini. Vilevile Kamati ina wajibu wa kuzisimamia na kuzishauri Tume hizo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao. Katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 3 Aprili, 2013 Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam na kupokea taarifa ya Tume zote mbili kuhusu utekelezaji wa bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti hizo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Tume hizo kwa mwaka wa fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, Kamati ilipokea muhtasari wa kazi zilizofanywa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kipindi kilichopita pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza mwaka 2012/2013 ziliwasilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevyta ilitengewa kiasi cha Shilingi 1, 362, 388,400. Kati ya fedha hizo, Shilingi 362,388,400 zilikuwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za matumizi ya kawalda zillizopokelewa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013 ni Shilingi 666,664,000 na matumizi halisi hadi tarehe hiyo yalikuwa Shilingi 492,005,552.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zilitumika kutekeleza kazi mbalimbali zilizopangwa, baadhi ya kazi hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- (i) Kuendesha operesheni za ukamataji wa dawa za kulevyta nchini;
- (ii) Kuendesha operesheni za kubaini na kuteketeza mashamba ya bangi ambapo kuanzia Julai, 2012 hadi Februari, 2013 jumla ya ekari 184 za mashamba ya bangi na kilo 3,200 za bangi kavu ziliteketezwa;
- (iii) Kuwezesha asasi za kiraia kushiriki katika udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevyta kwa vijana na jamii kwa ujumla; na
- (iv) Kuratibu programu ya utoaji tiba na huduma za utengamano kwa watumiaji wa dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha

2012/2013, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,180,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha zote hizo ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 fedha zote zilizokuwa zimepokelewa ni Shilingi 903,675,000 na kiasi cha Shilingi 276,325,000 zilikuwa zimesalia hadi kufikia mwezi Machi, kiasi hicho kitaendelea kutumika katika kipindi cha Mwaka wa Fedha uliosalia.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Miradi ya Maendeleo zimetumika kutekeleza majukumu ya msingi ya Tume ambayo yanajumuisha kazi zifuatazo:-

(i) Tume imeweza kusaidia kuanzishwa kwa kituo cha kutoa tiba ya *methadone* kwa watumiaji wa *heroin* katika Hospitali ya Mwananyamala;

(ii) Kuwezesha ukarabati wa jengo litakalotumika kutoa tiba ya *methodone* kwa watumiaji wa *heroin* katika Hospitali ya Temeke; na

(iii) Tume imewezesha utoaji wa mafunzo kwa watoa huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevyा.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyा inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi;

(ii) Wananchi kutoshiriki kikamilifu katika vita dhidi ya dawa za kulevyा kwa kuhofia kudhuriwa na wafanyabiashara wa dawa za kulevyा ambao inajulikana kwamba wana pesa nyingi;

(iii) Ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevyा nchini; na

(iii) Bajeti ndogo inayotengwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy - Fungu 91, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 5,800,286,000; katika fedha hizo shilingi 3,002,286,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo mishahara itatumia shilingi 350,548,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 2,651,738,000. Aidha, jumla ya shilingi 2,798,000,000 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 350,000,000 na fedha za nje ni shilingi 2,448,000,000.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwa zitatumika kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kutekeleza miradi ya afua za UKIMWI mionganini mwa wanaojidunga sindano;

(ii) Kuendeleza uanzishwaji wa vituo vya matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevy katika Manispaa za Temeke na Ilala; na

(iii) Ukarabati wa majengo, ununuzi wa dawa na vifaa kwa ajili ya vituo vya matibabu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupitia mpango wa bajeti wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, vita ya kupambana na dawa za kulevy na ufinyu wa bajeti ni ukweli usiofichika kwamba, wafanyabiashara wa dawa za kulevy ni watu wenye pesa nyingi na mbinu za kisasa za kuingiza na kuuza dawa za kulevy nchini na nje ya nchi. Aidha, sisi sote ni mashahidi wa namna dawa za kulevy zinavyozidi kuathiri vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu na kwa mujibu wa habari hiyo kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kupigana na vita hivi haramu vya dawa za kulevy, ni lazima ihakikishe inaiwezesha Tume hii kwa kutengewa bajeti ya kutosha kukabiliana na watu hawa ambao tunaweza kuwaita kwamba ni majasusi.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa sasa wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI uko Dar es Salaam pekee na watumishi waliopo ni wachache ukililinganisha na ukubwa wa tatizo. Kamati inapenda kusitiza kuwa, janga la dawa za kulevyta ni la nchi nzima na kwa kuwa suala la dawa za kulevyta ni mtambuka na watumiaji wengi hasa wanaojidunga sindano wana uwezekano wa kupata maambukizi ya UKIMWI. Kamati inashauri, Sekta ya UKIMWI na Sekta ya Dawa za Kulevyta ziunganishwe kwa kuwawezesha kielimu na kifedha waratibu wa UKIMWI walioko mikoani ili waweze kutekeleza majukumu ya UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevyta kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Sheria iliyoanzisha Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevyta kuitwa na wakati. Sheria Na. 9 ya Mwaka 1995 ilipoanzishwa illainisha tatizo la dawa za kulevyta kuwa la kiuchumi, kijamii na kiafya. Aidha, Sheria hili inataja baadhi ya majukumu ya Tume kuwa ni pamoja na kukamata bila kushtaki, Kamati inashauri ili kuongeza ufanisi wa Tume ni vyema Sheria hili ikarekebishwa ili iendane na wakati. Aidha, Kamati inapendekeza Tume iwezeshwe kwa kupewa meno ili iweze kukamata na kushtaki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inathamini mchango mkubwa unaofanywa na Tume hili, pamoja na kwamba, Tume inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, vitendea kazi na upungufu wa rasilimali watu. Tume imeweza kufanikiwa kukamata wafanyabiashara wa dawa haramu za kulevyta na kukamatwa kwa kiasi kikubwa cha dawa hizo. Kamati inaamini kuwa, Tume ikiwezeshwa kwa kuongezewa bajeti na motisha kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira hararishi sana, kuna uwezekano mkubwa wa kushinda vita ya dawa za kulevyta na kuokoa kizazi chetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutumia fursa hili kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubali kuwa mlezi wa vijana walioamua kuacha kutumia dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2012/2013, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa jumla

shilingi 13,143,351,000; kati ya fedha hizo, shilingi 2,799,016,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 1,303,882,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,495,134,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Tume ya Kudhibiti UKIMWI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 15,334,355,200 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha zote hizo ni za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013, jumla ya shilingi 6,319,613,946.74 zilipokelewa. Shilingi 3,507,844,049 zilitumika, matumizi ya fedha hizo ni sawa na asilimia 35 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Tume ya Kudhibiti UKIMWI imefanikiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Tume imeweza kuimarisha uratibu wa shughuli za UKIMWI mikao kwa kuwezesha waratibu 21 wa mikoa wa *TACA/DS* kifedha na kiutaalamu.

Mheshimiwa Spika, pili, Kuainisha mambo ya kisheria katika masuala ya UKIMWI yanayokwamisha mchango wa sekta binafsi katika afua za UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu, kumalizia ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya Tume liliopo Mtaa wa Luthuli Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, utegemezi wa bajeti kutoka kwa wahisani hususan kwenye Miradi ya Maendeleo, umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa. Changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Utegemezi wa asilimia mia moja ya fedha za UKIMWI kutoka nje ya nchi; na

(ii) Kutokuwa na uhakika wa fedha zinazotolewa na wadau wa maendeleo na hata zikitolewa huwa ni pungufu na hazifiki kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa kujiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi yote muhimu yanayohusu uanzishwaji wa Mfuko wa UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano (2013/2014 - 2017/2018), Mpango wa Maendeleo wa Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara unalenga katika kusimamia uratibu wa utekelezaji mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa sekta mbalimbali ili kupunguza kasi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI nchini. Ili kuanza kutekeleza mpango huu katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, kiasi cha shillingi 17,893,505,000 kinaombwa kwa ajili ya Fungu 92, ambapo kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shillingi 2,559,170,000 na fedha za matumizi ya maendeleo shillingi 15,334,335,000.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo za maendeleo, zinazoombwwa zote ni za nje, hakuna fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwwa zitatumika kutekeleza malengo ya Tume kwa mwaka 2013/2014 ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kufanya mapitio ya matumizi ya fedha za umma zitakazotengwa na kutumika katika afua za UKIMWI;

(ii) Kufanya ufuatiliaji kwenye Halmashauri kwa kufuatilia matumizi sahihi ya fedha. Naomba kurudia hapa, kufanya ufuatiliaji kwenye Halmashauri kwa kufuatilia matumizi sahihi ya fedha;

(iii) Kufanya mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Jinsia

ili uendane na Mkakati mpya wa Taifa wa Mapambano ya UKIMWI;

(iv) Kuandaa na kusambaza taarifa ya mwaka ya mwitikio wa kitaifa;

(v) Kuimarisha uwezo wa vikundi vyta akina mama wanaoishi na Virusi vyta UKIMWI;

(vi) Kufanya vikao vyta uraghibishi kuhusu masuala ya UKIMWI mahala pa kazi kwa Idara 30 za Serikali; na

(viii) Kuandaa na kufanya mukutano na Viongozi wa Vyama vyta Siasa ili kuwahamasisha wahusishe masuala ya UKIMWI katika llani za Uchaguzi za vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili makadirio ya Bajeti ya Tume na kuridhika nayo na sasa naliomba Bunge lako likubali kujadili na kuitisha maombi hayo yenye jumla ya Shilingi 17,893,505,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuujadili Mpango na Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa sana na Bajeti ya Serikali kwa kuendelea kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, licha ya ukweli kwamba, wahisani wengi wameendelea kujitoa kufadhili Miradi ya UKIMWI na kwa wale wanaoendelea kufadhili, baadhi yao kutotoa fedha walizoahidi kwa wakati na wakati mwingine kutoa fedha pungufu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Wajumbe walishindwa kuchambua bajeti hiyo kwa kuwa fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinategemea Wafadhili. Wajumbe walibaki wakijihoji

inawezekanaje utegemee fedha za kupewa na kisha uwe na uwezo wa kuhoji matumizi yake?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati inaamini suluhisho la kupunguza utegemezi wa Wahisani ni kuanzishwa Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania, na kwa kuwa mchakato wa kuanzishwa Mfuko huo umechukua muda mrefu na kila wakati Kamati inapohitaji maelezo kuhusu Mfuko huo, huambiwa kuwa andiko limefikia pazuri na limeshawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri tayari kwa utekelezaji. Kamati inaisihi sana Serikali kuona umuhimu wa kukamilisha mchakato huo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ukipitia taarifa ya maombi ya fedha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, unaweza ukashangazwa na kiasi cha Shilingi 2,559,170,000 tu ndicho kinachoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara ya Watumishi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Hata hivyo, ukipitia *Medium Term Expenditure Fund (MTEF)* zote utagundua kuwa, karibu kila Wizara, Halmashauri na Taasisi za Serikali, zimekasimu fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI.

Kwa mwaka huu wa fedha, jumla ya fedha zote zilizokasimiwa kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI ni shilingi 10,714,059,979.33. Fedha hizi ni nyingi na inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali kupambana na UKIMWI ili kuweza kufikia zero tatu; yaani Tanzania bila maambukizi mapya, unyanyapaa na kutokuwa na vifo vitokanavyo na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonesha kwamba, baadhi ya Wizara, Halmashauri na Taasisi za Serikali, huziita fedha za mapambano dhidi ya UKIMWI kuwa fedha zisizo na mwenyewe. (*Makofii*)

Kwa kiasi kikubwa fedha hizi hutumika kwenye makongamano, semina na posho za vikao. Kamati inachukua fursa hii kuwatangazia Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Watendaji wa Taasisi na Wakala wa Serikali na

Wakurugenzi wa Halmashauri wote waliokasimia fedha za UKIMWI na kutengewa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, fedha za UKIMWI sasa zimempata msimamizi ambaye ni Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Kamati inawatangazia kwamba, haitafumbia macho ubadhirifu wowote utakaofanywa kwa kutumia fedha za UKIMWI. Aidha, Kamati inawashauri wahusika wote kuandaa mpango wa utekelezaji wa fedha hizo, ambapo kila Wizara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi za Serikali zitatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa fedha hizo mbele ya Kamati ya Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaanmini hatua hii itasaidia kuwepo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za UKIMWI na hivyo kusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuongeza huduma za kudhibiti UKIMWI hususan tiba, kinga na kuweka mazingira wezeshi na kupunguza madhara yatokanayo na UKIMWI. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi wa namna fedha za UKIMWI zinavyotumika vibaya katika Halmashauri zetu. Ufujaji huu wa fedha za UKIMWI umekuwa ukisababishwa na uvunjwaji wa mwongozo wa uendeshaji wa Vikao vya Kamati katika baadhi ya Halmashauri. Katika vikao hivyo, baadhi ya Halmashauri huteua Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI ya Halmashauri, ambao hawana dhamira ya dhati ya kupambana na UKIMWI. Kamati inazitaka Halmashauri zote nchini kufuata mwongozo uliopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Makundi Maalum ndiyo changamoto kubwa Kitaifa na Kimataifa katika kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI. Makundi haya Maalum ni ya watu ambao mara nyingi wanafikiriwa kuwa katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa Virusi vya UKIMWI (VVU). Watu hawa wanajihusisha na mienendo haramu na inayoainishia jamii ni kama ifuatavyo: makahaba; wateja wa makahaba; wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga

sindano na bila kujidunga; wanaume wanaolawitiana na kulawiti; na wanaofanya ngono zembe (bila kujikinga).

Mheshimiwa Spika, inasemekana kuwa maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI kwa sasa na kwa siku zijazo yatatokana na makundi hayo hatarishi yaliyotajwa hapo juu. Ili kuweza kuzuia maambukizi mapya, Kamati inashauri Serikali iimarishe mwitikio wa Taifa kwa makundi haya hatarishi kwa kuruhusu mijadala ya wazi ya Kitaifa ya namna ya kukabiliana na makundi hatarishi. Kamati inasisitiza kuwa, tabia hizi za kutumia dawa za kulevyia na kujidunga sindano, wanaume wanaolawitiana na wanaume wanaofanya ngono kinyume na maumbile, ziko kwenye jamii zetu na zinakua kwa kasi. Ikiwa Taifa litaona haya kuzungumza mambo haya hadharani na kwa uwazi, uwezekano wa usemi wa kuwa Tanzania bila UKIMWI inawezekana, ukawa ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Uzinduzi wa Matokeo ya Taarifa ya Viashiria vya UKIMWI. Uzinduzi huo ulifanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Katika uzinduzi huo, taarifa iliyotolewa ilionesha kuwa, kuna baadhi ya mikoa imefanikiwa kupunguza maambukizi mapya na kuna baadhi ya mikoa maambukizi mapya yameongezeka kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo, Kamati imejifunza kuwa rasilimali za UKIMWI ni vyema zikatengwa kulingana na ukubwa wa tatizo. Aidha, Kamati inashauri kuwa mikoa iliyofanikiwa kupunguza maambukizi mapya isibweteke bali iendelee kupambana na janga hili. Vilevile, Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini kujadili taarifa ya maambukizi ya virusi katika mikoa na Halmashauri zao na kutumia takwimu hizi mpya katika kupanga mpango wa kupambana na maambukizi haya.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine ya muhimu ambayo Kamati inashauri Tume ya Kudhibiti UKIMWI kuyapa kipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2013/ 2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Vikao vya Kamati vilivyomalizika, Kamati iliweza kutembelea mradi wa kituo cha kupumzika madereva wa masafa marefu kilichoko eneo la Mdaula Chalinze. Kituo hiki na vingine vya aina hiyo, vinajengwa kufuatia makubaliano yaliyofikiwa kwenye programu za kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI katika Nchi za Jumuia ya Kusini mwa Afrika (*SADC*). Pamoja na mambo mengine, Programu hii ina lengo la kuwawezesha madereva wa masafa marefu kuwa na mahali salama pa kupumzika wanapokuwa safarini. Hatua hii inalenga kusaidia madereva kupata burudani mbalimbali pamoja na huduma ya maelezo kuhusu Virusi vya UKIMWI. Vituo hivi vinalenga kuwapunguzia madereva muda wa kwenda kwenye vishawishi vingine wanapokuwa safarini. Ikumbukwe kuwa madereva hawa wanaweza kuwa nje ya familia zao kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea kituo hicho haikuridhishwa na huduma zinazotolewa kituoni hapo, kwani kituo kimejengwa karibu na makaburi na kiko mbali na Chalinze ambapo ndipo walengwa halisi walipo. Kufuatia hali hiyo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

- (i) Kituo kingine kifunguliwe Chalinze ili kiweze kuwahudumia walengwa (madereva wa masafa marefu);
- (ii) Halmashauri husika ishirikiane na Tume ya Kudhibiti UKIMWI na kutoa huduma za masuala ya UKIMWI na mafunzo ya aina mbalimbali ili kuweza kuvutia watu wengi zaidi kufika kituoni na kupata huduma za UKIMWI na huduma nyinezo;
- (iii) Serikali itoe mwongozo utakaonesha vituo vyote vinatakiwa kujengwa kwa ukubwa gani (kuwe na ramani maalum);
- (iv) Vituo viboreshwe kwa kuweka burudani tofauti tofauti ili viweze kuvutia madereva wa masafa marefu kuona umuhimu wa kupumzika kituoni;

- (v) Wakufunzi wa kituo wapewe elimu; na
- (vi) Vituo vyaa aina hii vitangazwe ili viweze kufahamika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliweza kufanya ziara katika Manispaa ya Kinondoni, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipokea taarifa kuhusu Mfumo wa Ufuatiliaji Masula ya UKIMWI (*Tanzania Output Monitoring System (Non Medical) for HIV and AIDS (TOMSHA)*).

Mheshimiwa Spika, *TOMSHA* ni mfumo wa Kitaifa wa kiteknolojia unaotumika kufuatilia na kurekodi shughuli zisizo za kitabibu. Katika Manispaa ya Kinondoni, mfumo huu unafanya kazi kwa kushirikiana na asasi za kudhibiti UKIMWI. Asasi 43 zillizoko Manispaa ya Kinondoni zimeingia katika mfumo huu na hutoa taarifa za namna zinavyoratibu mapambano dhidi ya UKIMWI. Taarifa hizo hukusanywa kutoka katika Halmashauri zote na kuwasilishwa kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI ambao huandaa taarifa za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, majumuisho ya taarifa hizi ndiyo huwawezesha Tume ya Kudhibiti UKIMWI kuweza kupanga bajeti na programu mbalimbali za kupambana na UKIMWI. Kamati inapongeza uanzishwaji wa mfumo huu, ingawa utekelezaji wake katika Manispaa kubwa kama ya Kinondoni ni tatizo. Hii ina maana kuwa upo uwezekano wa kuwepo kwa tatizo la utumiaji mfumo huu wa kiteknolojia katika Manispaa nyingi. Hivyo, Kamati inashauri kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, fedha za kutosha zitengwe ili kuwawezesha wataalamu wa mifumo ya kompyuta wa Manispaa kupata elimu kuhusu mfumo huu. Aidha, Kamati inawakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri zote kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa mifumo ya kompyuta. Hatua hizi zitasaidia kuwa na takwimu sahihi kuhusu UKIMWI na hivyo kuirahisishia Tume ya Kudhibiti UKIMWI kupanga mipango ya rasilimali fedha itakayoendana na ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Wiliam V. Lukuvi, (Mb) - Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge); Ndugu Paniel L. Lyimo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Joseph Shekiondo - Kamishna Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevyaa na Dkt. Fatuma H. Mrisho - Mwenyekiti Mtendaji Tume ya Kudhibiti UKIMWI, pamoja na Wataalamu wote wa Tume hizi, kwa ushauri na utaalamu wao ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii, kutambua mchango mkubwa unaofanywa na wadau wa maendeleo katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifaa (*UNDAP*), Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), Shirika la Maendeleo la Canada (*CIDA*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*), Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), *Rapid Fund Envelop*, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI (*GLOBAL FUND*), Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya UKIMWI (*PEPFAR*) na Mfuko wa Dunia (*GFATM*). Aidha, naomba niwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati kwa busara zao na kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa, ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti inayoombwa na hivyo kufanikisha Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Chiku Aflah Abwao, Mheshimiwa Omary A. Badwel, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Rashidi Ali Omar, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Ignus A. Malocha, Mheshimiwa Said Ally Bungara,

Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Neema M. Hamid, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Dkt. Engelbert F. Ndugulile, Mheshimiwa Maulida Anna V. Komu, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale na Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallack.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Didimu Kashililah, Makatibu wa Kamati; Ndugu Rachel Nyambuli Nyega na Ndugu Abdallah Hancha, wakisaidiana na Ndugu Halima Laizer, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa liipokee taarifa hii na kukubali kuidhinisha Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Bara, pamoja na Tume ya Kudhibiti wa Dawa za Kulevyta kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, naye tumempangia muda wa saa moja. (*Makof*)

Tangazo linguine, Waheshimiwa kama tulivyojiwekea utaratibu toka zamani, anayependa kuongea na Waziri Mkuu siyo humu ndani, kwa sababu ukianza kuongea na Waziri Mkuu humu ndani tunapishana hapa. Tafadhalii, Mawaziri mkienda mna sababu ya dakika mbili siyo tena kuhamia hapo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU NA TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia marekebisho kadhaa ya kanuni hususan zinazolenga kwa sasa Utaratibu wa Kutunga Sheria kuhusiana na mambo ya fedha, nasi kama Kambi Rasmi ya Upinzani tutafanya marekebisho katika utaratibu tutakaotumia katika kutoa maoni yetu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, kufuatia utaratibu wa mfumo wa bajeti ulivyokuwa huko nyuma, tulitumia muda mwingu kuishauri serikali namna bora ya kuboresha bajeti na utendaji wake wa kazi. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana, Serikali hii imekuwa siyo sikivu vyakutosha hata pale ambapo ushauri unaotolewa uko wazi kwa maslahi na mustakabali mwemwa wa Taifa letu. Aidha, pale ambapo Serikali imechukua maoni yetu, mara nyingi imekuwa haina ustaarabu wa kutambua, kukiri na kushukuru mchango wa Kambi ya Upinzani, bali mbele ya macho ya umma imeendelea kutoa kebehi, kujaribu kuuaminisha umma kuwa Vyama vyakutoa havina ufumbuzi mbadala kwa matatizo yanayolikabili Taifa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la Serikali inayoongozwa na CCM ni kukosa weledi wa kutekeleza kikamilifu vipaumbele vyake pamoja na kuvianisha kuitia Mpango wake wa Miaka Mitano, Bajeti na Programu mbalimbali. Hali hii inaweza kutafsiriwa kama uwezo duni wa kusoma alama za nyakati ikiwemo kubuni na kusimamia inachokiamini. Ni dhahiri vilevile unapolazimika kufanya jambo usiloliamini au lisilo kipaumbele chako, bali cha kulazimishwa na mazingira, unatekeleza bila kujua undani wake na hatima yake ni kuharibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni mtambuka, mwaka huu tutajielekeza kuzungumzia mambo makuu machache ambayo sisi tunaamini ni vipaumbele muhimu ambavyo Waziri Mkuu na Wasaidizi wake wanapaswa kuja na majibu ya kueleweka kwa Watanzania. Aidha, mengine yatawasilishwa kuitia hotuba zetu mbalimbali katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Novemba, 2011 Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Kufuatana malalamiko mengi kuhusu utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria hiyo na kufuatia vikao kati ya Mheshimiwa Rais na Kamati Maalum ya CHADEMA pamoja na wadau wengine, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge hili uliofanyika mwezi Februari mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho hayo yalikuwa ni awamu ya kwanza ya awamu tatu za marekebisho ya Sheria hiyo kwa mujibu wa makubaliano yetu na Mheshimiwa Rais. Awamu nyininge mbili za marekebisho zilitarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka jana, yaani 2012. Hata hivyo, hadi nasoma maoni haya leo hii, Sheria ya Marekebisho ya Katiba haijafanyiwa marekebisho mengine yoyote.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kuitishwa mwaka jana, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa Wajumbe na Watendaji Wakuu wa Tume na Tume yenye ilianza kazi mwezi Mei, 2012. Kwa maana hiyo, hadi kufikia leo, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imeshafanya kazi kwa karibu mwaka mmoja.

Kwa masikitiko makubwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, katika kipindi hiki mtiririko wa matukio kadhaa ndani na nje ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba imethibitisha kwamba haina weledi, dhamira au nia ya kusimamia mchakato huru usiofungamana na upande wowote.

Katika mwaka wa kwanza wa mchakato wa upatikanaji Katiba mpya, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imethibitisha hofu tuliyokuwa nayo toka mwanzo kwamba lengo la mchakato wa Katiba Mpya uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kuhakikisha kwamba, mabadiliko pekee yatakayokuwepo ni yale yenye kulinda matakwa ya CCM na Serikali yake au yale pekee yatakayokuwepo na baraka za *Status Quo*.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Tume haikuweka utaratibu wowote madhubuti wa kutoa elimu kwa Wananchi juu ya masuala yote yanayohusu Katiba Mpya ili kuwaandaa Wananchi kuchangia maoni yao kwa Tume wakiwa na uelewa wa kutosha. Badala yake, wakati wa mikutano ya Tume ya kupokea maoni ya Wananchi, Wajumbe wa Tume walipewa jukumu la kuwaeleza Wananchi juu ya Katiba Mpya kwa muda usiozidi nusu saa!

Kwa kulinganisha, Tume ya Katiba ya Kenya ilifanya kazi ya kutoa elimu kwa umma kwa nchi nzima kwa muda wa miezi sita kabla ya kuanza kukusanya maoni ya Wananchi wa Kenya juu ya Katiba Mpya. Matokeo yake ni kwamba, mchakato wa Katiba Mpya wa Kenya umeiletea nchi hiyo Katiba Mpya ya Mwaka 2010, ambayo imeanza kudhihirisha ubora wake kwa jinsi ambavyo mambo yatokanayo na Uchaguzi Mkuu wa nchi hiyo wa hivi karibuni yaliviyotatuliwa.

Mheshimiwa Spika, pilii, muda uliowekwa na Tume wa kukusanya maoni ya Wananchi ulikuwa mdogo sana ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu na wingi wa Watanzania. Katika Majimbo karibu yote ya Uchaguzi Tanzania Bara, Tume iliendesha wastani wa mikutano saba kwa kila Jimbo kwa lengo la kukusanya maoni ya Wananchi. (*Makof*)

Katika mikutano hiyo, Wananchi walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu Katiba Mpya kwa muda wa dakika tano kila mmoja na mikutano yenye ilichukua muda wa saa tatu ikiwa ni pamoja na muda wa kutambulishana Wajumbe wa Tume na mambo mengine yaliyo nje ya kuchukua maoni ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kwamba, kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti wa Tume, Jaji Joseph Sinde Warioba kwa waandishi habari tarehe 5 Januari, 2013, hadi awamu nne za kukusanya maoni ya Wananchi zinakamilika tarehe 19 Desemba, 2012, Tume ilikwisha kufanya mikutano 1,776 kwa nchi nzima. Aidha, kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti Warioba, hadi kufikia kipindi hicho Wananchi

wapatao 64,737 walikwishatoa maoni yao kwa kuzungumza wakati Wananchi 253,486 walitoa maoni kwa njia ya maandishi, na wengine 16,261 walitumia njia ya posta, tovuti ya Tume, mitandao ya kijamii na ujumbe mfupi wa simu za mkononi.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa taarifa hizi za Mwenyekiti wa Tume, kati ya Watanzania takriban milioni 45, ni Watanzania 334,484 ndiyo waliota maoni juu ya Katiba Mpya hadi kufikia tarehe 4 Januari, 2013. Idadi hii ni sawa na asilimia 0.7 ya Watanzania wote! Na hao ndiyo waliota maoni yao kwa muda wa dakika tano kila mmoja, wakiwamo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ni wazi, kwa takwimu hizi za Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kwa vyovypole vile, Katiba Mpya itakayotokana na maoni haya, haiwezi kuwa Katiba Mpya ya Watanzania wote. Utaratibu wa hovsky namna hii utazaa Katiba Mpya ya hovsky! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, utaratibu huu wa hovsky hauwezi kutupatia Katiba Mpya yenye maridhiano ya Kitaifa kwa ajili ya kutatua migogoro mingi ya kisiasa, kijamii na kidini, ambayo inaikabili nchi yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tatu, licha ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kutangaza kuwa Tume itakuwa huru katika utekelezaji wa majukumu yake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kila dalili za Tume kutokuwa huru au kuutafsiri uhuru vibaya. Kwa mfano, kuna ushahidi kwamba, Tume imekuwa na mawasiliano ya karibu na Serikali na Ofisi ya Rais kwa namna ambayo inaashiria Tume kutokuwa huru. Ndiyo maana katika hotuba yake ya kumaliza mwaka uliopita na kufungua Mwaka Mpya, Rais Jakaya Kikwete, alilitangazia Taifa ratiba ya kazi za Tume ambayo Tume yenywewe ilikuwa hajjawahi kuitoa hadharani.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Kikwete alitangaza siyo tu kumalizika kwa awamu ya kukusanya maoni ya Wananchi, bali pia alitangaza ratiba ya Tume kuanza kuchukua maoni

ya vyama nya siasa, taasisi nyingine na makundi maalum, tarehe ya kutolewa kwa Rasimu ya Kwanza ya Katiba Mpya, Mikutano ya Mabaraza ya Katiba na Bunge Maalum la Katiba na hata tarehe ya kura ya maoni na upitishwaji wa kura ya maoni kuihalalisha Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais asingeweza kufahamu ratiba hii yote bila kupatiwa taarifa ama na Tume yenye we ama na watendaji au watumishi wake au na Wajumbe wa Tume. Mbali na taarifa ya kwisha kwa awamu ya tatu ya zoezi la kukusanya maoni ya Wananchi, taarifa hizi hazikuwa zimetolewa hadharani na Tume kabla ya hotuba ya Mwaka Mpya ya Mheshimiwa Rais Kikwete!

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetambua siku zote kwamba, msemaji rasmi wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa Joseph Warioba. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hajawahi kusikia wala kuona mahali popote ambapo Sheria ya Mabadiliko ya Katiba imempa Mheshimiwa Rais Kikwete jukumu la kuwa msemaji wa Tume. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kama Rais anaweza kupatiwa taarifa za kina namna hiyo kuhusiana na shughuli za Tume, kuna uhakika gani kwamba ye ye au Serikali yake hawatoi kwa Tume maelekezo ya kichinichini juu ya nini cha kufanya, kwa namna gani na kwa wakati gani.

Mheshimiwa Spika, nne, wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba ikitoa taarifa za kina juu ya shughuli zake kwa Mheshimiwa Rais Kikwete na Serikali yake, Tume hiyo hiyo imetangaza wazi wazi kwamba, haiwajibiki kwa Bunge kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Zaidi ya kumtuma Naibu Katibu wa Tume, Viongozi wa Tume kama vile Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume, wamekataa kuhudhuria Vikao nya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ili kuieleza Kamati juu ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya Nchi.

Katika hili, Tume imeungwa mkono na Serikali hiyo hiyo inayoelekea kupata taarifa za kina juu ya utekelezaji wa kazi

zake! Hii ni licha ya kupatiwa jumla ya shilingi bilioni 33.944 za walipa kodi wa Tanzania zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, wakati Tume inaharibu mchakato wa Katiba Mpya kama tulivyoonesha hapa, Bunge, kwa kuititia kwa Kamati yake, limezuiliwa kuhoji shughuli za Tume kwa hoja kwamba Tume iko huru.

Mheshimiwa Spika, hii inaweza kuwa mara ya kwanza kwa chombo cha umma kinachotumia mabilioni ya fedha za umma kilichopewa majukumu ya umma na Sheria iliyotungwa na Bunge hili Tukufu kukataa kuwa chini ya usimamizi wa Kikatiba wa Bunge (*Parliamentary Oversight*). Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imesikitishwa sana na kushindwa kwa Kamati husika ya Bunge kudai madaraka yake ya usimamizi yasipuuze na Tume na/au Serikali. Udhafu huu wa Bunge na Kamati unaweza kuligharimu Taifa endapo mchakato wa Katiba Mpya utachakachuliwa na kuliingiza Taifa katika machafuko ya kisiasa, kidini au kijamii.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu juu ya uwajibikaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa matumizi ya mabilioni ya fedha za umma iliyoidhinishiwa mwaka jana na inayoyaomba mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tano, Tume imetengeneza utaratibu wa Mabaraza ya Kikatiba ambao kwa ushahidi wa mwanzo tu unaonesha kwamba, hayo ni Mabaraza ya CCM na siyo Mabaraza ya Katiba ya Watanzania wote. Hili limefanyika kwa kuititia Mwongozo Kuhusu Muundo, Utaratibu wa Kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Uendeshaji wake, uliotolewa na Tume mwezi Februari, 2013. Kwa mujibu wa Muundo huu, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya watachaguliwa na Kamati za Maendeleo za Kata, yaani *WDC* baada ya kuwa wamechaguliwa moja kwa moja na Wananchi katika vijiji na mitaa. Wajumbe wa *WDC* ni Madiwani wa Kata ambao ni Wenyeviti wake, Watendaji wa Kata ambao ni Makatibu na Wenyeviti wa Viji au Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuatana na chaguzi za vijiji na mitaa za mwaka 2009, zaidi ya asilimia 90 ya vijiji na mitaa inaongozwa na Wenyeviti ambao ni Wana-CCM. Aidha, kutokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, zaidi ya asilimia 80 ya Kata zote nchini zinaongozwa na Madiwani wa CCM.

Hawa ndio waliochagua Wajumbe wa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba tangu mwanzoni mwa wiki iliyopita. Matokeo yake, kwa taarifa ilizonazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu, kila mahali wagombea ambao hawakuwa Wana-CCM walienguliwa katika ngazi ya uchaguzi wa vijiji au mitaa au wameenguliwa na *WDC* baada ya kushinda katika ngazi hizo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina ushahidi kwamba, Viongozi wa Kiserikali kama vile Wakuu wa Wilaya na Mikoa walliwhamasisha Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Madiwani kuhakikisha kwamba, wagombea wote wasiokuwa Wana-CCM, hasa wa CHADEMA, wanaenguliwa katika chaguzi za vijiji, mitaa au kata.

Mfano mzuri ni wa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Ndugu Jackson Msome, aliyeitisha mukutano wa Wenyeviti wote wa Mitaa ya Musoma Mjini na kuwapa maelekezo ya kuhakikisha kwamba, watu wasiokuwa wanachama wa CCM hawapati nafasi katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya au Manispaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, licha ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kupatiwa maoni ya wadau kwamba utaratibu huo utaharibu mchakato wa Katiba Mpya, Tume ilikataa katakata kuubadilisha Muundo wa Mabaraza haya. Ni wazi kwamba, Tume inafahamu inachokifanya.

Ni wazi vile vile kwamba, Tume inafahamu matokeo ya hicho inachokifanya, yaani kuundwa kwa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ambayo ni ya Wana-CCM na wala haihitaji shahada ya uzamivu kufahamu kwamba Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, yenye kutawaliwa kwa kiasi hicho na Wana-

CCM, yatatoa maoni ya aina gani juu ya Rasimu ya Katiba Mpya yatakayojadili.

Itakuwa ni Katiba Mpya kwa jina tu, mambo mengine ya msingi yatabaki vile vile. Kwa maneno mengine, itakuwa ni Katiba ile ile, ya watu wale wale, wa chama kile kile.

Mheshimiwa Spika, uchakachuaji wa mchakato wa Katiba Mpya wa aina hii ndiyo ulioiingiza Zimbabwe katika machafuko makubwa ya kisiasa toka mwaka 1998 na Kenya mwaka 2007/2008.

Kwa utaratibu huu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, inaelekeea Serikali ya CCM kutotaka kujifunza kutohana na yaliyowakuta jirani zetu wa Kenya na marafiki zetu wa Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali imekataa ama imeshindwa kuheshimu makubaliano iliyofikia na wadau mbalimbali ikiwemo CHADEMA, kufanya marekebisho zaidi ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kwa sababu hiyo, bado hajulikani Wajumbe mia moja na sitini na sita watakaotokana na taasisi mbalimbali zilizotajwa na Sheria hiyo watateuliwa kwa utaratibu gani na nani atakayefanya uteuzi huo.

Vile vile, bado hakuna mwafaka juu ya uhalali wa idadi kubwa ya Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kutoka Zanzibar kushiriki katika mijadala wa Katiba Mpya kwenye masuala yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara wakati hakuna Mjumbe hata mmoja wa Tanzania Bara anayeweza kushiriki katika mijadala ya Kikatiba inayohusu masuala ya Zanzibar yasiyokuwa Mambo ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, bado hakuna majibu yanayotosheleza yanayompa Rais mamlaka ya kuliitisha upya Bunge Maalum la Katiba na kulielekeza kuboresha' masharti ya Katiba Mpya mara baada ya Bunge hilo kuipitisha. Aidha, hajulikani ni uhalali upi wa Kisheria na Kikatiba utakaoiruhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kusimamia na kuendesha kura ya maoni ya kuhalalisha Katiba Mpya,

kwa sababu Katiba na Sheria za Uchaguzi za sasa hazitambui wala kuweka utaratibu wa kuendesha kura ya maoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Serikali kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ili kufanya marekebisho katika maeneo tajwa ni ushahidi wa wazi kwamba, Serikali ya CCM haina nia ya dhati na dhamira safi ya kuhakikisha Tanzania inapata Katiba Mpya inayoistahili. Aidha, si nia ya CHADEMA kuendelea kushiriki na kubariki mchakato huu kama ulivyo sasa kwani ishara zote ziko wazi kuwa Katiba inayokusudiwa ni ile tu itakayokidhi matakwa ya Wana-CCM na Washirika wake na hivyo kutokutimiza azma ya kuwa na Katiba itakayoponya majeraha mbalimbali na kurejesha uzalendo, mshikamano wetu wa kitaifa na upendo wa dhati mionganini mwa Watanzania na kisha mfumo wa Utawala utakaokidhi mahitaji ya wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inatangaza rasmi kwamba, CHADEMA itajitoa ushiriki wake katika mchakato wa Katiba Mpya endapo mambo yafuatayo hayatapatiwa ufumbuzi hadi kufikia mwisho wa mwezi huu, yaani tarehe 30 Aprili, 2013:- (*Makof*)

Kwanza, kufutwa kwa uteuzi/uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba uliofanywa na Kamati za Maendeleo za Kata, na badala yake Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya wachaguliwe moja kwa moja na Wananchi wa Kata husika bila kuchujwa na WDC. (*Makof*)

Pili, Serikali ilete mbele ya Bunge hili Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yatayofanyia maeneo yafuatayo marekebisho:-

(a) Vifungu vyote vinavyohusu uwakilishi katika Bunge Maalum la Katiba wa taasisi zilizoainishwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba;

(b) Vifungu vyote vinavyohusu ushirikishi wa Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kutoka Zanzibar katika mijadala inayohusu mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara;

(c) Vifungu vyote vinavyohusu mamlaka ya Rais kuitisha tena Bunge Maalum la Katiba baada ya Bunge hilo kuwa limeshapitisha Rasimu ya Katiba Mpya kwa lengo la kufanya marekebisho katika Rasimu kabla hajapelekwa kwenye kura ya maoni; na

(d) Vifungu vyote vinavyohusu mamlaka ya Kikatiba na ya Kisheria yatakayo iwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendesha na kusimamia kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya hotuba yangu, itazungumzia suala la anguko la Elimu Tanzania, angamizo la kizazi na janga la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia umuhimu wa elimu kwa kumnukuu Rais wa 55 wa Marekani, John F. Kennedy (1917 – 1963);

*"Our progress as a nation can be no swifter than our progress in education. The human mind is our fundamental resource."*

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kumekuwepo mijadala mzito sana kuhusiana na hali ya elimu nchini. Pamekuwepo na malalamiko mengi sana yakiwemo yaliyomtaka Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Naibu wake, Mheshimiwa Phillip Mulugo, wajiu zulu kama ishara ya uwajibikaji wa kisiasa. Ni dhahiri kuwa, elimu yetu kama Taifa, imeporomoka kwa kiasi kikubwa cha sasa kuhatarisha mustakabali wetu kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni mwaka mmoja tu umepita tangu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inayoongozwa na CHADEMA itoe angalizo kali kwa Serikali juu ya kasi kubwa ya kuporomoka kwa Elimu ya Tanzania na hivyo kuitaka

Serikali kuchukua hatua madhubuti ili kuliepusha Taifa na balaa hilo. Hata hivyo, Serikali hii ya CCM imeendelea kupuuza ushauri mzuri inayopewa bure na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na matokeo yake ni kwamba, anguko la mwaka huu ni kubwa kuliko maanguko yote yaliyowahi kutokea katika Historia ya Tanzania ambapo asilimia 60.6 (240,903) ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne wamepata daraja sifuri na wengine asilimia 26.02 (103,327) daraja la nne. Jumla ya kufeli huku ni zaidi ya asilimia 86.62.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kufeli huku kwa kutisha kwa wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2012, wadau wengi walitaka baadhi ya Viongozi wa Sekta ya Elimu akiwemo Waziri, kuwajibika. Ni bahati mbaya sana kuwa Waziri Mkuu ni mmojawapo wa Viongozi Wakuu aliystahili kuchukua hatua za kuwawajibisha watusika lakini hakufanya hivyo. Badala yake, akakimbilia kuunda Tume ya Uchunguzi, ilhalilieye mwenyewe Waziri Mkuu, Waziri wake wa Elimu na Serikali yake yote, ikijua fika nini kinasababisha kuperomoka kwa elimu yetu. Yumkini, kama kweli Serikali hadi leo hajui sababu ya kuperomoka kwa elimu yetu, basi haina tena sifa wala weledi wa kusimamia siyo tu elimu, bali maisha ya kila siku ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kufeli huku hakuwezi kuchukuliwa kama bahati mbaya hasa ikiwekwa maanani kuwa, mserereko wa watoto wetu kufeli umeshika kasi chini ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne hasa kuanzia mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, ufaulu wa vijana wetu wa kidato cha nne ilikuwa (90.3%), 2008 (83.6%), 2009 (72.5%) na 2010 (50.4%). Kufuatia mserereko huu wa kufeli, Serikali iliunda timu iliyoshirikisha wataalam kadhaa, kubaini chanzo chake na tiba ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Timu hii iliyokuwa chini ya Uenyekiti wa Bw. Francis M. Liboy wa TAMISEMI, ilikamilisha Ripoti yake mwaka 2011 na kutoa mapendekezo kadhaa kwa Serikali. Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, anajua Ripoti hii kwani ndiye aliyeadhika dibaji yake.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chetu tumeambatanisha kama kiambatisho A ripoti hiyo ya elimu ya mwaka 2010, iliyokuwa inafanya utafiti kuhusiana na kufeli kwa wanafunzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba uendelee kunilinda ili Mheshimiwa Waziri Mkuu, aendelee kunisikiliza kama ulivytangaza mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, mbali na ushauri wetu wa mara kwa mara, Serikali hii imebeza kwa nguvu zote juhudimbalimbali zinazofanywa na wadau wengine wenye kuumizwa na kusikitishwa na kuporomoka huku kwa elimu. Watanzania ni mashahidi namna katika Mkutano wa Kumi wa Bunge, hoja binafsi ya Mheshimiwa James Mbatia (Mb), kuhusu udhaifu ulioko katika Sekta ya Elimu ilivyochukuliwa kimzaha na kutolewa majibu mepesi na Serikali kinyume na Kanuni za Bunge na hatimaye kuyazima Maazimio ya Bunge ya kuinusuru elimu ya Tanzania yaliyokuwa yamependekezwa katika hoja hiyo.

Ni katika mkutano huohuo wa Bunge ambapo hoja binafsi ya Mheshimiwa Joshua Nassari (Mb), kuhusu Baraza la Mitihani linavyoathiri elimu ya Tanzania iliondolewa katika orodha ya shughuli za Mkutano wa Kumi wa Bunge bila ridhaa ya mtoa hoja kinyume na Kanuni ya 58(5).

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali ya CCM chini ya mwavuli wa wingi wa Wabunge wake Bungeni, cha kuzivuruga hoja hizi na hivyo kusababisha Maazimio ya Bunge juu ya hoja hizi kutoteklezwa, ni udhaifu mkubwa sana kwa chama kinachotawala cha CCM na Serikali yake na ni ushahidi uliokamilika kwamba, Elimu kwao siyo kipaumbele cha Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali, naomba nirudie kwa nguvu, Serikali, ambayo Elimu siyo kipaumbele chake, haiwafai Watanzania kwa karne hii. Kuendelea kuukumbatia utawala na aina hii ni kukaribisha maafa yasiyoepukika kwa Taifa. Mbali na kulisababishia Taifa hili aibu kubwa mbele ya

majirani zetu na jamii ya kimataifa kwa vijana walio wengi wa Kitanzania kuonekana kuwa na elimu ya mashaka na isiyoweza kuhimili ushindani wa soko la ajira, ubovu wetu wa elimu umedumaza uwezo wetu wa ndani wa kusimamia rasilimali za Taifa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inawapa angalizo Wananchi wote wa Tanzania kwamba, haya yote yanatokea kwa kuwa Serikali ya CCM haijaiweka elimu kuwa kipaumbele cha Taifa na kwamba umefika wakati wa kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa utawala kwa kuchagua chama chenye nia ya dhati ya kuleta mabadilko kitakachounda Serikali inayojali elimu ya watoto wao na bila shaka chama hicho hakiwezi kuwa CCM ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mbali na kuweka Taifa mbali na CCM, Taifa kuititia hotuba hii linataka kujua Serikali ina nini cha kusema kuhusiana na utafiti huu uliofanyika mwaka 2011, imetekeleza mangapi kati ya mapendekezo 27 yaliyotolewa. Aidha, ni kwa nini Waziri Mkuu aliunda Tume nyingine kwa kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hii ingali Ripoti nyingine inayohusu somo hilo hilo ilikuwa iko tayari mkononi mwake.

Mheshimiwa Spika, unyanyapaa wa fikra Vyuo Vikuu: Pamoja na nia njema ya Katiba ya nchi yetu kuheshimu haki ya uhuru wa mawazo kama ilivyowekwa bayana katika Ibara ya 18(a) na Ibara ya 20(1) kwa kutoa uhuru wa mtu kushirikiana na wengine, kumekuwepo na propaganda mbalimbali hasa kwenye taasisi za elimu ya juu, zenye kuminya nafasi na uhuru wa Vyama vya Upinzani kuendesha shughuli zake kwa usawa, uwazi na kwa haki katika ngazi ya elimu ya juu kama ambavyo Chama Tawala kimejiwekea na kujitengenezea mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema hivi: "*Lakini kutoa uongozi maana yake siyo kuwanyang'anya watu wenyewe mamlaka yao. Watu lazima wafanye uamuzi wao wenyewe kuhusu maisha yao ya baadae kwa kufuata njia za demokrasia. Uongozi hauwezi kuchukua nafasi ya demokrasi; uongozi lazima uwe sehemu ya demokrasi.*"

Mheshimiwa Spika, tafakuri ya nukuu hii imekuja wakati ambao ushiriki wa wanafunzi wa elimu ya juu katika siasa unaonekana kuelemea upande mmoja tu wa kukipendelea na kukipa uwezo Chama Tawala katika shughuli zake kwenye taasisi hizo. CCM wamefikiri na kuamua kuanzisha mkoa maalumu kwa sasa wakitambua kuwa vyuo (hasa Vyuo Vikuu) haviruhusiwi kuendesha shughuli za siasa vyuoni, kama ilivyo majeshi, makanisa au misikiti na ili kuthibitisha hilo, wameelekeza pia shughuli za mkoa maalumu ulioanzishwa zifanyike nje ya chuo. Tujiulize na kutafakari zaidi kuhusu mshindo (*impact*) wa shughuli za mkoa maalumu wa kisiasa ndani ya himaya za vyuo vikuu na elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ngumu kuamini kuwa shughuli za siasa vyuoni, ambazo *Tanzania Commission of University Act* imeweka bayana kuwa ni kosa, zitaweza kudhibitiwa ikiwa vyama vingine vinajiwekea uhalali na mazingira ya kuingiza wanavyuo kwenye siasa, jambo ambalo udhibiti wake ni mgumu kwa mamlaka husika hasa vyuoni kwa kuwa wanavyuo hufanya vikao vya siasa kwa siri, na kwa nyakati ambazo uongozi wa vyuo hauna taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa uangalifu mkubwa, ningependa kutoa angalizo kuwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitokubali unyanyapaa wa fikra wa aina yoyote utakaoendana na kujenga matabaka kutokana na utofauti wa mitazamo baina ya jamii ya wasomi kwa kuwa, kutoka taasisi mbalimbali za elimu ya juu, chimbuko la viongozi mahiri wa nchi hii pamoja na nchi nyingine mbalimbali duniani limechipukia. Kambi Rasmi ya Upinzani, itaendelea na juhudhi zake za kuhakikisha kuwa Taifa kwa kuititia Wanafunzi wa Elimu ya Juu, wanapata fursa mbalimbali za kuikomboa Jamii ya Kitanzania ambayo inadumazwa kwa unyanyapaa wa fikra.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kufuta unyanyapaa wa fikra kwa vijana waliopo kwenye elimu ya juu ni kwa Serikali kurejesha rasmi na kuruhusu uwepo wa siasa katika elimu ya juu na Vyuo Vikuu vyote nchini kama shughuli ambazo ni nje ya masomo ili kusaidia kujenga uwanja wa

demokrasia katika serikali za vyuvo. Vilevile itasaidia katika kuweka mazingira ambapo wasomi wetu wanaanza kujifunza mbini na utendaji wa kisiasa katika mazingira ya elimu ili waweze kujifunza kuishi pamoja, kipingana kwa hoja na kujua jinsi ya kuvumiliana katika mazingira ya tofauti mbalimbali za kiitikadi, imani na mtazamo, kama ilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi ya CHADEMA ya Mwaka 2010. Hapa nikisisitiza maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, juu ya kuboresha maisha ya Watanzania:

*"Tukiwasaidia watu wa Tanzania kuendelea ndiyo tunaiendezea Tanzania. Maana Tanzania ni ya Watanzania Na Watanzania ni wote, hakuna mtu mwenye haki ya kusema "Mimi ndiyo watu". Wala hakuna Mtanzania mwenye haki ya kusema "Najua linalowafaa Watanzania na wengine lazima wafuate."*

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu wa Juu ni katika kusaidia kupunguza maumivu ya wazazi na walezi wa Kitanzania katika kuhakikisha vijana wetu wanapata elimu ya juu kwa kusaidiana na taasisi hii ya Serikali (*HELSB*), kwa kugawa mikopo kwa waombaji wenyewe vigezo sahihi na kuwapa mikopo kwa viwango vya madaraja mbalimbali ya uhitaji.

Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo vimekua vikitumika katika utoaji wa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, vimekua vikilalamikiwa. Baadhi ya wanufaika wa mikopo hii, wamejikuta wakipewa asilimia chache huku wakiwa wametoka katika familia za kifukara ambazo hazina uwezo wa kuendesha maisha yao. Familia nyingi hazina uwezo hata wa kuhimili mlo mmoja kwa siku; je, mzigo wa kuwasomesha watoto na vijana wao ngazi ya elimu ya juu nani ataubeba? Kutokana na udhaifu huu, vijana wameanza kujigawa katika matabaka ya 'wao' (matajiri na wenyewe nazo) na 'sisi' (masikini, wasionacho) na wamefikia mahali wanankuu maandiko ya dini kuwa "mwenye nacho huongezewa, asiye nacho hypokonywa hata kile kidogo alicho nacho."

Mheshimiwa Spika, malalamiko juu ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu yameendelea kuwa mengi, huku waombaji wakilalamikia mlolongo wa taratibu zilizowekwa ili mwombaji aweze kufanikisha usajili wake katika Bodi. Malalamiko haya yameendana sambamba na utaratibu mbovu wa utunzaji wa kumbukumbu za watu katika mfumo mzima wa elimu Tanzania, ambao unajenga urasimu mgumu katika kupata taarifa za mwombaji na hivyo waombaji kulazimika kujaza taarifa upya kila mwaka mpya wa masomo unapoanza.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ilingia gharama ya kununua mfumo utakaotumika katika kuchambua viwango vya ukopeshaji kwa wanafunzi, kutoka kwa kampuni ya nchini Afrika Kusini ya *ADBSC* kwa gharama za Dola za Kimarekani 188,000 na marekebisho ya mtambo huu yaliigharimu Bodi kiasi cha Dola za Kimarekani 42,000. Mfumo huu ultarajiwu kupunguza malalamiko ya waombaji na badala yake malalamiko yanaongezeka kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la malalamiko mbalimbali juu ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi waliopo vyuoni hali ambayo imekua ikisababisha migomo ya mara kwa mara katika taasisi hizo, nalo limekua tatizo lisiloisha. Tumeshuhudia migomo hiyo ikiambatana na kusimamishwa ama kufukuzwa kwa wanavyuo, hali ambayo inajenga kizazi chenye hofu hasa inapokuja katika kutetea haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 19(1) cha Sheria Na. 9 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ni wajibu wa kila mtu aliyenufaika na mikopo ya elimu ya juu, kurejesha mkopo Serikalini kupitia Bodi ya Mikopo. Pamoja na changamoto ya urejeshwaji wa mikopo kwa walionufaika, Bodi haijafanya kazi ya kutosha katika kufuatilia na kujua kuhusu wanufaika wa mikopo hiyo (*tracking system*).

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, Bodi ya Mikopo haijaweka utaratibu na mfumo sahihi wa kuwafuatilia wadeni wake, na hivyo, kuna asilimia kubwa ya wanufaika wa mikopo

hiyo ambao wako makazini na wana ajira, lakini mpaka leo hawajawahi kukatwa marejesho ya mikopo wala kufuatiiliwa na Bodi kwa ajili ya taratibu za kuwaingiza katika mfumo wa marejesho.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa kumekuwa na ubabaishaji mkubwa si katika marejesho tu, hata katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu. Pamoja na ushauri ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliutoa kwa Serikali katika uwasilishaji wa hotuba ya mwaka 2012/2013, kuanzisha na kutumia mfumo wa urejeshaji mikopo kwa kutumia teknolojia ya kibenki kupitia mitandao ya simu kama *M-PESA*, *TIGO PESA*, *Airtel Money*, *Z-Pesa* na kadhalika, Serikali na Bodi ya Mikopo inaonekana kutofufata ushauri huu na hivyo kuendelea kuwanyima fursa wahitaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara husika pamoja na Bodi ya Mikopo kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa mapendekezo haya, kama wamefanya tathmini juu ya uanzishwaji wa mfumo huu, faida na hasara zake na kama hawajafanya tathmini, Wizara husika itoe kauli katika Mkutano huu wa Bunge, juu ya njia mbadala na mfumo utakaohakikisha wanufaika wanapata urahisi katika urejeshaji wa makato ya mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaendelea kusisitiza juu ya utekelezaji wa mapendekezo yake yaliyopo katika llani ya CHADEMA ya kuivunja Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutokana na uendeshaji mbovu, mfumo wake mbovu wa kisheria na uongozi ambao umeshindwa kufanya elimu ya juu ipatikane kwa kila kijana na ambayo kutokana na uongozi usiofaa, imeshindwa kukusanya madeni toka kwa wakopaji.

Mheshimiwa Spika, hatima ya watoto wanaoshindwa kuendelea na masomo ya Sekondari baada ya kumaliza elimu ya Msingi: Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali, watoto na vijana wa Kitanzania walio chini ya umri wa miaka 18 ambao wamefeli darasa la saba na au kidato cha nne, kwa sasa ni wastani wa watoto 800,000. Wengi wa watoto hawa ambao

wengi hutoka familia masikini, hawana uwezo wa kuijendeleza na hawana sifa za kuajiriwa ikiwa ni pamoja na umri mdogo. Kundi hili ni kubwa na linakua kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka 51 ya Uhuru, Serikali hajitatengeneza Sera yoyote au Sheria ya kusaidia kundi hili kubwa ili liweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi ili waweze kujikimu wao wenyewe na kuchangia katika Pato la Taifa. Kundi hili lilito hazina kubwa ya nguvukazi ya Taifa letu siku za usoni, limeachwa solemba huku likipewa majina ya kebehi ya kila aina ikiwemo wazururaji, vibaka, machinga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kwamba ina mpango gani wa kupunguza idadi hii ya watoto wanaobaki mitaani bila shughuli rasmi ya kufanya?

Pili, kwa wale ambao imeshindikana kabisa kuendelea na masomo, kuna mpango gani wa kisera wa kuweza kuwasaidia ili waweze kushiriki katika shughuli rasmi za kiuchumi ili kulinusuru Taifa kuondokana na umaskini uliokithiri?

Mheshimiwa Spika, chaguzi huru na za haki ni kipimo muhimu cha demokrasia ya kweli. Kwa kutambua umuhimu huu katika chaguzi na hatimaye katika kuongoza nchi, Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatoa haki ya kupiga kura kwa kila Raia wa Tanzania, aliyetimiza umri wa miaka kumi na minane.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka utaratibu mzuri wa kila raia wa Tanzania mwenye sifa ya kupiga kura aweze kupiga kura, Ibara ya 5(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetoa fursa kwa Bunge kutunga Sheria ya Uchaguzi ambayo pamoja na mambo mengine, itaanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika Daftari hili.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lipo, lakini ni bahati mbaya sana pia kwamba utaratibu wa kurekebisha au kuboresha yaliyomo katika Daftari hilo hauendi sawia na haki ya raia kupiga kura na mahitaji makubwa ya kukuza demokrasia katika chaguzi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa nimewuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, mbele ya Bunge hili juu ya mkakati wa Serikali kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Wakati wote majibu yamekuwa ni mepesi na yasiyokidhi hitaji hili muhimu la Kikatiba. (Tazama Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 19 Aprili, 2012 na 8 Novemba, 2012).

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu akijibu swalilangu la papo kwa papo juu ya Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, tarehe 8 Novemba, 2012 alisema kwamba, mfumo uliopo wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni mzuri. Jambo hili linaibua mashaka makubwa juu ya utayari wa Serikali kulinda haki ya mwananchi ya kupiga kura kama iliyotolewa na Katiba ya Nchi, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutokana na Wananchi kukosa haki ya kupiga kura kutokana na Daftari hilo kutofanyiwa marekebisho. Aidha, mtazamo huo wa Waziri Mkuu, hautoi fursa ya kulifanyia maboresho Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa wakati; na kwa maana hiyo, haki ya kupiga kura na demokrasia ya uchaguzi katika Taifa hili viro katika hatari ya kupotezwa au kupatikana kwa hisani ya watawala na siyo haki ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tangu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 kumefanyika chaguzindogo mbili za Ubunge katika Majimbo ya Igunga, Tabora na Arumeru Mashariki mkoani Arusha; aidha, kata kadhaa zimerudia chaguzi nchini kwa sababu mbalimbali. Katika Chaguzi hizi, Daftari la Kudumu la Wapigakura halikufanyiwa marekebisho na hivyo kuwanyima Wananchi wengi waliokuwa na sifa ya kuandikishwa na kupiga kura, haki ya kushiriki katika chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, ni kilio cha muda mrefu ndani ya nchi hii kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*), haiko huru na inafanya kazi zake kwa shinikizo la Viongozi waliopo madarakani. Kilio hiki kimethibitishwa na Tume yenyewe pale walipokutana na Tume ya Marekebisho ya Katiba wakati walipotoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, kuna mchakato wa maandalizi ya siri unaoendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) wa kuandaa utambuzi wa wapiga kura kwa kutumia mfumo wa “biometric” kwa maana ya kumtambua mpiga kura kwa alama za mwili kama alama za vidole na au mboni ya jicho kama sehemu ya maandalizi ya Uchagizi Mkuu ujao wa 2015.

Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, tayari Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeshaanza maandalizi mengi ya msingi bila hata vyama vya siasa kujua. Aidha, mchakato huu unaofanywa kwa siri kubwa na unaokisiwa kutumia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 200, tayari umeanza kutafutiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, teknolojia hii kwa siku za karibuni imetumika katika chaguzi nchini Ghana na Kenya. Kote huko, ilifeli na chupuchupu ingeyaingiza Mataifa hayo katika vurugu kubwa za uchaguzi. Mataifa haya yalilazimika kurudia mfumo wa upigaji na uhesabuji kura *manually*, hali iliyosababisha hofu kubwa.

Mheshimiwa Spika, si kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA haifiki matumizi ya teknolojia mpya kurahisisha na kuboresha mfumo mzima wa uchaguzi katika nchi yetu, bali inatambua athari kubwa zinazowezekana siku za usoni kama zoezi hili lillio *sensitive* halitafanywa katika misingi ya uwazi na ushirikishwaji wadau muhimu kama vyama vya siasa katika hatua zote la tangu awali kabisa.

Ni kwa sababu hizi basi, tunaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuwa ni sheria gani iliyotungwa na Bunge inayoruhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mfumo huu na ni bajeti ipi inatumika kutekeleza mpango huo? Na ni kwa nini mpango huo unafanyika kwa siri?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haioneshi dhamira ya dhati ya kusukuma mchakato wa kuleta marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ili kuondoa ukomo wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura (wa mara mbili kwa kipindi cha miaka mitano) na badala yake Daftari hilo liwe huru wakati wote kuandikisha wapigakura wapya wanaotimiza masharti ya kupigakura na kuingiza marekebisho ya taarifa za wapigakura wengine, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa kusikiliza na kuzingatia sauti na utashi wa watu na uzingativu wa kutosha wa dalili za nyakati na mazingira ya nchi pamoja na kuheshimu maono na falsafa za Waasisi wa Taifa letu, inakusudia kuleta Hoja Binafsi kuhusu marekebisho ya Sheria zote za Uchaguzi nchini ili kuinusuru haki ya Kikatiba ya Raia wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika chaguzi tena zilizo huru na za haki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Taifa kuwa katika mchakato wa kuandika upya Katiba ya nchi yetu, hakuna *guarantee* kuwa Katiba hiyo itakuwa tayari kwa ukamilifu wake kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015. Hivyo basi, ni bora hatua zote za urekebishaji wa viashiria vya mvurugano kuendelea kushughulikiwa sambamba na mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kiungwana kwa Viongozi wanaoondoka madarakani kukabidhi madaraka na ofisi kwa wale watakaoingia madarakani na katika ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa muda wa siku saba, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 42(1) kuwa, "*Rais Mteule atashika madaraka ya Rais mapema*

*iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwamba amechaguliwa kuwa Rais, lakini kwa hali yoyote itabidi ashike madaraka kabla ya kupita siku saba."*

Utaratibu huo haujatungiwa sheria na ni utaratibu ambaao ulikuwepo tangu enzi za chama kimoja na kwa misingi hiyo haukidhi mahitaji ya kipindi hiki cha vyama vingi endapo itatokea kwamba mgombea Urais kutoka Chama cha Upinzani atashinda uchaguzi na kuapishwa kushika madaraka ya Urais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi mbalimbali duniani zimeanzisha sheria ya kipindi maalumu cha mpito cha kukabidhiana madaraka ya Urais baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge;

Na kwa kuwa sheria kama hii huelekeza mtu atakayesimamia rasilimali za nchi ili kudhibiti ubadhirifu mkubwa ambaao hufanyika katika kipindi hiki cha mpito;

Na kwa kuwa nchi yetu imeridhia kipindi cha Uongozi wa Urais wenye ukomo wa miaka kumi;

Na kwa kuwa mfumo wetu wa Siasa ya Vyama Vingi sasa umekomaa na hivyo kutoa nafasi ya uwezekano wa Chama cha Upinzani kutwaa madaraka ya Dola;

Hivyo basi, ni jambo la busara sana kutunga Sheria ya Kipindi cha Mpito chenye kutoa muda wa kutosha na utaratibu utakaotumika kuruhusu kukabidhiana madaraka ya Urais na Serikali (*Presidential Transition Act*) kutoka utawala mmoja kwenda mwengine ili kuepusha migongano au hofu ya kutojua kitakachotokea.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuleta Hoja Binafsi Bungeni ili Bunge liazimie kutungwa kwa sheria hii muhimu sana kwa Taifa letu kwa sasa na hata kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, uchochezi wa kisiasa, udini, ukabila na ugaidi. Nchi yetu kwa miaka mingi imesifika sana duniani kutokana na tunu yake ya "Amani na Utulivu." Hata hivyo, tunu hii ya amani na utulivu iko mashakani baada ya kuibuka kwa matukio kadhaa ya uvunjifu wa amani yenye sura ya udini.

Mheshimiwa Spika, matukio hayo ni pamoja na mgogoro kati ya Waislamu na Wakristo huko Geita, Tunduma na kwagineko juu ya uhalali wa kuchinja ambapo watu kadhaa walijeruhiwa na wengine kuuawa. Matukio mengine ni kushambuliwa kwa viongozi wa dini akiwemo Katibu wa Mufti wa Zanzibar Sheikh Fadhil Soraga ambaye alimwagiwa Tindikali na watu wasiojulikana, Padre Ambrose Mkenda ambaye alinusurika kifo baada ya kupigwa risasa na kuvunjwa taya na Padre Evaristi Mushi ambaye aliuawa kwa kupigwa risasi tarehe 17 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, matukio haya ya kihalifu yenye sura ya kidini yalijumuisha pia kuchomwa moto nyumba za ibada hususan Makanisa huko Zanzibar na Dar es Salaam na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali. Aidha, matukio haya kuhuzunisha yalizua hofu kubwa miongoni mwa wananchi kwa kuwa hawakuwa na uhakika wa usalama wao.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa, mengi yameandikwa, mengi yamehubiriwa kwenye nyumba za ibada na vyombo vya habari. Lakini jambo moja ambalo halijasemwa wazi na ambalo tumekuwa na kigugumizi kulisemea, ni hili: Kwamba kwa kiasi kikubwa mgogoro huu wa kidini nchini, hasa mgogoro wa uchinjaji wa kitoweo, umechochewa na baadhi ya wanasiaya wa kutoka Chama Tawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Madhehebu ya dini yamekuwapo kwa muda mrefu nchini na katika kipindi chote hicho, hakujawahi kutokea mgogoro wa uchinjaji wa nyama kwa minajili ya kitoweo. Pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haina nia ya kutoa hukumu juu ya matukio haya, lakini ni vema Watanzania wakaelewa kwamba kwa vyovoyote iwavyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo ina dhamana kusimamia maisha yao, haiwezi kukwepa lawama katika kulikuza tatizo hili na kwamba imeshindwa kujua wajibu wake wa msingi wa kuilinda nchi na raia wake na kuhakikisha jamii yote inaishi kwa upendo na kuvumiliana. Uhalifu wowote unaotorea dhidi ya nchi na raia ni dalili ya wazi kabisa ya udhaifu wa Serikali iliyoko madarakani katika kutimiza wajibu wake. Utawala unaotumia dini kuwagawa wananchi wake na kutafuta ushindi ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Spika, uchochezi na propaganda za kidini na kikabila vilichagizwa kasi na CCM mara baada ya kuanza mfumo wa vyama vingi vyaa siasa kama mojawapo ya turufu yake ya kukabiliana na vyama vyaa upinzani. Uchochezi huu ambao tumeukemea mara kwa mara ulishika kasi katika uchaguzi wa mwaka 2005 na mwaka 2010. Vikundi kadhaa vyaa kidini vilifadhiliwa kuhubiri chuki dhidi ya dini nyingine waziwazi na kwa muda mrefu katika maeneo kadhaa ya nchi. Mihadhara, mahubiri na hata matamko ya hatari na uchochezi yalitolewa waziwazi hata kupitia vyombo kadhaa vyaa habari vyaa kidini na mitandao ya kijamii. Malalamiko mengi yalitolewa lakini Serikali ilifumbia macho tatizo hili kwani pengine ilionekana kuwa mpasuko na hofu inayotokana na propaganda hizo ulikinufaisha zaidi Chama Tawala na baadhi ya viongozi wake.

Mheshimiwa Spika, chuki na hofu hii iliyopaliliwa kisiasa sasa ndiyo inayoitesa nchi yetu na hakika linastahili kuwa somo kwa wanasiasa wote wa vyama vyote na hasa wale walioasisi uhalifu huu dhidi ya mstakabali mwema wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama vile hili halitoshi, sasa tunashuhudia kuibuka kwa uchochezi mpya wa kisiasa tena

wenye ubia kati ya chama kikubwa kinachoongoza na vyombo vya dola na kinachoitwa "Ugaidi".

Mheshimiwa Spika, vitendo viongozi wa dini kujeruhija na kuuawa kwa kupigwa risasi, kuchoma moto nyumba za ibada huko Zanzibar na Dar es Salaam ni Ugaidi kwa mujibu wa tafsiri ya Sheria ya Ugaidi ya Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa sana kuona kwamba Serikali haikuyachukulia matukio haya ya wazi ya kigaidi kama ni ugaidi ila imekuwa hodari sana kuchukua suala la mtu aliyebambikiwa kesi ya ugaidi kwa ushahidi wa kughushi kuwa yeze ndiye gaidi. Pili, Kwa mujibu wa Sheria ya Ugaidi, mtu ye yote anayefanya mawasiliano na gaidi au magaidi, yeze pia anahamasisha ugaidi na hivyo naye anastahili kuunganishwa katika tuhuma hizo za mashtaka ya ugaidi. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitika sana kuona wale wote waliokuwa wakiwasiliana na hao wanaoitwa magaidi ambaeo pia ni viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi na washirika wao hawajachukuliwa hatua yoyote. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaulaani mkakati huu wenye nia ovu ya kuffifisha demokrasia hapa nchini. Aidha, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, kamwe mpango huu haramu hautafanikiwa na naomba kuchukua nafasi hii kuonya kuwa vyama vya siasa vifanye siasa zake kwa ushindani wa sera na isiwe kwa mikakati ya kiharamia ya kudhuru, kubambikiza na kisha kutengeneza ushahidi kwa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama. Hili nalo likiachiwa likakomaa litaliingiza Taifa letu katika hatari nydingine ya machafuko. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari, ni dhahiri kwamba uhuru wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*), ni kichocheo muhimu sana katika kujenga na kukuza demokrasia katika Taifa lolote linaloamini katika haki. Hali kadhalika, uhuru wa kujieleza na kupata habari ni mionganini mwa haki za msingi za raia. Ibara ya 18 ya Katiba yetu inaweka msisitizo kwamba, kila raia wa Tanzania anao uhuru wa maoni na kueleza fikra zake, uhuru

wa kutafuta na kupokea habari na haki ya kufanya mawasiliano bila kuingiliwa katika mawasiliano yake.

Mheshimiwa Spika, matukio yaliyotokea mwaka jana peke yake katika tasnia ya habari ni kinyume cha katiba ya nchi lakini pia yanapingana na dhana ya Utawala Bora na kaulimbiu ya Serikali ya Uwazi na Uwajibikaji (*Transparency and Accountability*).

Mheshimiwa Spika, gazeti la Mwanahalisi limefungiwa kwa muda usiojulikana na Serikali. Muda usiojulikana maana yake, ni hadi mtawala atakapotaka na au hadi walifungia gazeti watakapojisikia kutaka kulifungulia.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, gazeti hili limefungiwa bila wamiliki wa kampuni inayochapisha gazeti hilo kupewa haki ya kusikillizwa. Mbali na kitendo hiki kuwataabisha wafanyakazi kadhaa walioajiriwa na kampuni inayochapisha gazeti hili, kitendo hiki vilevile kimewanyima mamilioni ya Watanzania haki yao ya kupata habari kwa mujibu wa Katiba. Kutokana na hali hiyo, ninaitaka Serikali itafakari upya uamuzi wake wa kulifungia gazeti hili ili kuondoa kiza na malalamiko kuwa gazeti la Mwanahalisi limefungiwa kwa sababu ya kulinda uhalifu dhidi ya waliomteka na kumtesa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Madaktari nchini, Dkt. Steven Ulimboka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika kadhia hiyo hiyo ya kuminywa kwa vyombo vy ya habari na uhuru wa habari, Mwandishi wa Habari Daud Mwangosi aliuawa kwa kupigwa kitu kilichohisiwa kuwa bomu na Polisi. Utata mkubwa umezunguka tukio hili na Polisi walewale ambao kwa mtazamo wa jumla ni watuhumiwa, wameachiwa mamlaka ya kuchunguza na kushtaki kuhusiana na kifo hiki.

Mheshimiwa Spika, kifo hiki kimelitia doa kubwa Taifa letu na zaidi kutokana na kitendo cha Serikali kuonekana kulinda wahalifu. Sina hakika kama watu walioshiriki katika kumpiga na kumuua Mwangosi wamekamatwa, ila nina hakika kuwa kifo chake kimepunguza wigo wa upatikanaji

habari katika Taifa na nina hakika limekuwa ni doa la Taifa.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iweze kujinasua katika lawama, shutuma na tuhuma kwamba ilihuksika katika kupanga njama za mauaji ya Mwangosi, ni vema itumie kupitia Rais, mamlaka yake ya kisheria kuunda Tume Huru ya kimahakama itakayochunguza kifo hiki na vingine kadhaa vyenye utata.

Mheshimiwa Spika, kilio hiki cha kuundwa kwa *Judicial Commission of Enquiry* kimekuwa cha muda mrefu na kila mwaka nazungumzia jambo hili katika hotuba zangu bila hatua zozote kuchukuliwa. Mara kadhaa, nimezungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani na nje ya Bunge, nimezungumza na Rais Jakaya Kikwete naye nimemwandikia na hata kuzungumza naye kuhusiana na haki hili ya msingi ya raia. Pamoja na wote kuahidi kuchukua hatua, hadi sasa hakuna hatua iliyochukuliwa hali inayoashiria Serikali kujua ukweli na pengine kuhusika na hivyo kulindana katika mauaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa pole kwa Ndugu Absalom Kibanda, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri ambaye pia ni Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Tanzania kwa maumivu na mateso makali aliyo yapata kutokana na watu wasiotaka kusikia uhuru wa kujieleza. Na kama ilivyo kwa matukio mengine kadhaa ya kuongezeka kwa utesaji wa aina hii, tunaitaka sasa Serikali itoe tamko rasmi la ni nani waasisi na watekelezaji wa mkakati huu wa kuzima uhuru wa wanahabari na vyombo vyao vya habari.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji wa kisiasa ni moja kati ya misingi ya utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Serikali inayofuata misingi ya utawala bora huwa inawajibika kwa mema na mabaya yanayotokea chini ya utawala wake. Ni vyema ikaeleweka kuwa hitaji la kumtaka kiongozi wa kisiasa kuchukua hatua za uwajibikaji wa kisiasa, pale jambo linalosababishwa na uzembe wa ama yeye binafsi, walio chini ya mamlaka yake na hata mfumo

anaousimamia, siyo jambo la chuki binafsi; narudia siyo jambo la chuki binafsi bali ni kielelezo cha uongozi unaojali, unaojutia madhila yaliyosababishwa na ulio tayari kujirekebisha ili yaliyotokea yasijirudie tena siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania siku zote hujikweza kama Serikali inayofuata misingi ya utawala bora lakini jambo la kushangaza ni kwamba kila mara viongozi wake wanakwepa kuwajibika kwa mambo mengi ya aibu yanayotokea chini ya utawala wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipiga kelele ikiwataka Mawaziri wa Serikali hii kuwajibika kwa kuijuzulu kwa kushindwa kutimiza wajibu wao wa kusimamia vyema kazi za Serikali lakini hakuna chochote kinachofanyika jambo ambalo limesababisha maovu kuendelea kufanyika na hivyo kuathiri ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilimtaka Waziri wa Mambo ya Ndani na Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini kuijuzulu kwa kushindwa kuzuia mauaji holela ya raia wasio na hatia yaliyofanywa na Polisi maeneo kadhaa hapa nchini lakini hakufanya hivyo. Tulinmtaka Waziri wa Elimu na Naibu wake kuijuzulu kwa kushindwa kusimamia mfumo wa Elimu hapa nchini jambo ambalo limepelekea kiwango cha wanafunzi wanaopata alama sifuri katika mitihani kuongezeka kila mwaka na hivyo kuweka hatarini mustakabali wa maisha ya wanafunzi hao na Taifa kwa jumla, lakini bado wameng'ang'ania madaraka. Tuliitaka Serikali kuwajibisha Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Morogoro na Iringa kwa kusimamia mauaji ya raia wasio na hatia lakini mpaka leo wanafurahia maisha kana kwamba hakuna kilichotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu ndiye Kiongozi Mkuu wa shughuli zote za Serikali. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo daraja kati ya Serikali Kuu na wananchi. Ni dhahiri kuwa Waziri Mkuu ndiye mtunza nidhamu na uwajibikaji mkuu katika Taifa hili. Ni nafasi ya uongozi inayostahili kuwa tayari kupokea lawama katika kufanya maamuzi magumu. Ni nafasi inayohitaji uwezo

wa kufanya maamuzi hayo mazito na kwa wakati kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa idadi ya makosa ya kizembe yanayotokea katika nchi hii na jinsi viongozi kadhaa wa Serikali hii wasivyowajibika tena kwa kubeza na kukejeli malalamiko ya mara kwa mara ya wananchi; kitendo cha Waziri Mkuu kukaa kimya wakati mwingu bila kutumia rungu lake la madaraka kulitetea au kuliokoa Taifa ni kigezo tosha cha kutafakari kama upole na uungwana wa Waziri Mkuu leo ni tija au fedheha kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Waziri Mkuu kwamba, Ofisi yake inategemewa sana kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania. Kwa misingi hiyo, Waziri Mkuu hana budi kuwa mstari wa mbele katika kujibu kero na matatizo ya wananchi kwa haraka kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, bado Taifa liko katika msiba mzito uliosababishwa na kuperomoka kwa ghorofa katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Ofisi ya Waziri Mkuu imekalia kwa muda mrefu bila kuchukua hatua stahiki ripoti kadhaa zilizotahadharisha kuhusu ujenzi holela wa maghorofa katika nchi yetu. Mbali na waliopelekwa Mahakamani, hakuna waliochukua hatua ya kuwajibika kisiasa/ kiutendaji. Hili ni janga kuu na ishara ya watendaji na viongozi wengi wa Serikali kutoikutambua kuwa nafasi zao za kazi ni dhamana waliyonayo kwa niaba ya Umma wa Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kutangaza mgogoro na Serikali kwa tabia hii ya kutowajibika, lakini napenda kuiasa Serikali kwamba kwa tabia hii inajitangazia mgogoro yenye na wananchi. Hili si jambo zuri kwani uvumilivu wa wananchi utakapofikia ukomo, Serikali isishangae kuona nguvu ya umma ikitumika kuwawajibisha viongozi wanaong'ang'ania madaraka huku wakiwa hawana sifa na weledi wa kufanya kazi za umma. Aidha, naomba kuwataka wananchi wasiendelee kutegemea "muujiza wa uwajibikaji" hivyo watafakari wenye na uwezo walio nao kuchukua hatua muda muafaka wa uchaguzi ukifika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa, mwaka 2012 takwimu zinaonyesha kuwa deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 15.2. Ndani ya mwaka mmoja wa fedha kutoka shilingi bilioni 18,258.62 Desemba 2011 na kuwa shilingi bilioni 21,028.61 Desemba 2012. Kati ya hizo deni la nje lilikuwa ni asilimia 75.97 na sababu inayotolewa kuwa ndiyo chanzo cha kuongezeka kwa deni hili kwa kasi namna hiyo ni pamoja na mikopo mipyä kwa ajili ya kugharamia miradi ya miundombinu hususani ya Barabara na Umeme na malimbikizo ya riba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali alieleze Bunge hili ni utaratibu gani uliotumika nje ya Bunge kuchambua na kuidhinisha matumizi hayo kwani bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya barabara ilikuwa ni shilingi trillioni moja (1) na bajeti nzima ya nishati ilikuwa shillingi billioni 502 kwa mujibu wa bajeti 2012/2013 ilhalii mkopo huu ulio katika deni la Taifa ni zaidi ya shillingi trillioni tatu (3)? Ni miradi gani mikubwa hivyo ya barabara na umeme ambayo iligharimiwa na fedha hizo kama kweli zilikopwa kwa ajili ya kuhudumia miradi hiyo?

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tume ya Mipango iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge Zima na Waziri, Mheshimiwa Stephen Wassira inaonyesha kuwa barabara zilizojengwa kwa kipindi hicho ni kilomita 170.6 ikilinganishwa na lengo na bajeti iliyopitishwa na Bunge ya kujenga kilomita 414 kwa mwaka 2012/2013 kwa barabara kuu kwa kiwango cha lami, hii ikiwa ni sawa na asilimia 41.2 tu ya lengo lilitokuwa limepangwa.

Aidha, ukarabati uliofanyika kwa barabara kuu ulikuwa kilomita 64.57, ikilinganishwa na lengo la kukarabati kilomita 135 kwa mwaka 2012/2013 na kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa barabara zinazounganisha Mikoa na Wilaya ni ujenzi wa kilomita 8.2 tu ndio umekamilika ukilinganishwa na lengo la kujenga kilomita 31.9 kwa mwaka kwa kiwango cha lami. Kwa upande wa ukarabati ni kilomita 99.45 tu zilikarabatiwa ikilinganishwa na lengo la kilomita 573.6

zilizokuwa zimepangwa kufanyiwa ukarabati (chanzo taarifa ya Ofisi ya Rais Tume ya Mipango).

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa miradi ya umeme ambayo ilitekelezwa ni pamoja na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi ambayo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kulipa fidia wanakijiji wapatao 3,092 na kwa upande wa mradi wa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira kwa ajili ya kuzalisha MW 200 ni stahiki za wafanyakazi kulipwa pamoja na sehemu tu ya madeni ya *CRDB, NSSF* na *PSPF* ndio viliweza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa taarifa hizi mbili yaani ya Waziri wa Fedha na ile ya Tume ya Mipango inaonyesha wazi kuwa kuna tatizo kubwa kuhusiana na suala la deni la Taifa, kwani upande mmoja unasema fedha hizo zillikopwa kwa ajili ya miradi ya umeme na barabara wakati upande wa Tume ya Mipango unaonyesha wazi kuwa hakuna miradi kama hiyo iliyoweza kutekelezwa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa hakuna Kitengo/Idara ya Madeni na sasa ndiyo Serikali ipo kwenye mchakato wa kuanzisha Idara ya Madeni ambayo pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu na kuhakikisha usimamizi madhubuti wa deni la Taifa. (Chanzo: Taarifa ya Waziri wa Fedha juu ya mwongozo, matazamio na upeo wa bajeti ya Serikali kwa Bunge 2013/2014, tarehe 25 Machi 2013).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, alieleze Bunge na Taifa, kwa kuwa haikuwepo Idara kwa ajili ya uchambuzi juu ya mikopo hii, nani alikuwa anahuksika na kusimamia ukopaji huu na hasa kuhusiana na riba kwani katika taarifa hiyo takwimu zinaonyesha kuwa fedha iliyolipwa kwa ajili ya deni la nje kama riba tu ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 66.1 wakati deni halisi tulilipa kiasi cha shilingi bilioni 35.5 na hivyo tulilipa jumla ya shilingi bilioni 101.56 kwa deni hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa deni la ndani tulilipa kiasi cha shilingi bilioni 1,044.85 na kati ya fedha hizo tulilipa riba ya kiasi cha shilingi bilioni 210.7 tu. Je, riba halisi kwa ajili ya mikopo hiyo tuliyochukua ilikuwa ni kiasi gani kwa mwaka? Je, madeni mapya riba yake iko kiasi gani kwa mwaka? Ni kitengo gani kilihalalisha uchukuaji huu wa mikopo hiyo? Ni vyema sasa taarifa rasmi ya madeni ya Taifa yawe yanawekwa hadharani ndani ya Bunge kwani kuna hisia ya kuwepo ujisadi wa kutisha kupitia akaunti ya madeni ya nje kama ilivyokuwa kwa akaunti ya *EPA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, gesi asilia, Waziri Mkuu akiwa ndiye Msimamizi na Mdhibiti wa shughuli za kila siku za Serikali ndani na nje ya Bunge, anapaswa kutoa maelezo kuhusu hali inayoendelea hivi sasa katika sekta ndogo (*sub sector*) muhimu kwa nchi yetu ya gesi asili kuhusu mazungumzo yanayoendelea na makampuni mbalimbali ya kimataifa na mikataba inayozidi kusainiwa huku kukiwa na ombwe la kisera na udhaifu wa kiuongozi katika sekta hizo nyeti hali ambayo itakuwa na athari za muda mrefu sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kwa mfano nchi haina Sera ya Gesi Asili huku Sera ya Nishati ikiwa imepitwa na wakati, lakini mazungumzo yanaendelea na mikataba inazidi kusainiwa bila kuwa na mfumo thabiti wa kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi zinanufaisha wananchi wa maeneo husika kwa ridhaa yao.

Aidha, kumekuwepo na ujisadi kama ambavyo ulielezwa pia katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni Novemba 2011 ambayo msingi wake ulikuwa pia madai ya Kambi ya Upinzani ya Julai 2011; hata hivyo mpaka sasa sehemu kubwa ya maazimio ya Bunge toka wakati huo mpaka sasa hayajatekelezwa kwa ukamilifu. Wakati ujisadi huo ukiwa haujashughulikiwa, yameibuka madai mengine ya kasoro katika mkopo wa ujenzi wa Bomba la Gesi, huku kukiwa pia na tuhuma za usiri katika mkataba huo ikiwemo kuhusu dhamana na masharti mengine yaliyoko kwenye mikataba ya ujenzi wa bomba husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo mwezi Februari 2013 katika maswali ya papo kwa papo Bungeni, nililiza swalii kwa Waziri Mkuu iwapo mikataba hiyo sasa inaweza kutolewa kwa Bunge na kwa Wabunge na kuahidi kwamba Wabunge wanaweza kupata nakala hiyo kwa kufuata masharti ya Sheria, naomba ninukuu kauli yake:-

*"Serikali imekwisha kubali kwamba, Bunge hili linayo fursa ya kupata mkataba wowote, kubwa ni kufuata utaratibu kupitia ofisi ya Spika".*

Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia kwa Waziri Kivuli wa Nishati na Madini alitumia Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kuomba kuona nakala ya mkataba wa ujenzi wa bomba husika ili kutekeleza wajibu wa Kibunge wa kuishauri na kuisimamia Serikali lakini toka wakati huo mpaka sasa mikataba hiyo imeendeelea kufanywa kuwa ni siri hata kwa Wabunge. Hata baada ya mazungumzo kati ya Rais wa Tanzania na Rais wa China masuala hayo yameendelea kufanywa kuwa siri. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Bunge hili inaitaka Serikali kuweka wazi masharti ya mikopo na dhamana zinazohusika kwa kuzingatia kwamba mwelekeo unaonyesha kuwa miradi ya chuma na makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga imetumika kama sehemu ya mpango wenye kuacha maswali mengi kuhusu unyonyaji wa rasilimali za Taifa katika sekte hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika, udhaifu huo unapaswa kurekebishiwa kwa kuongeza jitihada za kutekeleza ahadi za kuhakikisha kwamba matumizi ya gesi katika viwanda vyta mbolea, viwanda vyta bidhaa za kemikali zinazotokana na mafuta (*petrochemicals*), saruji na uzalishaji wa umeme katika Mikoa ya Mtwara, Iringa, Ruvuma, Dar es Salaam na maeneo mengine yanayohusika. Pamoja na Serikali kuingia Makubiliano ya Awali (MOU) na Kampuni ya kutoka nchini Marekani ya Symbion kuhusu uzalishaji wa umeme Mkoani Mtwara, ieleze pia hatua ilizochukua katika kurekebisha kasoro zilizopo kwenye miradi ya Mchuchuma na Liganga na Mnazi Bay kwa kuzingatia ahadi ilizotoa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na kutaka maelezo zaidi na vielelezo vyta ziada kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa bomba la gesi na matumizi ya gesi; inatoa mwito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania kwa ujumla kufungua mjadala mpana zaidi wa kitaifa kuhusu gesi kwa kujikita katika suala la ubovu wa Sera ya Gesi na mchakato unaoendelea hivi sasa kuhusu Rasimu ya Sera hiyo na uozo wa mikataba kwenye utafutaji, uvunaji na usafirishaji wa gesi. Serikali badala ya kuendelea kukimbilia kusaini mikataba mipyä kuhusu utafutaji wa gesi asili na mafuta ishughulikie kwanza ubovu wa mikataba ya utafutaji wa mafuta na gesi kuweka hadharani ripoti ya uchunguzi kuhusu mikataba 26 ambayo ilikamilika tangu mwaka 2012 na kueleza hatua ambazo zimechukuliwa toka wakati huo.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni muhimu kwa kuwa toka kusomwa kwa orodha ya mafisadi (*list of shame*) tarehe 15 Septemba 2007 mpaka sasa yamekuwa yakitolewa madai mbalimbali kuhusu baadhi ya viongozi na watendaji kutuhumiwa kufanya ujisadi kupitia mikataba ya utafutaji na uvunaji wa gesi asili, utafutaji wa mafuta na uchimbaji wa madini na kufichwa kwa fedha katika akaunti za nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Rais wa China ambayo ilihusisha usiri katika kusainiwa kwa mikataba 17 ya Sekta mbalimbali imedhihirisha kwa vitendo kwamba Serikali inayoongozwa na CCM isivyo na dhamira ya kutekeleza Maazimio ya Bunge kuhusu usimamizi wa Kibunge kwenye michakato ya mikataba. Wabunge na wananchi wakumbuke kwamba mwaka 2008 kufuatia kashfa ya Richmond, Bunge lilipitisha Azimio kwamba Kamati za Kisekta za Bunge zihusishwe kwa niaba ya wananchi kwenye maandalizi ya mipango na mikataba kuanzia hatua za awali ili kuishauri na kuisimamia Serikali; Azimio ambalo halitekelezwi na hivyo kuibua migogoro kati ya wananchi na wawekezaji na maeneo mengine kufanya nchi kuingia mikataba mibovu.

Mheshimiwa Spika, mathalani, wakati Tanzania imekopa mkopo mkubwa kutoka China kwa ajili ya ujenzi

wa Bomba la Gesi; miaka michache iliyopita kutokana na udhaifu wa mipango na mikataba ulifanyika ujenzi wa Bomba lingine kutoka Songosongo chini ya kampuni ya Songas kwa mkopo. Hata hivyo, katika mradi huo kulijengwa bomba lenye kipenyo kidogo na matokeo yake ni kwamba miaka michache baadaye Taifa linaingia gharama kubwa ya mkopo mwingine kutokana na upungufu wa miundombinu ya gesi asili huku kukiwa na mzigo wa madeni makubwa ya mikopo ya awali. Serikali inapaswa kutoa maelezo kuhusu hatua ilizochukua kurekebisha hali hiyo toka wakati huo na kuhakikisha uwajibikaji wa viongozi na watendaji walohusika ambapo wengine mpaka sasa bado wako katika ofisi za umma.

Mheshimiwa Spika, Bunge kama mhimili wa kuisimamia na kuishauri Serikali. Mamlaka ya Bunge yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara za 62 hadi 64. Ibara hizi zote zinaeleza majukumu ya Bunge juu ya kusimamia utendaji mzima wa Serikali katika mchakato wa kuwapatia huduma za msingi wananchi.

Mheshimiwa Spika, jukumu hili kwa hali ilivyo sasa linashindwa kutekelezeka kutokana na ukweli kwamba Bunge linakosa taarifa au uelewa wa kutosha kuhusu sekta mbalimbali za kiutendaji. Kwa hali ya kawaida ni vigumu kumshauri au kumsimamia mtu bila ya kuwa na uelewa wa ziada kumzidi yule unayemshauri au kumsimamia.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 64 ni lazima Kurugenzi husika ndani ya Bunge kuwezeshwa kuwa na watendaji wanaoweza kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge kutimiza matakwa ya Ibara hiyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka kuelewa toka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Miswada Binafsi ya Waheshimiwa Wabunge Zitto Kabwe uliohusu Mabadiliko ya Sheria ya Maadili ya Viongozi na John Mnyika uliohusu Uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa ambayo tayari imekwishawasilishwa Ofisini kwa Katibu

wa Bunge ni lini italetwa rasmi Bungeni kwa utaratibu wa kuzifanya ziwe sheria za nchi?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilieleza kuhusu Watendaji wa Serikali kushindwa kutimiza masharti ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Haki na Madaraka ya Bunge mwaka 1988 na marejeo yake ya mwaka 2002. Hali ya kutokuheshimu sheria hii bado inaendelea, Waheshimiwa Wabunge wameomba kupatiwa nyaraka mbalimbali toka Serikalini kuititia kwa Katibu wa Bunge, lakini kwa bahati mbaya hadi sasa nyaraka hizo bado hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, je, Bunge linawenza kukidhi matakwa ya Ibara za 63? Utaishauri vipi na kuisimamia Serikali ukiwa huna taarifa za kutosha? Je, ni mara ngapi Waheshimiwa Mawaziri wametoa majibu ya kudanganya na kupelekea Waheshimiwa Wabunge kukiambia Kiti kuwa Waziri hajajibu swali lake? Mapungufu haya yote yanababishwa na kutokuwepo kwa taarifa sahihi na za ziada kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi ili kukidhi matakwa ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, katika moja ya taarifa za asasi za kiraia zinazofuatilia mwenendo wa Bunge, pamoja na mambo mengine zimeonesha kuwa Bunge letu ni dhaifu na kuwa halitekelezi majukumu yake. Taarifa za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*) na *The Citizens' Parliament Watch (CPW)* za Februari 13, 2013 zimeonesha kuwa:-

*"...kumeendelea kuwa na mivutano yenyeye upendeleo wa vyama katika kujadili na kuchangia hoja na kuonekana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeleviti wa vikao kutumia vibaya kanuni za Bunge kuwadhibiti Wabunge kulingana na vyama vyao. Ukiukwaji wa Kanuni za Bunge, matumizi mabaya ya muda na kukosa tija kumeendelea kuliathiri Bunge letu. Aidha, baadhi ya Wabunge wamekuwa na matumizi ya lugha zisizostahili Bungeni na hata kushambuliana katika ubinafsi wao. Wakati Wabunge wengine wakitumia muda wao nje ya Bunge kukutana na*

*wananchi na kueleza ufanisi wao ndani ya Bunge, wengine wametumia nafasi hizo kupingana na wananchi na kulidhallishaa Bunge mbele ya jamii".*

Mheshimiwa Spika, Asasi hizi zinatukumbusha mambo muhimu sana kwa jamii yetu. Tuna kila wajibu wa kuwatendea haki watu wetu na kutafakari taarifa zinazotupima utendaji wetu na kuchukua hatua kurekebisha udhaifu huu.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ya kukumbusha. Mara kadhaa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA imekuwa ikiitaka Serikali kutekeleza mambo ya msingi katika ustawi na maendeleo ya Taifa hili lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba Serikali hii ya CCM inayojiita sikuvi imeendelea kuziba masikio yake juu ya mahitaji muhimu kwa Taifa. Kwa mfano, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa pendekezo zuri la kuwapatia wazee wote pensheni (*Universal Pension*) sambamba na kuwa na mpango maalum wa kuwawezesha wazee wetu hawa kuishi maisha ya amani katika siku zao za izeeni.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kambi ya Upinzani kuonesha njia ya kupata fedha za kuwalipa wazee hawa, lakini mpaka leo Serikali imekuwa na kigugumizi cha kutekeleza nia hii njema. Jambo hili linapelekea Kambi ya Upinzani iamini kwamba Kauli aliyoitoa Waziri Mkuu, tarehe 01 Oktoba, 2009 wakati akiwahutubia wazee kwamba: "*Wazee ni rasilimali na hazina kubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta mabadiliko ya kiuchumi*" ilikuwa ni kuwakejeli na kuwahadaa wazee waliovuja jasho kuijenga nchi hii hadi hapa ilipo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieletez ukweli ili wazee hawa wajue kama Serikali imeamua kuwatupa wajitafutie utaratibu mwingine wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipiga kelele sana juu ya matumizi mabaya ya fedha za umma unaofanywa na Serikali kwa kisingizio cha uendeshaji wa shughuli za Serikali. Limekuwa ni jambo la kawaida kwamba katika bajeti ya Waziri Mkuu na Wizara nyiningine, fedha za matumizi ya kawaida ni takribani asilimia

80 wakati fedha za maendeleo ni takriban asilimia 20 tu. Jambo la kushangaza hapa ni kwamba hata hii asilimia 20 ya fedha za maendeleo, zaidi ya nusu zinatoka kwa wahisani. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iueleze umma wa Watanzania: Kipi ni kipaumbele; kutumia fedha za walipa kodi wa Tanzania kwa matumizi ya ofisi au kuwaletea wananchi maendeleo?

Aidha, ni vyema Serikali ikaeleza Taifa ni njia gani inatumia kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwani kila siku tunaona kukua kwa kutisha kwa matumizi ya kawaida ya Serikali. Ni dhahiri hakuna uchungu na fedha za walipa koda kwa Serikali hii ya CCM.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kuikumbusha Serikali ni kuhusu Sherehe za Kitifa. Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukihoji matumizi yasiyofanyiwa ukaguzi ya sherehe za kitaifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka bayana matumizi ya fedha katika Sherehe za kitaifa kuwa fedha inayotumika ni fedha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha tena Serikali kusema ukweli kuhusu dhamira ya kuhamia Dodoma. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri tena Serikali kufuta mpango huu kwani ni upotezaji wa fedha za wananchi na fedha zinazopotezwa zielekezwe kwenye mipango mingine ya maendeleo na Dodoma iendelee kuwa mji wa Kibunge na Elimu kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikishauri kila wakati.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti 2012/2013 na uchambuzi wa bajeti ya 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 35.2 ikiwa ni matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.4 ilikuwa ni mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 10.6 ikiwa ni ruzuku kwa taasisi na shilingi bilioni 21.1 matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari 2013, shilingi bilioni 20.7 sawa na asilimia 59 zilikuwa zimepokelewa kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Ofisi ya Waziri Mkuu ilitengewa shilingi bilioni 91.7 lakini hadi kufikia Februari, 2013 ni kiasi cha shilingi bilioni 10.7 sawa na asilimia 11.7 zilizokuwa zimetumika katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mchanganuo huo ni kwamba fedha za matumizi ya kawaida zinatumika zaidi kuliko fedha za maendeleo. Aidha, karibu asilimia 90 ya bajeti ya maendeleo, Ofisi ya Waziri Mkuu haikutekelezwa hadi kufikia Februari 2013.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mkuu atoe majibu kuwa inawezekanaje hadi kufikia "quota" ya tatu (3) ya mzunguko wa bajeti, asilimia 90 ya bajeti ya maendeleo haijatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 35.08 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 43.87 kwa bajeti ya maendeleo. Wakati matumizi ya kawaida yamepungua kwa asilimia 0.34 ukilinganisha na mwaka 2012/2013, bajeti ya maendeleo imepungua kwa asilimia 52.2 ukilinganisha na mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, licha ya bajeti ya maendeleo kupungua kwa zaidi ya nusu ukilinganisha na mwaka jana bado imeendelea kuwa tegemezi kwa wahisani. Katika shilingi bilioni 43.87 za maendeleo, shilingi bilioni 37.87 sawa na asilimia 86.3 ni fedha za nje na shilingi bilioni sita (6) sawa na asilimia 13.7 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haiamini kama tunaweza kupata maendeleo ya kweli kwa kutegemea fedha za wahisani katika bajeti za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya meaendeleo imetengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya uendelezaji wa kuzikia viongozi wa Kitaifa. Kambi ya Upinzani inataku kujua kama ni ombi la viongozi wa kitaifa kuandaliwa eneo

maalumu la kuzikwa au ni utashi wa Serikali kufikiri kwamba viongozi wa kitaifa wanahitaji eneo maalumu la kuzikwa!

Kwa uzoefu ni kwamba waasisi wa Taifa hili walizikwa kwenye makazi yao. Kwa nini viongozi wa kitaifa walio hai sasa wasifuate mfano huo? Hivi kweli kuna mantiki yoyote ya kutumia shilingi bilioni moja ya kuandaa sehemu ya kuzikia watu ambaao hawajafariki wakati kuna watu wenye njaa, wagonjwa, wamama wajawazito wanaojifungulia sakafuni ambaao wanahitaji huduma ya matibabu na dawa ili wapone?

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo, Kitengo cha Maafa kimetengewa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa. Mheshimiwa Spika, Watanzania wameshuhudia maafa makubwa katika nchi yetu hasa ya kuzama kwa Meli kwa mfano Meli ya MV Bukoba, Meli ya MV Skagit na Meli ya MV Spice Islanders huko Zanzibar na pia wameshuhudia kuperomoka kwa maghorofa na mengine kuungua moto. Katika ajali na maafa haya Watanzania wengi walipoteza maisha yao na daima waokoaji wa ndani wamekuwa na uwezo mdogo sana wa kuokoa watu na hivyo kutegemea zaidi waokoaji na vifaa toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa fedha hizi ni ndogo na hivyo ni vyema Serikali ileze uwezo huo unaokusudiwa kujengwa ni upi!

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza gharama za uendesha wa shughuli za Serikali, Kambi ya Upinzani imekuwa ikipinga matumizi mabaya ya fedha za umma na hasa posho za vikao (*sitting allowances*) kwa kuwa vikao ni sehemu ya majukumu yao ambayo wanalipwa mshahara. Kambi Rasmi ya Upinzani inazidi kusisitiza kuwa posho za vikao zifutwe kwani zinaongeza gharama za uendeshaji wa Serikali ambazo si za lazima.

Mheshimiwa Spika, jedwali lifuatalo linaonesha tofauti ya posho za vikao katika kasma 210314 kwenye Fungu 37 kwa

Idara zilizo Ofisi ya Waziri Mkuu kati ya mwaka wa bajeti 2012/2013 na 2013/2014.

### **Chanzo: Randama Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37**

KASMA	IDARA	POSHO YA VIKAO - 2012/2013	2013/2014
<b>210314</b>	Utawala	95,000,000	92,000,000
	Fedha na Uhasibu	20,250,000	8,850,000
	Sera na Mipango	31,500,000	19,950,000
	Ukaguzi wa Ndani	17,400,000	17,400,000
	Habari, Elimu na		
	Mawasiliano	3,000,000	3,000,000
	Ugavi	20,000,000	42,000,000
	Sheria	1,500,000	1,200,000
	Menejimenti ya		
	Mifumo ya Habari	800,000	600,000
	Uratibu wa Maafa	39,000,000	39,000,000
	Maadhimisho ya		
	Sherehe za Kitaifa	47,000,000	47,000,000
	Bunge na Siasa	15,000,000	16,000,000
	Maendeleo ya		
	Sekta Binafsi	24,000,000	43,500,000
	Uratibu wa Shughuli		
	za Serikali	100,500,000	61,500,000
	Mpiga Chapa wa		
	Serikali	55,100,000	53,000,000
	<b>470,050,000</b>		<b>445,000,000</b>

Mheshimiwa Spika, tofauti kati ya matumizi ya mwaka wa fedha 2012/13 na 2013/14 ni shilingi 25,050,000/-

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI kuhusu Mpango wa Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Kanuni ya 99(9).

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kutoa pole kwa wananchi wangu wa Tunduma kutohana na vurugu kubwa za kidini zilizotokea hivi karibuni kati ya tarehe 30.03.2013 mpaka 06.04.2013 za mgogoro wa uchinjaji wa nyama kati ya dini kubwa mbili za Kikristo na Kiislam zilizopelekea wananchi wengi kuibiwa mali zao, wengine kujeruhija kwa kupigwa na Polisi, kubambikiziwa kesi na mmoja kufariki katika mazingira ya kutatanisha. Nitoe pongozi kwa viongozi wa dini za Kikristo na Kiislam na wananchi kwa kumaliza mgogoro katika awamu ya kwanza huku tukisubiri msimamo wa Serikali, nami kama mwakilishi wenu nipo nanyi katika kipindi hichi chote cha matatizo na kulishughulikia mpaka tutakapopata suluhu ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwepo wangu hapa Bungeni ni kwa ajili ya mchango mkubwa wa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Mbozi Magharibi, natoa shukrani na ninaomba tuendelee kuwa na ushirikiano kwani sasa hivi ndio kipindi kinachohitaji utulivu na mshikamano mkubwa katika kujenga Jimbo letu. Nguvu ya Umma mara zote ndiyo inayoshinda hata kama kutakuwepo na ghiliba na udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa naishukuru kwa uvumilivu na upendo familia yangu, wanangu mapacha Ernest na Ernesto Che Guevara pamoja na mchumba wangu Mariam Ibrahim (mama wawili). Ninawaambia nipo pamoja nao kwa sala na maombi na Mwenyezi Mungu atawalinda kila siku na atawalipa kwa kadiri watakavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kuangalia baadhi ya masuala kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni vyombo vyta wananchi ambavyo vipo katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Serikali za Mitaa huwawezesha wananchi kuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali ama kwa kushiriki moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi wao katika shughuli za maendeleo na utawala. Serikali za Mitaa zinatokana na dhana ya madaraka kwa umma. Dhana na madhumuni ya madaraka kwa umma ni kuwapa wananchi (wanaume na wanawake) wote uwezo na fursa sawa ya kushiriki kikamilifu katika masuala ya siasa, uchumi na utawala katika nchi yao. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa jamii ni utaratibu uliotokana na Sera ya Serikali kutoa nafasi kwa jamii kuchukua majukumu zaidi kwa maendeleo yao katika kufanya maamuzi kuchagua mradi wa jamii, kupanga, kutekeleza, kutawala, kudhibiti na kuongoza ili kuleta maendeleo. Hiki ni kiini macho kilichopo kwenye makaratsi kwani maamuzi hasa ya maendeleo yanaamuliwa toka ngazi za juu za utawala.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Serikali ya Kijiji. Mkutano Mkuu wa Kijiji ni chombo cha utawala kinachoundwa na wajumbe wafuataao:- Wakazi wote wa Kijiji wenyewe umri usiopungua miaka 18 na wenyewe akili timamu; Mwenyekiti wa Kijiji; Wenyeviti wa Vitongoji vyote kijijini; Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji amba ni kati ya 15 na 25; Afisa Mtendaji wa Kijiji – Katibu. Kwa mujibu wa kifungu cha 103 (2) cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982. Mkutano Mkuu wa Kijiji huitishwa mara mmoja kila baada ya miezi mitatu. Kwa mujibu wa kifungu cha 141 cha Sheria Namba 7 ya

mwaka 1982. Mkutano Mkuu ndiyo Mamlaka yenyeye madaraka ya juu kabisa kuhusu maamuzi yote ya sera na maendeleo kijiji na ndiyo yenyeye wajibu wa kuwachagua na kuwaondoa madarakani wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji ikiwa ni pamoja na kutekeleza majukumu mbalimbali iliyopewa kwa mujibu wa sheria hii na nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa muundo huu wa Serikali ya Kijiji unatoa mamlaka kwa umma kufanya maamuzi yanayohusu matumizi ya rasilimali zao ni mzuri na kwenye maandishi hauna tatizo lakini kwa uhalisia muundo huo sio unavyofanyakazi bali mwenye mamlaka makuu katika mfumo huo ni Mtendaji wa Kijiji, ambaye ni mwajiriwa wa Serikali na mara nyingi yeye sio mwenyeji wa Kijiji hicho na hivyo anaweza kutumia vibaya rasilimali za kijiji na mwisho akapewa uhamisho na kwenda sehemu nyingine. Huu ni udhalfu mkubwa katika uhalisia wa muundo.

Mheshimiwa Spika, wajibu na majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji ni kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali; kupokea na kujadili mapato na matumizi ya fedha; kupokea na kujadili taarifa za makusanyo ya fedha yakiwamo ya ushuru, ada na mapato mengine yanayopaswa kukusanya ndani ya kijiji kwa mujibu wa sheria; kupokea na kujadili taarifa za watu walioomba kupewa ardhi; kupokea maagizo (kama yapo) kutoka ngazi za juu za Serikali na kuweka mkakati wa utekelezaji; kufanya maamuzi yanayozingatia demokrasia; kuchagua Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji; kujadili na kuitisha bajeti na mipango ya maendeleo ya Kijiji; pamoja na mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi inaonyesha kuwa wananchi wanauelewa mzuri wa sheria hiyo hapo juu kuliko watendaji wa Serikali wanaotakiwa kusimamia sheria hiyo. Kumekuwepo na migogoro mingi sana hapa nchini wakati wananchi wanapotimiza wajibu wao wa kisheria katika kuwaondoa viongozi wabadirifu katika nafasi zao, lakini kwa masikitiko makubwa watendaji wa Serikali (Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya, *OCD*) badala ya kuheshimu maamuzi

yanayofanywa na wananchi wamekuwa wakiwatisha wananchi kwa kuwapiga na kuwaweka mahabusu na kuwafungulia kesi ili kuwalinda wahalifu.

Mheshimiwa Spika, mifano ya hayo ni mingi sana kama ilivyotokea katika Wilaya mpya ya Mombasa Kata ya Kamsamba na Wilaya ya Hanang' katika Kata ya Basutu kijiji cha Basotu tarehe 20.02.2013 na 21.02.2013 ya kudai taarifa za uwajibikaji wa uongozi wao na mwisho wa kikao wananchi waliamua kufunga ofisi yao ya kijiji mpaka Mkuu wa Wilaya afike kutatua tazito hilo. Aidha, kuna mgogoro ulitojitokeza kijiji cha Ruaha (Kilosa) baada ya wananchi kumwondoaa Mwenyekiti kwa kura ya kutokuwa na imani naye lakini baadaye CCM, Serikali na Jeshi la Polisi wakaanza unyanyasaji kwa raia hali inayoendelea mpaka hivi sasa. Mgogoro huo unaeleweka vyema na Serikali inaelewa kabisa haki imeminywa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya na kwa mtendaji huyo wa Serikali kutokujua taratibu na sheria zinazowalinda wananchi aliamuru kukamatwa kwa wananchi waliokuwa wasemaji na waliota taarifa ya ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa watendaji wa namna hiyo wanachukuliwa hatua za kinidhamu kwani inaonyesha kuwa hawaelewi nini wanatakiwa kusimamia, hivyo basi sheria na maamuzi ya wananchi katika kuwajibisha viongozi wezi yanaheshimiwa na watendaji wa Serikali pamoja na vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Chaguzi za Vijiji na Mitaa badala ya mfumo wa sasa ambao chaguzi zinaendeshwa kwa kanuni tu zilizotungwa na Waziri wa TAMISEMI na hivyo kuleta upungufu na migogoro mingi kwenye chaguzi. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa chaguzi za 2009 ziligubikwa na kasoro nydingi na kasoro hizo hazijarekebishwa toka wakati huo na zimeendelea kuleta

matatizo katika chaguzi za marudio za vijiji na mitaa mwaka 2010, 2011, 2012 na chaguzi zilizofanyika katika baadhi ya maeneo mwaka huu wa 2013.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa mwaka 2014, tumebakiza muda mfupi kutokana na ukweli kwamba takriban mchakato wa kupatikana kwa Katiba Mpya utachukua muda mwingi, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iharakishe kuleta Muswada huo wa sheria mwaka huu wa 2013 katika mukutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa bado kuna maeneo mengi ambayo hakujfanyika chaguzi za marudio za udiwani, vijiji na mitaa pamoja na nafasi kuwa wazi kwa muda mrefu. Kwa mamlaka ya kisheria, TAMISEMI ndiyo inayopaswa kusimamia hadi chaguzi hizo zinafanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kuhakikisha Wakurugenzi wanatimiza wajibu wao wa kuanzisha mchakato wa kuitishwa kwa chaguzi hizo haraka kabla ya muda wa kuanza kwa chaguzi nyingine hapo mwakani, kwani kusubiri hadi chaguzi zingine ni kuwanyiwa wananchi haki yao ya uwakilishi katika mchakato mzima wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, ugatuaji wa madaraka. Dhana nzima ya kugatua madaraka ni kutimiza matakwa ya kikatiba yanayosema wazi kuwa Tanzania ni nchi yenye Serikali za aina mbili, kwa maana ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na majukumu ya Serikali za Mitaa tayari nimekwishayataja hapo juu nayo ni kwa mujibu wa Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Pia Ibara ya 6 ya Katiba inakwenda mbali na kutambua mtu ye yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali yoyote.

Mheshimiwa Spika, maelezo au ufanuzi wa utendaji kazi wa Serikali za Mitaa umetolewa katika sheria zilizotungwa na Bunge, yaani sheria ya "*the Local Government (District Authorities) Act, and the Local Government (Urban Authorities) Act*" ya mwaka mwaka 1982. Katika taarifa ya

utafiti wa utekelezaji wa sheria hizo hapo juu (*Report on Local Government Decentralization Mandates*), unaonyesha Serikali Kuu imeshindwa kuweka mkakati uliowazi na makini wa kufanikisha matakwa ya Kikatiba na Kisheria na katika uchambuzi huo kwa ngazi ya mkakati wa utekelezaji umeeleza kuwa:

*"There is no explicit implementation plan regarding decentralisation. The separation between central government matters and local affairs is not established".*

Mheshimiwa Spika, vigezo au viashiria vilivyoonyesha kushindwa kwa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa mujibu wa andiko hilo ni: *Transfer of competencies and sector-based policies*: Serikali za Mitaa hapa nchini sio taasisi inayojitegemea kama inavyotakiwa kuwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria, uhawilishwaji wa rasillimali watu katika Serikali za Mitaa ni matakwa ya Serikali Kuu na si matakwa ya Serikali za Mitaa. Pili, uteuzi na ajira kwa watumishi hufanywa na Serikali Kuu kupitia kwa kilinachoitwa- "*Local Government Service Commission*". Hivyo jambo hilo husababisha mamlaka za Serikali za Mitaa kutokuwa na uwezo wa kuajiri au kufukuza mtumishi hadi pale Mamlaka iliyofanya uteuzi au uajiri kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya sababu za kushindwa kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi kwa Halmashauri nyingi hapa nchini, inatokana na kukosa au kutokuwa na uwezo kwenye utawala na fedha katika kutoa maamuzi yanayohusu maendeleo ya Halmashauri zao. Badala yake maamuzi mengi ya kiutawala na kifedha yanatolewa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, nyenzo muhimu inayotumiwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa inazidi kuhodhi madaraka ya Serikali za Mitaa ni kuhodhi Watumishi Waandamizi (Senior Staffs) wa Serikali za Mitaa walio kwenye sekta za utawala, afya, fedha, kilimo na kadhalika, wote hawa huteuliwa kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Mwanazuoni aitwaye Lytou Bouapao, *Director General Department of Planning and Cooperation*, Wizara ya Elimu katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa LAO iliyopo Mashariki ya Mbali alitoa uchambuzi wa maneno haya: Dhana ya ugatuaji kwa kuipunguzia mzigo Serikali Kuu (deconcentration): Hapa akimaanisha; “*Concept of Deconcentration: Authority is devolved to administrative levels closer to the institutional operations, but administratively under the authority of the central organization.*

• *Concept of Decentralization: Authority is devolved to administrative levels closer to the institutional operations administratively, but with a high degree of autonomy in relation to the authority of the central organization”.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na dhana hiyo hapo juu, ukweli ni kwamba kinachotokea hapa kwetu sio ugatuaji wa madaraka halisi bali ni uhamishaji wa shughuli za utendaji wa Serikali lakini maamuzi yote bado yanashikiliwa na kuhodhiwa na Serikali Kuu. Hivyo basi, ni dhahiri demokrasia ya kweli kwa wananchi haiwezi kupatikana kwani maamuzi ya watu hata siku moja hayawezi kuheshimiwa hadi pale matakwa ya Serikali Kuu yatakapochukua nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kupeleka madaraka kwa wananchi kwa maboresho ya Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kuna udhaifu katika aina hii ya uwezeshaji kwani mara nyingi kinachotokea ni mategemeo kuwa serikali itawawezesha wananchi. Lakini Serikali, kama tulivyokwishakuona, haiko radhi kupoteza mamlaka yake kirahisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa uwezeshaji wa kweli utatokana na Mapinduzi ya Kidemokrasia (Nguvu ya Umma), uwezeshaji utaletwa na watu kwa ajili ya watu. Uwezeshaji hapa utaanzia kwa watu wenyewe kwa kuangalia watu wanataka nini na sio dola kuamua kwa niaba ya wananchi. Misaada toka kwenye taasisi na asasi za Serikali itasaidia pale tu ambapo jamii itakuwa tayari kwa misaada hiyo na tayari ina mipango yake

ya maendeleo. Kinyume na hapo ni kupoteza rasilimali nyingi bila ya kuwepo matunda.

Mheshimiwa Spika, kuonyesha kuwa ugatuaji wa madaraka umeshindwa ni mfano mdogo tu pale Sheria Ndogo zinazotungwa na Mabaraza ya Madiwani haziwezi kutumika katika Halmashauri zao hadi pale zitakapopata au kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Huu ni upungufu mkubwa na Kambi ya Upinzani inaona kuwa upungufu huo upo kwenye mnyororo unaoanzia juu kwa utendaji na watendaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuona upungufu huo unaoendelea kudhihirisha kuwa Serikali hii inashindwa kuielewa dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka na ndiyo sababu CHADEMA kwa kullona hilo tumeanza sasa kutekeleza mfumo huo kwa kuanzisha Tawala za Kanda au Majimbo ili tunapochukua nchi mwaka 2015 mfumo mzima uwe tayari umeshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Baada ya mfumo wa vyama vingi pamoja na mpango wa maboresho katika Halmashauri za Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Wilaya hawana kazi maalum ya kufanya zaidi ya kuomba mafuta ya magari kwa Wakurugenzi wa Halmashauri. Kazi nyingine zisizo rasmi ni kukisaidia Chama Tawala kuweka mikakati ya ushindi katika chaguzi mbalimbali. Mikakati yaweza kuwa ya ushindi wa kweli au ya hila.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine kwenye ngazi ya Wilaya yana watendaji wake na kwa hiyo kumfanya Mkuu wa Wilaya agombanie kazi na watendaji wengine. Mathalani, shughuli zote za maendeleo zinasimamiwa na Mkurugenzi na wataalam wake. Wakati Mkurugenzi na watu wake wanafanya shughuli hizi kwa utaaliam, upande wa siasa wa kazi zao unafanywa na Madiwani. Mpaka hapa Mkuu wa Wilaya anakuwa hana kazi.

Mheshimiwa Spika, shughuli za ulinzi na usalama zinasimamiwa vema na Afisa Usalama wa Taifa katika Wilaya (DSO) na Kamanda wa Polisi wa Wilaya (*OCD*). Hawa wana utaalam na maelekezo yaliyoandikwa kuhusu kazi yao. Wanapoungana na wenzao wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Uhamiaji, Magereza, Mgambo na vikosi vingine vidogo vya operesheni maalum, wanafanya kazi zao kwa ufanisi kuliko wakimwingiza Mkuu wa Wilaya ambaye mara nydingi hujikuta akituvu jisha siri ili kuwapendezesha wakubwa wake wasio katika mnyororo wa kiusalama.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ya Serikali Kuu, yasiyoangukia Halmashauri, yanafanya vizuri na Afisa Tawala wa Wilaya (*DAS*). Mambo hayo ni kama usajili wa vizazi na vifo, utatuzi wa migogoro, utoaji vibali vya muda maalum, ushiriki katika Tume ndogo za uchunguzi na uratibu wa safari za Maafisa Wateule wanapokuwa Wilayani.

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine ni kwamba Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Wilaya, lakini mipango yote inayopangwa katika Wilaya inapangwa na Baraza la Madiwani na Mkuu wa Wilaya sio mjumbe wa vikao hivyo, sasa huyu Mwenyekiti atakuwaje na tija katika nafasi yake ya Uenyekiti wa Kamati hiyo kama hawezo kutoa mchango wake katika vikao halali vinavyotoa mustakabali wa mazingira katika Wilaya?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majukumu haya yote tayari yana watu, Wakuu wa Wilaya wanajikuta hawana kazi zaidi ya kushinda wanazunguka na kujitambulisha kuwa wao ndio wawakilishi wa rais katika Wilaya. Nafasi hizi zimepitwa na wakati na ni lazima zifutwe kwani hazina tija kwa wananchi badala yake zinaiongezea Serikali matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inatoa mapendekezo yafuatayo kuhusiana na utawala katika ngazi Serikali za Mitaa

kama ambavyo iliyatoa kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Badala ya kuwa na Mikoa:-

- (1) Serikali za Majimbo ambayo yataongozwa na Gavana atakayechaguliwa moja kwa moja na wananchi katika Jimbo husika.
- (2) Miji, Manispaa na Jiji ndani ya Majimbo itaongozwa na Meya atakayechaguliwa moja kwa moja na wananchi katika Mji husika.
- (3) Maeneo yasiyokuwa Miji, Manispaa na Majiji yataunda Halmashauri za Wilaya zitakazoongozwa na Mwenyekiti atakayechaguliwa moja kwa moja na wananchi katika Halmashauri husika na Baraza la Madiwani watakaochaguliwa na wananchi.
- (4) Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji zitakuwa na mamlaka ya kuteua na kuajiri Watendaji Wakuu, Watendaji na Watumishi wote katika maeneo yao kwa kadri itakavyoonekana inafaa na mamlaka hizo.
- (5) Kila Jimbo litakuwa na Baraza la Kutunga Sheria la Jimbo (*Provincial Legislative Assembly*) litakalochaguliwa moja kwa moja na wananchi kwa utaratibu utakaowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge la Tanganyika.
- (6) Majimbo yatakuwa na mamlaka ya kutoza kodi za aina mbalimbali katika maeneo yao na vilevile yatakuwa na haki ya kupata sehemu ya kodi itakayotozwa na Serikali Kuu kutoka ndani ya eneo la mamlaka ya Jimbo kwa kiwango kisichopungua asilimia arobaini ya kodi yote itakayokusanya na Serikali Kuu katika Jimbo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi badala ya mamlaka zaidi kupelekwa kwa wananchi, kinachotokea huwa ni Serikali Kuu kutaka kuongeza udhibiti. Wakati huu ambapo Serikali

imejitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa uchumi, kinachotokea ni uwezeshaji wa aina fulani pale ambapo Serikali inaingia ubia au kuruhusu asasi za kiraia kujihusisha na maeneo kama utunzaji wa mazingira, ulinzi na usalama, mapambano dhidi ya rushwa, utoaji wa huduma za jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti ya utekelezaji ya TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Makadirio ya bajeti ya mwaka 2012/2013 katika ukusanyaji wa maduhuli na makusanyo katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 362,635,616,479.00 na taarifa ya karibuni inathibitisha kufikia makusanyo ya shilingi 117,806,757,658.00 sawa na asilimia 33 ya malengo yallyowekwa, hii ni uthibitisho wa wazi wa Serikali kutoweza kipaumbele katika mambo ya msingi ya kimaendeleo na kuendelea kujenga Taifa tegemezi kwa kutokuwa na mkazo katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kufanya Taifa liweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), inaitaka Serikali pamoja na kutoa ufanuzi wa kushindwa kufikia malengo pia inataka Serikali kutoa ufanuzi wa sababu za kushindwa na kuonesha mkakati wa kuweza kutekeleza kwa kipindi kulichobaki na kuwa na dira ya kutufikisha vema katika bajeti hii ya sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali hii kutoweza kipaumbele katika mambo ya msingi kwa Taifa, Ofisi ya Waziri Mkuu imeweza kufikisha asilimia 58 za matumizi ya kawaida kwa kutumia shilingi 96,622,804,335.00 ambazo ni fedha nyingi kuingizwa katika matumizi ya kulipana posho, matumizi mengineyo na mishahara, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inahoji nini kipaumbele cha Serikali kati ya maendeleo kwa wote na posho kwa walio na nyadhifa Serikalini?

Mheshimiwa Spika, fedha za mipango na maendeleo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa mwaka wa 2012/2013 ilikadiria kutolewa shilingi 22,276,872,000.00 na hadi kufikia Desemba 2012 fedha ambazo Wizara ilikuwa imezipata ni asilimia 11 tu na fedha zilizotumika kutoka asilimia 11 ni asilimia 32 katи ya shilingi 2,343,641,984.00 ambazo ni sawa na shilingi 742,206,531.00. Hali hii inathibitisha jinsi Serikali isivyoweka kipaumbele katika maendeleo kuanzia ngazi za juu hadi chini. Pamoja na Hazina kutoa kiasi kidogo cha fedha za maendeleo pia Wizara imeonekana wazi kutoweza kuzitumia kwa wakati, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali iliambie Bunge kweli kuna sababu yoyote ya Bunge kuitisha bajeti na baadaye bajeti hiyo ikashindwa kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tulishauri Serikali, kutokana na ukweli kwamba TAMISEMI ndiyo Wizara inayowafikia wananchi wengi na ndiyo Wizara ambayo matumizi mengi ya fedha za walipa kodi yanafanyika kienyeji na wananchi wanakuwa hawana utaalamu wa kufuatilia, hivyo tulionomba, nanukuu:-

*“Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaendelea kusisitiza matumizi ya asasi za kiraia kuismamia Serikali na kuiwajibisha kwa Jamii kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Uwajibikajikwa Jamii (Social Accountability Monitoring System- SAMs) na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (Public Expenditure Tracking System-PETS)”.*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mrejesho wa jinsi gani asasi za kiraia zitakavyofanya kazi kuismamia matumizi ya fedha za walipakodi kwenye ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya mwaka wa fedha 2012/2013, tulihoji kuhusu matumizi ya fedha za Rada, nanukuu:-

*"Katika Kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alijoitoa kuhusu matumizi ya fedha za Rada alisema, nanukuuu "...Serikali ya Uingereza na Serikali yetu zillijadiliana na kukubaliana kuwa ni vyema fedha hizi za wananchi wa Tanzania zikarejeshwa kupitia Serikali ya Tanzania. Serikali hizi mbili zilikubaliana kuwa fedha hizo zitumike kwenye Sekta ya Elimu. Mpango huo ulikuwa moja ya ushahidi muhimu uliotolewa Mahakamani kumshawishi Jaji kutoa uamuzi wa kuridhia makubaliano kati ya SFO na BAE ... kununua vitabu 4.4 milioni kwa ajili ya wanafunzi, vitabu 192,000 kwa ajili ya Walimu kufundishia, madawati 200,000, kujenga nyumba 1,196 za Walimu wa shule za msingi vijijiini, kujenga vyoo 200,000 kwenye shule za msingi".*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa TAMISEMI ndiyo yenyeye mamlaka ya usimamizi wa matumizi ya fedha hizo za rada kwa mujibu wa maelekezo hayo, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge:-

- (1) Kwa nini fedha hizo hazikutumika katika mwaka wa fedha uliopangiwa kutumika wakati matatizo na mahitaji ni makubwa?
- (2) Kwa kuwa mchanganuo wa fedha ulikwishaainishwa mbele ya Bunge kuwa fedha hizo pamoja na vitabu, zingejenga nyumba za Walimu wa Shule za Msingi Vijijiini 1,196 na vyoo 200,000 katika shule za msingi vijijiini. Serikali ilieleze Bunge, je, mradi huo upo au umefutwa? Kama upo, fedha hizo zitatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, hujuma ya Serikali dhidi ya wakulima. Serikali imekuwa na mipango na mikakati pamoja na uhamasishaji mkubwa katika kuhakikisha wakulima wanalima kwa kutumia zana bora na za kisasa katika kuzalisha. Katika mpango huo, wakulima waliitikia wito huo wa Serikali kwa kutafuta uwezeshaji kwa kadri walivyoona ikiwa ni pamoja na kukopa fedha na pembejeo kutoka asasi mbalimbali za fedha na pengine kulingana na uwezo binafsi wa mhusika.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi hasa wa mpunga walilima na wamevuna mpunga mwingi sana na sasa maghala yao hasa katika Mikoa ya Morogoro maeneo ya Malinyi, Ifakara na Mvomero pia Mkoa wa Mbeya na Kilimanjaro hasa Wilaya ya Same na kadhalika yamejaa mpunga. Kutokana na neema hiyo ya mavuno ambayo imeshuka kwa wakulima, lakini jambo la ajabu ni kwamba Serikali huku ikielewa hali halisi ya mavuno ya mpunga bado imetoe vibali kwa wafanyabiashara kuagiza mchele toka nje na mchele huo unaingizwa kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuwa hii ni hujuma kwa wakulima wa ndani na kilimo kwa ujumla kwani mchele unaotoka nje kwa punguzo la kodi unasababisha mkulima kulazimika kuuza mpunga wake kwa bei ambayo haiwezi kukidhi gharama za uzalishaji. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wakulima ni kigezo gani wanakitumia cha kutoa vibali vya uagizaji wa mchele wakati ikielewa imekuwa ikihamasisha wakulima kulima kwa lengo la kukidhi utoshelevu wa chakula na pia kuondoa umasikini kwa jamii za wakulima. Je, kuna haja ya wakulima kuendelea kulima wakati Serikali haina nia ya dhati ya kuwaondolea umaskini wakulima?

Mheshimiwa Spika, nchi zote Duniani ambazo zimeendelea, jambo la kwanza walihakikisha na wanaendelea kuhakikisha kuwa wakulima wao wanalindwa kutokana na nguvu za soko. Hivyo basi, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wakulima wanalindwa kwa kutoa fidia ya tofauti ya bei ili waweze kukidhi gharama za uzalishaji na kwa njia hiyo wakulima wataendelea na kilimo na pia kulipa madeni yao kutoka taasisi mbalimbali walizokopa.

Mheshimiwa Spika, ajira katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Bunge lilipitisha sheria inayoitwa "*The Local Government Service Act, 1982*" na sheria hii iliunda "Tume ya Uajiri katika Serikali za Mitaa" kwa lengo kuu la kuwa ndicho kingekuwa chombo kikuu chenye mamlaka ya kutoa ajira katika ngazi hiyo ya Serikali. Aidha, kwa sasa kuna chombo kingine kinaitwa "Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi

wa Umma" ambacho kinatoa ajira hadi za watendaji katika ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania, hii sheria iliyotungwa na Bunge ya "*The Local Government Service Act, 1982*" imefutwa au majukumu yake yameingizwa kwenye Sheria ya *Civil Service Act, 1989*? Kama bado ipo, utendaji kazi wa sheria hiyo ukoje?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo hayo kutokana na ukweli kwamba katika kufanya usimamizi wa fedha za walipa kodi vyombo vyta Serikali vinavyotakiwa kufanya kazi hiyo ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (*Internal Auditor General*) na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (*Controller and Auditor General*). Katika hawa wote, mmoja hana nguvu kisheria ya kuhamisha watendaji wanaofanyakazi kwa niaba yake, naye ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwani katika Halmashauri mamlaka ya ajira kwa Wakaguzi wa Ndani sio ofisi yake bali wako Ofisi ya TAMISEMI chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hiyo ni kwamba hata hao Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wanakuwa ni sehemu ya utawala badala ya kuwa washauri. Jambo hili linatengeneza mazingira ya kifisadi yanayofanya katika ngazi hiyo kutokana na mahusiano yanayojengwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani anakosa mamlaka ya kufanya uhamisho ila kwa ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzifanyia marekebisho sheria husika ili Mkaguzi Mkuu wa Ndani awe na mamlaka ya kuwashauri Wakaguzi wa Ndani kwa kadri atakavyoona inafaa kama ilivyo kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam (*DART*). Mradi wa mabasi yaendayo kasi kwa Jiji la Dar es Salaam, kwa ratiba iliyopo ni kwamba unatarajia kukamilika ifikapo mwaka 2015, hii ni kukamilika kwa

miundombinu tu. Mradi huo ambao hadi kukamilika utakuwa umetumia jumla ya shilingi bilioni 460, baada ya Benki ya Dunia kuongeza shilingi bilioni 160 kwa mujibu wa Tanzania's Daily News reported Thursday (Januaryy 17<sup>th</sup>). Hoja ya msingi ni, je, Watanzania wanaweza kuhakikishiwa juu ya utayari wa mabasi hayo pindi miundombinu hiyo itakapokuwa tayari? Hii ni muhimu ili kuepuka kufanya uwekezaji usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti uliofanywa na *TIC* kuhusu "*traffic jams are eating up to 20 per cent of annual profits of most businesses*" na kuandikwa kwenye gazeti la *This day*, inaonyesha ukubwa wa tatizo, kwa siku nchi inapata hasara ya takribani shilingi bilioni nne (4), kwa mwaka inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi trilioni 1.4. Hizi ni fedha nyingi sana kupotea kwa nchi maskini kama yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mradi huo, lengo lilikuwa ni kupunguza msongamano wa magari kwa barabara zetu, sambamba na kupunguza matumizi ya mafuta ya magari yanayosimama kwa muda mrefu barabarani. Japokuwa hadi sasa mradi bado unaendelea lakini tulitarajia kuwepo kwa sehemu maalum za maegesho ya magari ya wananchi katika sehemu maalum zilizotengwa kwa kazi hiyo (*Park and drive*), kwa lengo la wananchi waje na magari yao hadi vituo vyta magari yaendayo kasi na wakirudi kutoka katika shughuli zao wachukue magari yao na kurudi majumbani. Kama maeneo hayo hayakutengwa msongamano wa magari utaishaje?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa ufanuzi kuhusiana na suala hilo ambalo kwa kiasi kikubwa ndilo litakalopunguza msongamano wa magari barabarani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona tumetumia muda mwingu kuwasikiliza Wasemaji Wakuu katika hotuba zao hizi. Kwa hiyo mjadala tutaanza jioni kuanzia saa kumi na moja mpaka saa moja kasorobo, tutakuwa na dakika 165, ukigawa kwa kumi, ina maana tutakuwa na wasemaji kumi na sita. Kama mkichangia vizuri wanaweza wakawa 17. Kwa hiyo, nina orodha ya wachangiaji ambao ningependa wajandae. Kwa kuanza, tutaanza na Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mwigulu L. Madelu, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa John Cheyo. Hawa ndiyo wataanza halafu tutaona tutakavyoendelea.

Kwa kuwa tumesikiliza hotuba nyingi sana na kwa muda uliobakia, naomba tupate muda wa kupumzika. Hivyo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge lilitishwa  
Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana niliwataja ambao wataanza kuchangia, sio kwamba wataanza kuchangia kama nilivyowataja, nitaanza na Mheshimiwa Jitu Soni na atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nichangie katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwanza kwa kuishauri Serikali iboreshe masuala ya Utawala Bora kwa kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa Wenyeviti wetu wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji na Halmashauri za Serikali za Vijiji

pamoja na Madiwani ili kuongeza ufanisi katika kazi kwa sababu wao ndiyo wanasmamia kwa sehemu kubwa katika ngazi hizo na kuangalia maslahi bora kwa ajili ya Kada zote hizo. Pia nilikuwa ninaishauri TAMISEMI ikiwa chini ya Ofisi ya Wazirii Mkuu ilete mapema Muswada wa kuajiri kada za chini ili watumishi tunaotaka kuwaajiri katika Halmashauri waweze kuajiriwa kwa mfano Watendaji wa Vijiji na Madereva na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kuwa mfumo wa uboreshaji wa maslahi wa watumishi wanaojiendeleza kimasomo ili wakirudi waweze kupanda madaraja, vyeo pamoja na mishahara yao kama ilivyo kwa upande wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie namna ya kuboresha ule mfumo mzuri uliokuwapo wa *customer charter*, namna ya kutoa huduma bora kwa wateja ambao ni wananchi wote na utoaji wa taarifa mbalimbali kwa Serikali kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iangalie mfumo bora wa kuunganisha Wizara mbalimbali kwa mfano wakati wanapoibua miradi na wakati wa kutekeleza miradi mfano ukitaka kujenga bwawa, unakuta ni Wizara ya Maji kwa ajili ya maji ya binadamu lakini hata mifugo inataka na upande wa kilimo na umwagiliaji. Sasa Wizara zote zingekuwa zinaunganishwa wakati wa uibuaji mradi na ule mradi Wizara zote zichangie pesa za maendeleo kidogokidogo, miradi mingi ingeweza kutekelezwa, pamoja na Wizara zingine mfano Nishati na Madini ili wakati wa kubuni na kuandaa mpango, Wizara zote zikifanya kwa pamoja ile miradi itakuwa na mafanikio na pesa itakayokuwa inatumika kwa kila Wizara ni ndogo lakini ufanisi utakuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia katika Sekta ya Kilimo Kwanza, Serikali iangalie namna ya kuboresha mambo mbalimbali mfano 75% ya Watanzania ni wakulima, wafugaji na kwangu Babati 96% ni wafugaji na wakulima. Sasa ili kuboresha ufanisi katika sekta hiyo kuna mambo mbalimbali tulikuwa

tunapendekeza. Moja, Wizara ya Ardhi iwe moja katika zile *Ministries* za Kilimo Kwanza kwa sasa hivi haipo na ardhi ni moja katika zile nguzo za Kilimo Kwanza. Kwa hiyo, Wizara hiyo ijumuishwe katika zile Wizara na kuwa mstari wa mbele katika mambo ya kilimo. Pia Serikali iangalie namna ya kuajiri wataalamu wa kilimo wapataao 15,000 wanaohitajika, wa Kilimo na Mifugo ili kuboresha ugani wa kilimo lakini muhimu hapo pia ni Serikali iangalie namna ya kuweka vituo vya kupimia udongo na mambo ya hali ya hewa katika kila Mkoa ili wakulima waweze kupata huduma kwa karibu na kuondoa hili lalamiko la kila siku kuwa mbolea hii haifai au mbolea hii siyo nzuri katika ardhi yetu. Ni bora Serikali iingie gharama kidogo kwa kuweka vituo katika kila Mkoa kwa sababu wataalam wapo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali iangalie mfumo mzima wa tozo ya kodi. Ushuru na tozo mbalimbali zinatozwa kwa wakulima na wafugaji ni nyingi mno na ni mzigo mkubwa. Serikali iangalie mfumo mzima huo kwa sababu tozo yoyote inayotozwa inasema ni wafanyabiashara ndiyo wanaotakiwa kulipa lakini mwisho wa siku ni mkulima ndiye anayebeba mzigo huo. Kuna kodi ambazo tulipitisha hapa zifutwe mfano katika tela za trekta, kodi zile za vipuri vya trekta, matela na matairi bado mpaka leo hii pamoja na kupitisha Serikali inaendelea kutoza, kwa hiyo, tozo hizo zote ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukitaka kuingiza mbolea aina mpya ni dola 10,000/= zinachajjiwa ili aina hiyo ya mbolea iweze kuingia sokoni. Sasa kwa mtu ambaye amezoea hizi busta mbalimbali, leo hii wameacha kuleta na inakuwa ni kero. Kwa hiyo, hizi *regulatory bodies*, zile tozo zao zote ziangaliwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ili kuboresha mapato ya Halmashauri zetu, ningeshauri Serikali iangalie namna ya kupata Mtaalam Mwelekezi yaani *consultant* katika kila Halmashauri ili tuweze kuangalia fursa zilizopo katika kila Halmashauri na namna ya kukusanya hayo mapato mbalimbali ili Halmashauri zetu ziweze kuongeza mapato bila kuwa tegemezi katika Serikali Kuu. Pia wale watashauri

namna mbalimbali ya kuondoa kero na namna ya kuangalia fursa zingine ili Halmashauri zetu ziwe na mapato mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali safari hii tunaomba itoe tamko ili Halmashauri zetu ziweze kukusanya zile ada za leseni ambazo kwa miaka miwili sasa tunasubiri tamko hilo ili tuweze kuogeza mapato, katika bajeti miaka hii mitano hatujaweza kukusanya, tunaomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iangalie Sheria ya Manunuzi ambayo imekuwa ni tatizo kubwa na ndiyo chanzo kikubwa cha hasara kwa Serikali yetu na katika Halmashauri zetu. Mimi ningeshauri kuwa hicho kingeleta kipaumbele chetu cha kwanza ili gharama za manunuzi na zile *tendering processes* ziweze kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninaomba tuangalie sekta mbalimbali kwa mfano Vyuo vya Elimu, vyote viko chini ya Wizara ya Elimu. Mimi ningeshauri kuwa mfumo ule ubadilishwe ili vyuo ambavyo vinahusika na Wizara husika viweze pia kuhudumiwa na Wizara hizo. Kwa mfano, Wizara ya Elimu inafanya kazi nzuri, vyuo vyote inaviangalia kama Baba na Mama, ni watoto wake wanawahudumia kwa usawa, lakini Chuo kama *Sokoine University* ambacho ni chuo pekee cha kilimo kina matatizo mengi hata pesa za maendeleo hazifiki kwa kiwango kinachohitajika. Mfano, Idara ya *Mechanization* pale *Sokoine University* haina vifaa vyote kwa mfano matrekti, *powertillers* na vifaa vingine vya umwagiliaji. Sasa wakitegemea Wizara ya Elimu kuwapa vitu vyote hivyo haitawezekana, Wizara zote ambazo zinahusika pale ziweze kuchangia hivyo hivyo katika vyuo vyote vya elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningeshauri katika sekta ya afya katika maeneo ambako kuna hospitali za Wilaya au tunategemea kujenga hospitali za Wilaya, ni muhimu kwanza tuboreshe vituo vya afya katika kila Tarafa kwa kuweka maabara za kisasa kwa sababu vituo vya afya vinaweza kulaza wagonjwa. Kwa hiyo, maabara ya kisasa ikiwepo

huduma inaweza kupatikana kwa karibu na baadaye ndiyo tufikirie kujenga hizi hospitali za Wilaya ambazo inakuwa ni gharama kubwa na hazikamiliki kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishauri Serikali katika mambo mbalimbali, ikipanga Wizara zote au Idara mbalimbali ziweze kushirikiana katika mipango mingi kwa mfano maji, bajeti inatolewa, kisima kinajengwa lakini mpaka Wizara nyiningine ya Nishati ije kuweka umeme pale na kusambaza inachukua mwaka mmoja au bajeti zingine mbili, kwa hiyo, mradhi unakuwa umechelewa. Wakati tunapanga mipango yetu, Wizara zote husika zingekuwa zimejumuishwa na wakae pamoja kwenye *planning board* ili fedha zote zikitolewa zitolewe kwa pamoja na hata kama miradi ikiwa ni michache lakini itakuwa ni miradi ambayo inakamilika kwa muda mfupi na ufanisi utakuwa umepatikana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwa tunaendelea kuboresha Daftari la Wapigakura na inasemekana kuwa sasa hivi kutakuwa na utaalamu wa kutumia digitali na mambo ya *biometrics*. Nashukuru sana kwa sababu kupiga kura kwa huu mtandao wa kisasa kwa kutumia mboni ya macho pamoja na *finger prints*, itaondoa tatizo la watu kuandikishwa na wale ambao hawajajiandikisha waendelee kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia lakini kama unavyokumbuka asubuhi ulitamka kuwa mimi nilikuwa ni mchangiaji wa pili lakini Mungu ndiyo muweza wa yote na sasa nimekuwa tena wa pili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri imekamilika na ninaweza kusema kuwa imetimiza yale yote ambayo yametakikana.

Mheshimiwa Spika, lakini nirejee tu kusema kuwa ni vyema tunapokula viapo ndani ya Bunge au viapo vya aina nyingine yoyote kuvizingatia. Katika kipindi chetu cha asubuhi, kuna baadhi ya wachangiaji wenzetu walitoa hoja ambazo mimi binafsi zilinistajabisha sana. Tulikula kiapo cha kuitetea na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini sisi ndio tumekuwa wa kwanza kuichambua, kuikana na kuisigina Katiba hiyohiyo ambayo tumekula kiapo juu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano mmoja katika hili, Ibara ya 61(1) ya Katiba inatoa Mamlaka ya Kikatiba kuwepo kwa Wakuu wa Mikoa, kuwepo kwa Wakuu wa Wilaya. Sasa leo hii tumeanza kusema kuwa watu hawa hatuwahitaji na sasa tuko katika Mchakato wa Katiba Mpya kwa nini haya hatuendi kuyasema ili Katiba inayofuata ambayo tutakuja kula kiapo chake hapa kama tutarejea tena Bungeni tukaifuata na kuona kuwa hawa wameondoka Kikatiba? Kufanya hivi ni kuwapotosha wananchi na tunawapeleka katika njia ambazo hazifai kwa maana hii ni mihimili iliyopo kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu ameainisha na amezungumzia suala la mfumuko wa bei ambao ulifika zaidi ya 19.5% lakini hivi sasa umeshuka na kufikia 9.8%, inawezekana kwa takwimu zilizoandikwa lakini hili siyo jambo halisia. Bei ya chakula bado iko juu sana na hali ya Watanzania kuhusu chakula ni mbaya. Nimeleta hoja hapa na ninashukuru kuwa umeipokea na umeipitisha lakini tunachosubiri ni muda, lazima sasa Serikali iwe na mkakati unaofaa kuweza kudhibiti bei za vyakula vinginevyo tunawapeleka kubaya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati hili suala la chakula tunalizungumzia, kuna chombo kingine tena kimeongeza bei za nauli za vyombo vya usafiri hasa mabasi na daladala. Kisingizio kikubwa wanasema kwamba gharama za uendeshaji zimeongezeka, gharama za mafuta zimepanda lakini takwimu tulizokuwa nazo sisi Bungeni hapa bei ya mafuta imekwenda kwa wastani huo kwa kipindi cha zaidi

ya miaka minne sasa. Sasa hili ongezeko linalozungumziwa limetokana na kitu gani? Haohao *SUMATRA* ambao wamezungumzia kuwalinda na kuwatetea wasafirishaji, hawajazingatia kuwa wasafirishaji hao bado hawajaboresha miundombinu mizuri katika vyombo vyao nya usafiri ili kuboresha huduma ambayo wanaitoa na kwa pesa ambayo wanalipwa na wananchi. Hili inabidi liangaliwe na litizamwe upya kwa maana hatia hao wasafirishaji wadogowadogo ambao wanamiliki hivi vyombo wataingia kwenye shida kwa kuwa *SUMATRA* haohao wametoa tangazo la kutaka wote ambao wanamiliki mabasi wafanye shughuli hizo katika kampuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia masuala ya uboreshaji wa huduma lakini huduma hizi hazitoweza kuboreka kama sekta muhimu ikiwemo Polisi, Walimu, Wanajeshi na watumishi wa kada ya afya hawajaboreshewa mazingira na malipo au maslahi yao ambayo wanastahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nizungumzie na hili Mheshimiwa Waziri Mkuu usimamie ipasavyo, mwaka jana tulipitisha Bungeni hapa Azimio la Kupandisha Bei ya Mafuta ya Taa ili iweze kudhibiti uchakachuaaji wa mafuta. Hili limefanyika lakini fedha zile hazikwenda kama ilivyotakiwa kwa maana kuwa hazijapelekwa *REA*. Tunayo miradi ya umeme kwenda katika maeneo ya viji viyetu lakini pesa hakuna. Mpaka sasa kuna upungufu wa zaidi shilingi bilioni 881, hizi pesa zitatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nilitaka nizungumzie suala la mgawanyo wa Mamlaka mpya Kiwilaya na Kimkoa. Wilaya ya Kilwa tumekuwa tukizungumza miaka yote kuwa tunahitaji tugawanywe kwa sababu Wilaya yetu ni kubwa kuliko Mikoa mingi tu mipya ambayo imetangazwa. Kwa hiyo, tunataka tupewe tamko ni sababu zippi ambazo zinapelekea wengine kupewa nafasi ya Mamlaka mpya za Wilaya na Mikoa na Kilwa ikawa imetengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fursa za gesi zimeonekana na zipo lakini katika hotuba ya Waziri Mkuu suaona sehemu ambapo amezungumzia ujenzi wa uzalishaji umeme katika eneo la Mtwara na Kilwa na hii miradi ipo. Sasa tunataka kauli ya Serikali kutuainishia kuwa kweli hii miradi itafanyiwa kazi na itakuwepo au lah imekuja kimaandishi tu kwa sababu kwenye hotuba yako Waziri Mkuu hili halijawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara, tunahitaji pesa maalum kwa ajili ya barabara kutoka Kipatimu hadi Tandawale, Kipatimu kwenda hadi Mihangalaya. Vilevile barabara zetu ziboreshw kutoka njia nne kwenda kipatimu lakini vilevile Nangurukulu hadi Liwale kuititia Njinjo na Mitolo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nafasi ya muda ninayo nitazungumzia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu suala la korosho ambalo limeleta utata na linaleta utata, hivyo tunakuomba Waziri Mkuu na Waziri husika tukae pamoja na Wabunge ili tuweze kutoa mbinu mbadala zitakazoweza kutatua matatizo ambayo wananchi wetu wanayakabili kama ulivyotukubalia kwenye suala la zao la ufuta.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Eng. Mfutakamba, Mheshimiwa Paul Lwanji halafu Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandae.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa kunipa fursa hii...

**SPIKA:** Naomba uhame inaonekana kama unasema mwenyewe tu.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 18, suala la uchumi.

Mheshimiwa Spika, wastani wa pato la Taifa imeelezwa kuwa ni 995, 298 na mfumuko wa bei sasa hivi ni takribani digiti moja, asilimia 9.8% lakini bado wananchi wa Igalula hali ni zulfali hali. Hata kushuka kwa bei ya petroli bado bei za nauli ziko palepale na zinaendelea kupanda na bei ya kusafirisha mazao na kuleta pembejeo bado ni kizungumkuti, bei ziko juu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Deni la Taifa; hili sidhani kama ni tatizo ukiliangalia katika misingi ya kiuchumi. Pato la Taifa katika ulinganifu, tunaangalia *debt GDP ratio*, nchi yetu ipo katika hali nzuri. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa asiwe na tatizo asilimia ya *debt equity ratio* Japan ni asilimia 192, Marekani ni 92%, Uganda asilimia 48, Kenya 70%, sisi Tanzania bado ni asilimia 38, kwa hiyo, tupo pazuri tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la Katiba, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ngazi ya Wilaya, kwa kweli sasa hivi wananchi wanapata msisimko mkubwa na wengi wanaojitokeza zaidi ya asilimia 78 ni wa Chama Tawala, kwa hiyo ndio maana wanakuwa wengi kwenye hizi Kamati. Kwa hiyo, hilo lisiwe tatizo na ndugu zangu wasijitoe kwa kweli, itakuwa siyo ukomavu wa kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la uchukuzi, ukurasa wa 53 na 54, nitoe tu pongezi kwa ujenzi wa reli ya Dar es Salaam - Isaka-Keza, Keza - Kigali na Keza - Msongati. Katika sherehe za CCM Taifa miaka 36 pale Kigoma, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alikubaliana na wazo la kujenga reli ya kutoka Msongati mpaka Uvinza, lakini mimi nimefarijika, nimepata taarifa kwamba reli zote hizi mbili zitajengwa na hii ya Uvinza pia itajengwa, kwa hiyo maendeleo yatakuwa makubwa katika utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 55, kuhusu Bandari, gati Na. 1 mpaka Na. 7, zimeongelewa vizuri, ninaamini maelezo ya kina yatatolewa kwa ujenzi wa gati Na. 13 na 14

kwa bandari ya Dar es Salaam ili kina cha lango la Bandari ya Dar es Salaam kiongezwe, meli za Jeneresheni ya Nne ambazo zinaweza kubeba kontena TU10,000 mpaka 15,000 ziweze kuja hapa Dar es Salaam na pia tuweze kuzishinda bandari za Beira, Mombasa, Lamu na pia ujenzi wa bandari ya Bagamoyo upo katika mpango wa *TPA*. Kwa hiyo, naamini kabisa sisi tutakuwa lango limefunguka la kiuchumi kwa nchi za jirani ambazo hazina bandari za Malawi, Rwanda, Burundi, DRC pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la *flyovers*, wenzetu kule Kampala wanajenga *flyovers* tano, Kenya wanajenga sasa hivi *flyover* saba na kampuni inayojenga ni CCC ile ile na *World Bank* ilitoa *no objection*, sasa na sisi tuwe tunajitathmini wakati tukisema huyu tusiweke kwa sababu ameonekana ni kampuni inayotoa rushwa, hiyo tuangalie wenzetu wanasonga mbele huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo na ufugaji endelevu, Ibara ya 17(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia uhuru wa mtu kwenda atakako. Ni kweli katika Mikoa ndugu zetu wafugaji wanaweza kwenda maeneo yoyote wanayotaka, lakini iko Sheria ya mwaka 2004 ya Hifadhi ya Hazingira. Rai yangu ni lazima tuweke utaratibu wa kuanzisha Wakala wa Miundombinu ya Ufugaji. Tatizo liliopo, hawa wafugaji wanatoka kwenye maeneo ya ufugaji nyasi hazitoshi, mabwawa hayatoshi, majosho hayatoshi, matokeo yake wanakwenda sehemu mbalimbali lakini kama Serikali itatenga pesa za kutosha yatapatikana mazao ya kutosha na wafugaji watakaa kwenye maeneo yao yaleyale, badala ya kuanza kutangatanga kwenye Mikoa mengine halafu yanakuja matatizo makubwa na wao wanajiona kama ni wananchi ambao ni wakimbizi katika nchi yao wenyewe, lakini tukiweka mpango mzuri na mkakati mzuri wa mifugo, itaongeza sana pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la migodi; migodi inaweza pia ikatoa fursa nzuri kwa mpango wa *cooperative social responsibility* ambapo maeneo haya yenye wafugaji wakaelekezwa kufuga ufugaji bora kwenye maeneo ambayo

yanazunguka migodi ili kupata maziwa ya kutosha, nyama ya kutosha pamoja na ufugaji wa kuku hata wa kienyeji, kupata mayai pamoja na matunda na mbogamboga hali kadhalika kwenye maeneo hayo, mazingira yatalindwa, vyanzo vya maji vitalindwa na pia wafugaji watapata fursa nzuri kama wakipewa mafunzo katika *National Insemination Centre (NIC)* ambayo ipo Arusha na maeneo mengine ili tuweze kufuga ufugaji wa kisasa na wa kisayansi. Hakuna sababu ya kuwa na mifugo, uwe na ng'ombe 3000 hadi 4000 kwa sababu ya *status au symbol*, wakati huu maeneo ya ufugaji na malisho hayatoshi. Kwa hiyo tuwape elimu wafugaji wetu waweze k -diversify katika uchumi wao. Baadhi ya ng'ombe wanaweza kuuza wakajenga *guest houses*, wanaweza kujenga shule, wanaweza kujenga hospitali na pia wakafuga mifugo michache lakini ambayo itakuwa na tija kubwa kwa Taifa letu pamoja na vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora; michango mingi inahitajika katika Kata na Vijiji vyetu katika kusukuma maendeleo, lakini tatizo kubwa lililopo wananchi hawasomewi mapato na matumizi. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri Mkuu atoe maelekezo kwa Watendaji wetu wa Vijiji, Watendaji wa Kata, wananchi wanapochanga sheria ile inavyoeleza, kila robo tatu ya mwaka wananchi wasomewe mapato na matumizi, wataweza kusukuma maendeleo yao na wataona wao ni sehemu ya yale maendeleo na kwamba ile michango inatumika kwa tija na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, niokoe muda, niachie hapo kabla ya kunipigia kengele, naunga mkono na nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Paul Lwanji atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, naunga hoja mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sikubaliani na baadhi ya watu wanaosema kwamba Serikali haijafanya kitu,

sikubaliani nao kabisa. Ushahidi ni jana wakati Waziri Mkuu alipotoa hotuba yake, imesheheni mambo mengi yanayoonesha ni nini Serikali imefanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya wengine hatusomi, tunawaza mambo mengine lakini hatuendi kwa kina kujuu mambo haya. Mara nyingine huwa hata hatuoni maendeleo yenyewe huko tunakopita, kila eneo kuna shughuli inafanyika sasa hivi. Kila eneo, ukienda Mijini, miji inatakata sasa hivi kwa ujenzi wa barabara kila mahali. Mimi kule porini hata umeme kila mahali unapita na hata Julai sasa hivi wataanza kusambaza umeme kutoka Mitundu kwenye Mwamagembé, haya ni mafanikio makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tungeomba wenzetu mtupe nafasi ya kutenda sisi ndiyo tumeshika hatamu na ni muda wetu kwa hiyo mtuache tufanye kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tutashukuru sana, mtupe nafasi kipindi kama chenu kitakuja kama kweli kitakuwepo maana yake leo tumeshuhudia njozi hapa, zinatajwa njozi kwamba ikifika mwaka 2015 tutashika hatamu sasa hiyo hatujui, lakini sisi tunachoja kwamba tunahudumia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tunalo tatizo la udini, lakini mimi nadhani Serikali ingejaribu kuangalia usajili wa madhehebu haya ukoje? Maana tunaona Madhehenu kila mahali mara nyingine huwezi kutambua kama ni Dhehebu hasa la dini au ni NGO hata huwezi ukaelewa. Hapa Mjini kuna Askofu mmoja anapitapita hapo anahimiza mambo ya ajabu sana na anagawa *leaflets* na hata kingine ninacho hapa, anahimiza watu kunywa pombe, anahimiza watu wasitumie kondomu, ni mambo ya ajabu sana.

**MBUNGE FULANI:** Kuoa ma-housegirl!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, lakini anaachwa yupo mitaani anapita kila mahali na anapenda sana kupita kwenye ma-grocery na nini na kuwabariki wanaokunywa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa haya ni mambo ya ajabu na yupo Mjini hapa, amevaa ile *purple* na kola kabisa ya Kiaskofu na msalaba mzito, yupo pale na kitabu cha Biblia mkononi. Sasa ana-quote vile vifungu anavibadili kwa mtazamo wake.

Mheshimiwa Spika, huyu mtu anaachiwa yupo tu Mjini anapita kila mahali. Anasema kwake mkifika Jumapili kwanza ni viroba asubuhi, ndio unaingia ndani, kweli tunaacha tu haya mambo yanaendelea, hii ni *laxity* ya wapi hatujawahi kuona! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtu mzima nimeona Serikali kuanzia ya Mwalimu Nyerere mpaka leo sijawahi kuona *laxity* ya namna hii kwa upande wa watendaji, kwa sababu huyo mtu angepaswa aulizwe kwanza dhehebu lake limesajiliwa, lakini yupo! Kiroba na yeye anasema anaweka safari mbili madhabahuni, halafu shilingi elfu mbili sadaka ni lazima, kwa hiyo ina maana kwamba unahudumia hicho kinywaji wewe mwenyewe. Ninaomba sana usajili uangaliwe upya ili tuweze kupata madhehebu bora. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kama nilivyosema, lakini ninaona katika eneo la makusanyo ya mapato na pia fedha za kigeni. Tunaambiwa kwamba wafadhili wanachelewa kuleta au mara nyingine siku hizi hawaleti kabisa, lakini sababu kubwa unayoambiwa wanasema kwamba watayarishaji wa ripoti, hizi taarifa kuonesha miradi inatekelezwaje hazifiki kwa wakati. Ni nani wa kulaumiwa hapa, ni wafadhili au ni sisi wenyewe? Naomba Serikali iangalie hilo eneo ili taarifa zitolewe mapema ili wafadhili waweze kutoa hela.

Mheshimiwa Spika, nina migogoro katika eneo langu kuhusu mipaka ya Wilaya. Hili tatizo ni la muda mrefu na mgogoro huu ofisi ya Waziri Mkuu inaujua wa Matagata, Mwamatiga na Chaya, wajaribu kuangalia. Mkoa wa Tabora una kilomita za mraba 75,000 na Mkoa wa Singida una kilomita za mraba 49,000, lakini naona wenzetu wanataka kutumega zaidi, hata sielewi ni sababu ipi chokochoko inatokea. Ningombaa sana Serikali itumie utaratibu tu wa zile

GN ya mwaka 1961 lakini hizi GN zinazotokea pemberi kama Rais hakuamua kugawa eneo basi hatuoni sababu kwa nini tuwe na chokochoko hiyo. Tungeomba wenzetu watusaidie ili watu wetu waweze kufanya kazi na waweze kutulia.

Mheshimiwa Spika, tuliahidiwa bandari ya nchi kavu mpakani mwa Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Ikungi, mahali panapoitwa Iwelewele, lakini nashangaa bandari ya nchi kavu sasa hivi naanza kusikia inajengwa Mkuranga sijui wapi, otherwise mimi hiyo *meaning* ya bandari ya nchi kavu nashindwa kuielewa maana sasa kama ni Mkuranga ni baharini pale, kwa hiyo ningeomba hii ahadi iangaliwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba ahadi ya Rais ya barabara ya Itigi, Rungwa mpaka Makongorosi kwenda Mbeya itimizwe tafadhalli! Imekuwa sasa kero, ni muda mrefu. Watu nyumba zimepigwa X muda mrefu sana mpaka sasa hivi haioneshi dalili yoyote, nadhani itabidi watueleze vizuri kwenye sekta inayohusika kama wametenga fedha kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba leo Serikali inieleze kwa takwimu umaskini wa Mkoa wa Singida hasa uko wapi? Wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifika Singida tarehe 3 April wakati wa mizinga ya nyuki, ulishangaa ukasema hizi takwimu ni takwimu gani, maana kila unapokwenda unaona maendeleo, sasa Mkoa wa Singida kuwa wa mwisho kwa kweli ni kutunyanyapaa, kweli kabisa na mimi sikubali. Hili suala aliletwa Mtakwimu pale Mkoani ajaribu kutathmini kuona takwimu za Mkoa huo, mapato yake na nini lakini sijawahi kuona hiyo taarifa, nadhani Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mamlaka sahihi ya kuweza kutueleza *status* hasa ya Mkoa wa Singida iko wapi maana tunakerwa na zinapokuja taarifa zinaweka Mkoa wa Singida ndiyo wa mwisho. Hata ukiniangalia kweli mimi... (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana tutendeane haki. Takwimu hizi za Serikali hazikukaa sawasawa katika maeneo mengi. Maendeleo makubwa yanafanyaika Mkoa wa Singida

chini ya Mheshimiwa Kone yupo hapa, watoto wetu hawana kwashakoo tunakunywa maziwa, sasa tunywe nini kama siyo maziwa na maziwa ni lishe bora! Ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu itueleze vizuri juu ya suala hili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, sasa nimwite Mheshimiwa Lucy Owenya atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu Serikali itachukua ushauri na maelezo ya Kambi ya Upinzani yaliyoletwa leo asubuhi, yaliyosheheni tafiti nzuri kwa mustakabali wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na elimu ya shule za msingi. Elimu bora ni ile yenye msingi mzuri, kama unataka nyumba imara lazima msingi uwe imara pia lakini elimu yetu ya shule za msingi siyo nzuri. Kwa mfano, shule nyingi za Serikali hazina shule za awali, shule nyingi zile za chekechea zinaendeshwa na taasisi za dini au watu binafsi. Hii inapelekea wale Walimu wa shule za Msingi wanapoteza muda mwingi sana kuanza kufundisha watoto kuandika, kuhesabu na kusoma. Unakuta shule nyingine hazina Walimu wa kutosha, mwalimu mmoja anafundisha darasa la kwanza mpaka la saba, sasa mwisho wa siku watoto wanafeli, tunabaki kulaumiana wakati sababu tunazijua.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kwamba mipango siyo mizuri. Wanafunzi wengi wa shule za *primary* pamoja na kukienzi Kiswahili na kukubali Kiswahili ni lugha ya Taifa na lazima tukifuate lakini tukumbuke kwamba wanafunzi tunawafundisha Kiswahili kuanzia darasa la chekechea mpaka darasa la saba, lakini wale waliopo shule za *private* wanafundishwa Kiingereza tangu chekechea, *standard one* mpaka Chuo Kikuu, sasa wakifika sekondari ndiyo maana unakuta watoto waliosoma katika shule za msingi za umma hawafanyi vizuri, wanafeli na mwisho wake wanafanya

vibaya unakuta hawajui kusoma wala kuandika. Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuweza kuwasaidia Walimu waliopo katika *Primary School* au wabadiilishe mfumo wahakikishe kama ni kufundisha Kiswahili basi kusiwe na *contradiction* kwamba *privatewanajua* wengine hawajui, kama ni Kiswahili watengeneze vitabu wafundishe Kiswahili tangu shule za awali mpaka Chuo Kikuu, kama ni Kiingereza basi kifundishwe Kiingereza tangu shule ya awali mpaka Chuo Kikuu hii itatusaidia wote lakini tukisema kwamba tunaenzi Kiswahili wengine Kiingereza si sawa. Tukumbuke kwamba tunaenda kwenye *competition* ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu kama Kenya wanafundishwa Kiswahili kama somo lakini Kiingereza wanakifanya darasani kwa masomo yote na tukizingatia kwamba hata mtoto akienda kwenye *Interview* sasa hivi hapa Tanzania hawafanyiwi *interview* kwa Kiswahili, hata barua za kuomba kazi ni za Kiingereza, wakienda kwenye *interview* ni kwa Kiingereza, yule anayejua Kiingereza ndiye anayechukuliwa hata kama hana akili ili mradi ameweza kujieleza kwa Kiingereza mara nyingi ndiyo wanaochukuliwa. Wanaacha wale wanafunzi ambao unakuta wanaweza kweli kufanya ile kazi kwa kuandika lakini unakuta hawawezi kujieleza kwa sababu hawa-*practice* kile Kiingereza kwa kuongea wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuangalia ni jinsi gani ya kubadilisha mitaala hii la sivyo wale walionacho ndiyo watazidi kuwa nacho. Kwa mfano, shule za msingi kuna upungufu wa Walimu 57,000 hii inatokana na takwimu za Hakielimu, huu ni upungufu mkubwa sana, Walimu hawa hawawezi kufanya kazi kwa furaha, hawana vitabu. Kwenye televisheni tumeona kuna baadhi ya shule wanafunzi wengine wanakaa chini ya miti, shule zingine hazina vyoo lakini mimi nashangaa Serikali inatumia vigezo gani kuhakikisha kwamba shule imepewa kibali mpaka ikawa shule? Unakuta shule zingine hazina vitu vyote hivi muhimu lakini wamepewa kibali cha kuendesha shule, hii inawapa shida sana watoto wa kike, wanakosa masomo, wengine

wanakosa masomo kwa zaidi ya siku saba sababu tu hamna choo shulenii. Kwa hiyo, tunaomba mliangalie suala hili, mtusaidie ili wanafunzi wetu waweze kusoma na kuwe na usawa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tuseme kwamba, matatizo ni fedha, fedha zipo. Kwa mfano, kwenye Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amesema suala la Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Maofisa wa Wizara, wanakuja Dodoma wakati wa Bajeti, wanakuja kufanya nini? Wote wanakuja na magari yao, wanakuja na wasaidizi wao, zote hizi ni fedha zinatumika; sasa hivi tunaenda na teknolojia tuko kwenye karne ya 21, tunatakiwa tutumie *teleconference*, wakae kulekule kwenye Ofisi zao, kama ni maswali wajibu kulekule hakuna sababu ya kuwaleta, kuwaketisha hapa juu wanasikiliza tu, kama ni kujibu maswali wanaweza wakajibu kulekule kwenye Mikoa yao na hii tutakuwa tuna-save hela kwa ajili ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lillonishtua, ni katika randama ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wameomba shilingi bilioni moja (1), yaani shilingi bilioni moja (1) kwa wananchi wanaoniskiliza ni milioni 1,000 wameziomba kwa ajili ya kuzika Viongozi wa Kitaifa, hii ni aibu na inatisha. Ukizingatia tuna matatizo ya fedha, matatizo yamejaa kila mahali, unatenga shilingi bilioni moja (1) kwa mtu ambaye yuko hai; hii ni *priority* yetu kweli kama Taifa? Mimi naomba tu kuuliza au wamesikia kuna kiongozi gani anayefariki karibuni wanatenga shilingi bilioni moja (1)? Inasikitisha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika hospitali zetu wanawake wanajifungulia chini kwenye sakafu, watoto wanakufa. Katika Bunge hili Tukufu, kuna Hospitali moja iliyoko Moshi inaitwa *Saint Joseph*, ile Hospitali ni Teule, nimekaa hapa Bungeni mwaka wa sita sasa hivi, hospitali ile wamejenga *wards* za kusaidia wanawake, wamejenga *wards* za watoto, wameomba vitanda 50 tu, vina-cost milioni 17 ili wanawake wale waweze kulala vitandani na kuweza kujifungua. Mheshimiwa Waziri Mkuu, natumaini wakati huu utawasadia

wale masista waweze kupata vitanda. Kwenye hii shilingi bilioni moja (1) basi toa hapo milioni 17 upeleke kule *Saint Joseph* wapate vitanda na ile hospitali yetu ya Mawenzi ambayo bado *theatre* inasuasua hawana fedha. Watu kwa magonjwa madogomadogo, vidonda, inabidi waende *KCMC*, wanaenda kujaza Hospitali ya rufaa kwa magonjwa ambayo yangeweza kutibika kwenye hizi hospitali ndogondogo. Kwa hiyo, mimi ninaomba kwamba, Serikali, iangalie, iweke vipaumbele vyetu vya muhimu ni vipi, badala ya kupeleka fedha kwenda kuzikia Viongozi ambaao bado wako hai. Hakuna sababu ya kutenga fedha nyingi namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unaniruhusu, naomba nizungumzie kidogo suala la upatikanaji wa maji. Suala la maji kama tunavyojua maji ni uhai, tunayatumia kwa killimo, wanadamu hata kwa wanyama. Nitaanza na Jiji la Dar-es-Salaam; kwa kweli, Serikali, imesema inajitahidi italeta maji kutoka Ruvu, lakini bado maji safi na salama ni tatizo katika Jiji la Dar-es-Salaam. Wanasema ni 68% tu ya maji yanayopatikana Dar-es-Salaam ambayo ni safi na salama, lakini si kweli. Ukipungua maji ya bomba yanayotoka katika mji wa Dar-es-Salaam ni machafu, ukitaka kufua nguo nyeupe inabidi uyakinge yatulie ndio ufue. Watu wa Afya, tumeona wakituhimiza ukichota maji ya Dar-es-Salaam ni lazima uchemshe unywe. Sasa kwa hali ya umasikini wa Tanzania sasa hivi, mtu yuko pale Dar-es-Salaam, hajui atakula nini mchana, unamwambia anunue maji ya dumu Sh.100/=, akanunue mkaa Sh.500/= achemshe anywe, atayafanya kweli hayo? Kwa hiyo, ninaomba hayo maji yatakayokuja sasa hivi basi yawe ni maji safi na salama kweli. La sivyo, kipindupindu hakiwezi kwisha Dar-es-Salaam, magonjwa ya kuhara hayawezi kwisha katika Jiji la Dar-es-Salaam kwa sababu, maji sio safi na wala sio salama.

Mheshimiwa Spika, vilevile hii inaenda sambamba pamoja na maji taka, mji wa Dar-es-Salaam unajengwa, majengo ni mengi, maghorofa ni mengi, wakazi wanazidi, lakini ile mitambo na *system* ya kupeleka majitaka bado ni ileille, haijaongezwa. Kwa hiyo, inabidi *Master Plan* ya Dar-es-

Salaam waangalie wanajenga mifereji mipyä ya kupeleka maji machafu au ni ileile? Kwa sababu, ukiangalia pale barabara ya Mwaikibaki, *Shoppers Plaza* na *TMJ Hospital*, nimekuwa nikilisema mara nydingi sana, maji yanajaa pale, pana daraja, siku moja watu watakuja kufa pale. Kwa sababu, ukiendesha gari pale kwenye kile kidaraja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.  
(*Makofî*)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Mimi nitachangia katika elimu, mazingira na kidogo afya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wanafunzi wengi wamepata sifuri na wengine wamepata *Division IV* ile ya mwisho, naomba nishauri tu mambo machache katika elimu yetu. Kwanza kabisa, naomba Serikali iweke mpango kwa ajili ya kuwasaidia hawa wanafunzi waliopata sifuri Kwa sababu, elimu ya Sekondari ndio kifunguzi cha maisha ya mtu ye yote yule, hasa wanafunzi wetu. Kwa hiyo, nachoomba ni Serikali iweke mpango kwamba, hawa wanafunzi waliopata sifuri ikiwezekana wapewe ruhusa warudie mwaka mzima halafu wafanye tena mtihani. Naomba niombe kwamba, warudie tena kwa sababu, najua wakisoma *part time* halafu wakafanya mtihani matokeo yanaweza kuwa ni yaleyale. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali, iangalie namna gani wanafunzi hawa wanawenza kusaidiwa kwa ajili ya ufunguo wa maisha yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali pia kuwepo na namna ya kupanga umri wa watoto. Wanafunzi wa darasa la kwanza wanatakiwa wote wawe na umri mmoja, ndio maana wenzeru wanafanikiwa sana katika elimu zao;

hawapeleki mtoto wa miaka 10 akasoma na mtoto wa miaka saba (7), wote wakati wa Januari wanapoanza shule, wanatakiwa wawe umri mmoja. Kwa namna hiyo, inakuwa *effective* kupima uwezo wao, wanapofeli unaweza ukatafuta ni kwa nini huyu amefeli lakini kama tukipeleka mtoto wa 15 na mtoto wa miaka 10, hatuwezi kupima uwezo wao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaomba pia niishauri Serikali, kutoa maagizo kwa Wakuu wa Shule kwamba, *information is power*, inawezekana shulenii wanafunzi wakatumia simu, lakini itafutwe namna nzuri ambayo Serikali itafanya hizi simu zitumike kwa manufaa ya wanafunzi hawa; zinatumika kucheza *game*, kupelekeana *message*, mwisho wa siku ni kwamba, hakuna *concentration*. Kwa hiyo, tutakuwa tunafanya yale ambayo hayatakiwi kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri, katika elimu ya msingi, mitihani ya *multiple choice* ya hisabati isiwepo. Kwa sababu, watoto hawa ni wadogo sana kuweza kujaribu kufanya hizi hesabu, ili uweze kupata jibu ambalo linaendena na kile kilichoandikwa kwenye karatasi. Mitihani iwe kwa namna ya kwamba, inaweza kumsaidia mtoto kuwa mbunifu kidogo na kuweza kuchambua mambo. Vilevile na elimu ya sekondari, ni vizuri hata kama ni *multiple choice* inafanyika, lakini nayo wale wanafunzi wawe tayari wanaweza kufanya majaribio, halafu ndio wanachagua swali ambalo linafaa. Mtihani wa Darasa la IV na Kidato cha II, ni vizuri pia ukafanya kwa makini na ukazingatiwa vizuri sana, yule ambaye atashindwa aweze kurudia darasa. Mwisho wa siku inawezekana kabisa akaendelea vizuri kwa sababu, kufeli sio mtoto mjinga, wakati mwingine unakuta ni *immaturity* tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninaomba pia kuwe na ukaguzi. Serikali, iweke mkazo kwenye ukaguzi wa shule. Wakaguzi wamekuwa mara nyingi hawapati vitendea kazi, wanakaa maofisini hawana magari, wakati mwingine ana

gari, lakini hana mafuta na shule hizi zinahitaji ukaguzi. Ukaguzi unatakiwa uwepo kwa sababu, wapo pia Walimu watoro ambaao hawafundishi, lakini mwisho wa siku tutasema wanafunzi wamefeli, wakati tulikuwa hatukagui shule. Kama Serikali, imeshindwa kununua magari kwa Wilaya zote kwa wakati mmoja, basi angalau maeneo mengine ufanyike ukaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kama kweli kuna madai ya stahili za Walimu na lenyewe liangaliwe ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni nyumba za Walimu; nashauri kwenye mpango wa *PPP*, Halmashauri za Wilaya, zigawe maeneo karibu na shule kwa ajili ya watu binafsi nao waweze kujenga nyumba ambazo Walimu wanaweza kukodi, sio lazima Serikali, ifanye kila jambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye jambo la pili. Tumesema katika vivutio vitatu ambavyo vimewekwa kwenye *Seven Wonders of The World*, Mlima Kilimanjaro upo. Katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, kumekuwa na kukata miti kwangi sana kiasi ambacho taftiti zinasema hata ile *glacier* itayeyuka; ninashukuru kinachofanywa na Serikali ya Mkoa na hata na Idara ya Misitu ya Maliasili, lakini kwa kweli kuna haja ya kuweka mkazo sana katika kupanda miti.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka iko mikutano iliyofanyika Kancún, ya mazingira ambayo imetengeneza *fund* ambayo inaitwa *Green Climate Fund*, ambayo iliahidi itatoa dola za Kimarekani bilioni 100 kwa ajili ya kusaidia mpango huo. Kwa sababu, mabadiliko ya Tabia ya Nchi yatakuwa yanatuathiri sana na wanasema katika mwaka 2020 kiwango cha kilimo kitashuka kwa 50% na 18% ya misitu itakuwa imetoweka na watu milioni 75 mpaka milioni 250

watakuwa wanakosa maji safi na salama na kwa hivyo, kutengeneza magonjwa mengi. Maana yake ni kwamba, Serikali pia na uchumi wetu utatetereka kwa sababu, Serikali, itaacha kufanya mambo mengine badala yake iwe ina-deal na magonjwa ambayo yatakuwa yametokea. Kwa hiyo, mimi ninaomba Serikali, ifanye kazi kwa bidii kabisa na hawa wafadhili, kwa ajili ya kusaidia hizo fedha zipatikane kusaidia changamoto za *climate change*.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka pia *EU* ilikuwa imesema itajenga Kituo cha Mabadiliko ya Tabia ya Nchi Tanzania, lakini hapa karibuni nimesikia kwamba, Serikali, tunasuasua kupokea mradi huo na mara wanasema unaenda Nigeria. Sasa ninaomba kama ni kweli hivyo, Serikali, ijizatiti kwa vile hicho kituo kiweze kujengwa Tanzania kwa sababu kitatusaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni ongezeko la watu ambapo sensa ya makazi inasema tuna watu milioni 44.9, *growth rate* ni ya asilimia kubwa kabisa, Serikali ili langalie hili. Nakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuwa anazindua hizi takwimu za sensa na makazi ya watu alisema kabisa kwa kutilia mkazo kwamba, kuna haja ya kuweka mpango madhubuti wa uzazi ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanazaa kutegemeana pia na pato la Taifa yaani *growth rate* ya pato la Taifa iwe inaendana pia na jinsi ambavyo Watanzania wanazaa watoto wengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza, niseme tu kwamba, njia moja ya kutatua matatizo tuliyonayo makubwa ni kujielekeza kwenye kilimo. Hivi sasa kilimo chetu, wakulima wetu 70% wanatumia bado majembe ya mkono, 20% ndio wanatumia *plough* na 10% ndio wanatumia matrekta. Ni dhahiri kuwa kilimo hakiwezi kuwa endelevu kwa sababu asilimia kubwa ya mfumuko wa

bei unatokana na chakula na kama hatukujielekeza vizuri katika kuzalisha chakula cha kutosha na ikawa nchi ambayo ina hekta zaidi ya milioni 10 na *point* zaidi za kuzalisha chakula, tunaagizia chakula mpaka leo, hali yetu itakuwa mbaya sana. Kwa hiyo, la kwanza naomba Serikali, ijielekeze kikamilifu na kwa mpango mzuri zaidi kuhakikisha kilimo tunakibadilisha kutoka kilimo cha mikono na kuanza kutumia matrekta. Haya matrekta 2,000 yaliyoagizwa bado hayajafikia hata idadi ya matrekta yaliyokuwepo 2006 ambapo tulikuwa na matrekta 17,000 leo tuna matrekta 8,000. Kwa hiyo, bado ni kidogo sana na hayawezi kubadilisha mfumo wa kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala zima la miundombinu. Nashukuru, nimeisikia Serikali ikitumia kwamba, mradi wa reli unaendelea vizuri, lakini naomba Serikali, ikae kitako, ijipange upya, ihakikishe huu mradi unamalizika sio reli kuitengeneza vipandevipande, haitatusaidia hata kidogo. Bandari na reli ni lazima viunganishwe kama kweli tunataka tukwamuke katika matatizo ya kiuchumi tuliyonayo, hizo ndio njia mbili pekeyake za kufanya, kama tulivyofanya kwenye *stimulus package* tukapata *1.7 trillion*, basi tufanye hivyo hivyo kuondoa tatizo la reli na bandari, haraka iwezekanavyo. Vinginevyo tutaendelea kupiga hadithi na hazitamalizika.

Mheshimiwa Spika, la tatu. Tuna maeneo ambayo yanazalisha kwa kiwango kikubwa mazao ya pamba na korosho. Tumeona katika bajeti zote zilizopita kwamba, tunashughulikia zao la pamba, bado kuna 10% tu ya pamba inayosafishwa ndio inasafirishwa nje, 90% bado inaendelea kuwa ni *raw cotton*; hatuwezi kubadilisha maisha ya watu hata kidogo. Una *population* kubwa ya watu milioni 7, 8, wanazalisha pamba na pamba yao bado ina tatizo la soko, bado wanununa pamba ambayo ina bei dhaifu; kama hatujali-*address* hilo bado tutakuwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa Serikali iwe na Mpango Mkakati kwa hili, kama vile ilivyo na Mpango Mkakati

wa Korosho. Ukiangalia urari wetu wa biashara sasa hivi sio mzuri hata kidogo, bado *importations* ni kubwa sana, lakini maeneo ambayo tunaweza tukaongeza kipato cha mkulima, maeneo ambayo tunaweza tukaongeza urari wetu wa biashara za nje ni korosho, karafuu, pamba; tukikazania maeneo hayo mimi nafikiri tunaweza tukapiga hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, la nne. Mazao ya baharini; ukiangalia takwimu za Serikali, zinaonesha kabisa sehemu kubwa ya mazao yanayosafirishwa baharini yanatoka kwenye ziwa la Viktoria 0.3% tu, lakini meli zinazovua za nje hivi sasa ni zaidi ya 110. Nalizungumza hivi, mimi bahati nzuri katika Jimbo langu la Wawi, upande wa Mashariki kuna eneo kubwa kabisa ni la *deep sea*, tunaziona meli kabisa za kigeni zinavua. Mpaka leo, pamoja na vyombo vidogovidogo kila siku kuharibiwa, lakini ni meli moja tu iliwhahi kukamatwa hapa Tanzania ikiwa imevua kiharamu, wakati kuna zaidi ya meli 100 zinavua kiharamu na meli moja ina wastani wa tani 2,500. Ushahidi tumeupata kuna meli ambayo imekuwa *licensed* Tanzania, ikaingia kwenye maji ya Msumbiji ikakamatwa, ikatozwa *fine* ya Euro 1,300,000 na meli hiyo imekuwa *licensed* Tanzania; sasa kama meli hiyo moja tu ndio imeingia Msumbiji ikakamatwa, meli ambazo tumeambiwa ndani ya Bunge hili na Wizara kwamba, ziko 111 je, ngapi katika hizo zimechukua *tones and tones* za samaki na kuondokanazo bila Watanzania kufaidikanazo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado kuna vitu ambavyo tunaweza kuvifanya vya harakaharaka tukawaondolea Watanzania umaskini kwa rasilimali zao ambazo ni za kuvuna tu kama samaki, kama pamba wanayolima, kama korosho wanazolima, kama karafuu wanayolima. Ningombaa sana Serikali ijielekeze katika hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la madawa ya kulevyia; sasa hivi katika dunia wanazungumzia sana madawa ya kulevyia kwamba, eti baadhi ya nchi waruhusu watu wauze madawa

madukani, ili kuondosha tatizo la kukamatwa watu kwa sababu, mtandao ni mkubwa. Kuna wastani wa dola bilioni 300 kwa mwaka zina-*transact* katika madawa ya kulevyia, sasa hii dhana imeanza kuingia kwa mataifa makubwa. Juzi tulipokuwa kwenye *IPU*, imekuja kama ni sehemu ya mjadala kwamba, sawa tutumie madawa, pengine itakuwa ni sehemu moja ya kuzuia madawa ya kulevyia, sisi tukasema hapana, huwezi kumwachia nguruwe shamba la muhogo ukategemea utavuna. Wanataka kutuulia vijana wetu wamalizike na ninaiomba Serikali kabisa, hizi dhana zimeanza kujengwa katika *level za Kimataifa*, tuanze kuwa makini nazo. Sasa nchi moja kwa mfano itakubali, ya Kiafrika, ikaruhusu na wewe ni *neighbour* wako, tayari una tatizo la msingi kwamba, tayari kuna soko na kuna *supplier*, wewe unafanya nini? Kwa hiyo, ni lazima tujipange vizuri katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba hii *agency* ambayo inashughulika na madawa ya kulevyia, kwanza iwezeshwe, lakini vilevile sasa ianze kutoa *education program* kwa vijana wetu kuona athari za mtu anayetumia madawa ya kulevyia. Sisi Wabunge, tulipopata fursa ya kuona kila mmoja alitaharuki, lakini ile *education* ilimalizikia kwa Wabunge tu. Mimi ninafikiri sasa isambae, iende kwa vijana waone athari za kutumia madawa ya kulevyia.

Mheshimiwa Spika, wako vijana wetu wengine wamekamatwa nje huko wana kesi, wamekimbia hapa Tanzania, wapo huko, wamejificha. Wagundulike wakamatwe, yaani hii hali ni lazima ichukuliwe hatua za haraka sana, *otherwise* jamii itateketea yote. Njia ambazo zinaingiza madawa wote tunaelewa, Tanzania *route* yake kubwa ni Pakistan, inaeleweka kabisa. Tupambane nayo kwa hali zote, *areas* ambazo zinajulikana lazima tupambane nazo. Naelewa vita vyenyewe sio ndogo ni kubwa, lakini ni lazima tujielekeze huko.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulisema, ni suala la Halmashauri. Ni aibu katika miaka hii hamsini hatuna hata Manispaa moja inayochangia kwenye pato la Taifa kwa maana ya kodi, zote zinategemea Serikali Kuu, sitegemei Dar es Salaam isiweze kujitegemea, lakini lazima mfumo wetu wa kodi urekebishwe ili Dar es Salaam iweze kujitegemea. Kama Johannesburg wanaweza kujitegemea, kama California inashinda hata nchi chungu nzima za dunia *why not* Dar es Salaam, *why not* Mbeya, *why not* Iringa *and so forth*. Lakini bado ni sera zetu za kodi hatujazielekeza vizuri ili tuweze kurekebisha hali hiyo ili Halmashauri, Manispaa ziweze kujitegemea badala ya kujitegemea Serikali Kuu. Tukifanya hivyo, demokrasia itakuwa ndani ya Serikali hizi na wananchi watapata uwezo wa kuamua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kuhusu bajeti yetu ya Bunge. Tunao Mfuko wa Bunge lakini bado umebakia Mfuko nadharia, *its high time* sasa Serikali ituachie Mfuko wetu, tuuendeshe wenyewe kwa sababu zifuatazo: Sisi na Mahakama, hivi sasa tumebadilisha mfumo wa bajeti, Kamati hizi za Kisekta za Bunge zinahitaji kuwezesha sana ili kufanya kazi vizuri na kuja hapa na takwimu sahihi, sasa hamuwezi kufanya katika utaratibu huu wa kazi kwa kutegemea *cash budget*, lazima muwe na bajeti zenu mlizojipangia, mlizojipangia Kamati, mlizojipangia Bunge lenyewe kufanya shughuli zake, bila ya hiyo hii *exercise* tulioifanya ya ku-review utaratibu wetu wa kibajeti haitasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunahitaji kuhakikisha Wabunge wetu wanapata bima ya maisha, wanapata Bima wakiacha kazi waonekane wamefanya kazi vizuri tu, yote haya yanataka kufanyika, lakini yanafanywa kwa kutegemea Mfuko wa *cash budget*.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda niseme tu, kwa sababu tunaingia katika mfumo mpya wa kibajeti na kwa sababu tunataka kuujaribu mfumo huu mara hii, hatutafanya vizuri sana, lakini mwakani tutafanya vizuri kwa sababu ya ile *budget circle* tutaanza nayo mapema.

Tunaomba upande wa Serikali ujitarishe kwa vipaumbele ili mtakapokuja sasa mtuambie kutokana na mpango wa 2020-2025 na mpango wa miaka mitano maeneo gani mmeshayafanya kazi, yapi bado, tatizo la fedha limetokea wapi na tatizo la utekelezaji limetokea wapi?

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu kuna tatizo la miradi mingi inakwenda miaka mitatu, minne, gharama zake za kuiendesha ni kubwa na matokeo yake wananchi hawaoni matunda ya miradi hiyo kwa sababu imechukua muda mrefu. Mfano, uwanja wa Songwe, zaidi ya miaka kumi tunauzungumza hapa ndani ya Bunge, mfano hai tu na mingine mingi. Kwa hiyo, moja ambalo linatuongeza gharama ya bajeti ya Serikali ni kwamba miradi haimaliziki kwa wakati. Kama miradi haitamalizika kwa miezi kumi na nane tutaendelea kuwa na tatizo hili sugu la kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama fedha hakuna tusipange miradi, tupange mradi tukihakikisha kuna fedha. Kwa kupiga ramli tu, tukapanga mradi, tutapata matizo haya kila siku na kila Mbunge atataka aingiziwe shilingi tano, kumi, kumi na tano, matokeo yake hakuna kinachotekeliza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kwa mara ya kwanza, naiunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana na umechangia vizuri tu. Nilisema namwita Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atafuata Mheshimiwa Faida Bakari na atafuatiwa pia na Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba uniruhusu nianze kwa kunukuu maandishi kutoka katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Kulingana na matarajio hayo Tanzania ni Taifa lenye sifa kuu tano zifuatazo:-

Maisha bora na mazuri, amani, utulivu na umoja, utawala na uongozi bora, jamii iliyoelimika na inayopenda

kujifunza zaidi na uchumi wenye uwezo wa ushindani na kutuletea ukuaji wa kudumu kwa maslahi ya watu wote.

Mheshimiwa Spika, lakini aliyeandika dibaji hii ni Mheshimiwa Benjamin Mkapa Rais wa awamu ya tatu, anatoa angalizo juu ya kufikia hapa; anasema amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao ni mazingira ya lazima kabisa ya msingi kwa maendeleo, bila mazingira hayo dira hii haitapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nimenukuu haya kuwakumbusha tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu juu ya Tanzania tunayoitarajia 2025 na wananchi kwa ujumla wajue hivyo. Lakini hatutaweza kufika hapo kwa chokochoko zinazotokea sasa na hasa hizi za kidini. Nataka kuisihi Serikali, haitoshi kuwaambia viongozi wa dini wazungumze na waumini wao, wajibu wa Kikatiba wa kulinda amani nchi hii ni wa Serikali, Serikali ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa rai pia kwa Serikali. Inaonesha kwamba, wenzetu wa *TRA* wanajitahidi kufanya kazi yao, lakini zipo Wizara ambazo pia zinapaswa kukusanya pesa kwa jina linaloitwa maduhuli. Wizara hizi ni kama Maliasili, Mifugo, Ardhi na nyininge kama hizo. Lakini kwa jinsi miundo ya Wizara zilivyo na wafanyakazi hao walivyo ndani ya Wizara hizo hawaoni kama hii ni kazi yao muhimu. Ombi langu ni kwamba, Serikali ihakikishe Wizara hizi zinapewa uwezo wa kutosha na elimu ya kutosha kwa sababu ndiko ziliko fedha nyangi zaidi hasa hizi za kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme pia, katika muundo wa Serikali tunalo Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) ambalo lipo chini ya Wizara ya Viwanda, kwa majukumu na kazi ambazo wamepewa *NDC*, naona kwamba shirika hili lingekuwa limewekwa vizuri zaidi chini ya Tume ya Mipango ikiwa ni mkono mzuri wa kuweza kusukuma maendeleo. Hili linakwenda sambamba na *NBS* (*National Bureau of Statistics*) ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha, ambayo kimsingi kama *TRA* haitaweza kwenda sambamba na *NBS*. *NBS* inakwenda vizuri na uchumi na mipango.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza hapa ni juu ya uwiano wa maendeleo. Ukiangalia nchi yetu, kuna sehemu ambazo zimepiga hatua na zingine zipo nyuma na zote hizi zinatakiwa pia zipewe fedha ili ziweze kupiga hatua zaidi, lakini tunataka kuona mkakati wa Serikali wa makusudi unaoelekeza nguvu yake katika sehemu zile ambazo bado hazijapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, mambo haya hayaonekani sana kwenye bajeti, hata katika vitabu vya bajeti sasa utakuta ile mikoa ambayo ina fedha nyangi inapata fedha nyangi zaidi, lakini pia ndani ya mikoa yenyewe Wilaya nydingine ziko duni na Wilaya nydingine zimekwenda mbali sana. Hili jambo Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba uliangalie na uweze kuweka mpango wa makusudi kabisa wa kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani wakati Wilaya moja, vijiji karibu vyote vina umeme, Wilaya ya Mbinga haina kijiji chenye umeme. Haiwezekani wakati Wilaya zingine zina maji ya bomba katika vijiji vyake vingi, Wilaya zingine hazina, hiki nacho ni chanzo cha uchokozi na chokochoko. Kwa hiyo, natarajia kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu atayasikiliza haya na kufanya marekebisho. Reli ilijengwa na Mjerumani hajjaweza kuongezwa tena na hivi watu kama wa Ruvuma ambako ndiyo mahindi yanatoka, hakuna namna ya kutoa yale mahindi kutoka kule Songea, kutoka Mbinga kuyapeleka Arusha, kuyapeleka Manyara ambako ndiko yapo mahitaji, hii *dichotomy* lazima tuimalize.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatakiwa kuwekeza na inanunua hisa katika makampuni mbalimbali hasa kuititia NDC na kuititia TPDC na wanatakiwa watoe fedha taslimu kununua zile hisa, lakini hawafanyi hivyo, wakati wakifanya hivyo, zile fedha zitazaa fedha nyangi zaidi. Kwa hiyo, naiomba Serikali yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ifanye hilo jambo, isione kwamba itapoteza hiyo fedha italeta fedha nyangi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, naipongeza Serikali kwa kuliangalia hili suala la ruzuku na kuamua kwamba, sasa

vikundi vyote tutakwenda kwenye mabenki kwa kupertia vikundi vya wakulima. Lakini najaribu kuangalia *representation* ya *banks* katika vijiji haipo, hivi vikundi vitasafiri mwendo mrefu sana kwenda kwenye mabenki katika Wilaya na Mikoa. Naiomba Serikali ifikirie njia nyngine mbadala zaidi za kuwezesha hivi vikundi vikapata hii mikopo pale walipo badala ya kwenda kwenye Wilaya au Makao Makuu ya Mkao, lakini wazo lenyewe ni zuri na ningeomba pia wafanye mazungumzo na mabenki waweze kupata *a better deal, deal/waliyonayo* hivi sasa siyo nzuri sana. Benki zinapata kiasi kikubwa, lakini Serikali haipati pamoja na kwamba *guarantee* inatoa na fedha inatoa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie viwanda, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imezungumzia habari ya viwanda, lakini ningependa tu kusisitiza kwamba, tunayo baraka kubwa ya Mwenyezi Mungu ya madini ya chuma kule Liganga na wenzetu wa *NDC* pamoja na Wachina wanashirikiana kuwekeza, lakini sioni mipango inayooonesha tutakitumia vipi kile chuma. Baadaye tutaishia kuvisafirisha kwenda China. Ningependa kuona tunaanzisha viwanda vya magari kwa wakati huu sasa, lakini pia ningependa kuona fedha nyngi zaidi zinawekezwa *SIDO* kama ambavyo hotuba ya Waziri Mkuu imetaja mafanikio makubwa ya *SIDO*, wanahitaji nguvu ya kifedha waweze kufanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha mapenzi makubwa kwenye kilimo. Tulianza na *power tillers*, sasa tumeingia kwenye matrekta ambayo yanatoka India. Pale *CAMATECH* ambayo ni Taasisi ya Serikali wametengeneza trekta, wapewe nguvu hao *CAMATECH* watengeneze matrekta yapelekwe Wilayani yakafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati na madini, hotuba ya Waziri Mkuu pia imezungumza hasa kwenye kupunguza *inflation* kwamba umeme umekuwa mwingi zaidi na kwa hivi *inflation* imepungua. Lakini sielewi kwa nini mpaka leo tunakuwa na tatizo la umeme. Tunavyo vyanzo vingi; tunayo makaa ya mawe pale Ngaka; Wilayani Mbanga na sioni juhudhi ya Serikali ya kutumia yale makaa ya mawe katika kuzalisha

umeme. Mjadala wa *TANESCO* na wawekezaji unaendelea na hakuna anayeingilia kati. Naomba Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu washirikiane na *NDC* kuhakikisha kwamba mradi huu unaweza ku-*take off* kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na madeni, kuna madeni ambayo Serikali inadaiwa yapo ya wakulima kule Mbinga, wakulima wanadai milioni 400 na yako ya wafanyakazi hasa Walimu. Ningombaa Serikali hii ilipe, badala ya kusherekea miaka hamsini, ingelipa madeni haya.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie madini, nimesoma hotuba ya Waziri Mkuu imezungumza juu ya maeneo ya madini mbalimbali katika vijiji; Mbinga tunazo sehemu za Masugulu, Kitai, Mkako, Paradise na Ruanda. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapohitimisha na hawa nao ni wananchi katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jamii, tunayo shida ya maji kule katika Mji wa Mbinga. Nashukuru niliongea leo na Mheshimiwa Waziri wa Maji, ataweka mradi mzuri pale Mbinga mjini, lakini pia kuna Kata ya Litumbadosyi na Vijiji vya Luhagala, Mabuni na Kingoli vina hiyo shida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia katika Wilaya ya Mbinga pamoja na Nyasa hakuna Sekondari ya Serikali kwa maana ya kama Kibaha na Pugu. Sekondari zilizopo ni za Kata na za Misheni, zimetaifishwa na sisi pia tunahitaji Sekondari nzuri kama ambazo zimejengwa katika Mikoa mingine ya Pwani, Dodoma na sehemu kama hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nassari!

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na kwa

sababu ya muda, naomba nisisome. Leo asubuhi mbele yetu yamesomwa maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbowe na kwa mujibu wa utaratibu ilitakiwa wote tupate nakala ya ile hotuba lakini cha ajabu ni kwamba baadhi ya Wabunge hatujapata na tunapouliza tunaambiwa kwamba zimetengenezwa nakala 200 peke yake kwa mujibu wa taarifa za wahudumu huku ndani na Wabunge tuko zaidi ya mia tatu. Sasa tunapata wasiwasi kwamba kuna watu watachangia na kuna watu wanaendelea kuchangia na wataweza kujaribu *ku-encounter* na wanaweza wakaongea uongo wakati wengine hatujapata hiyo hotuba.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa nini kwa mujibu wa taratibu hatujapata nakala ya Mheshimiwa Mbowe kama ambavyo tulipata ya Mheshimiwa Pinda jana kwa idadi kamili ya Wabunge wa Bunge lako.

**SPIKA:** Ahsante. Unajua sisi watu wazima saa nyiningine huwa tunasema maneno ili yawe yalivyo, hotuba zile zimekwenda *very late* kuchapishwa. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema zitafika, zipo, naomba unielewe hivyo. Siwezi kumwambia kiongozi wa Upinzani umechelewa kupeleka, siwezi nikasema hivyo, ndiyo maana nikasema zitakuja.

Tunaendelea! Nilisema nitamwita Mheshimiwa Waride Bakari Jabu atafuatiwa na Meshack Opulukwa.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, kabisa nami naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono, naomba kuchangia ukurasa wa 11 kwenye mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Naishukuru Serikali kwa kuanza tena mchakato wa kupeleka vijana katika Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kukuza uzalendo wa vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na jitihada hiyo ya Serikali, naomba Serikali ianzishe fani ya ufundi ndani ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hii itasaidia vijana hawa katika kujifunza uzalendo ndani ya jeshi, lakini pia wataweza kujifunza fani mbalimbali za ujuzi ambazo zitaweza kuwasaidia wakati wakiwa uraiani waweze kutumia ujuzi huu katika kujiedeleza kimaisha na kuzalisha vijana wengi ambao tayari wamepata mafunzo ya kijeshi, lakini hawana ujuzi na matokeo yake tutakuwa tumezalisha vijana ambao wataingia katika wimbi la ujambazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia katika tatizo la madawa ya kulevyo. Kwa kweli limekuwa ni janga kubwa kwa Taifa letu na sisi sote ni wazazi, tumeona na tumekuwa tunashuhudia watoto wetu wanavyoathirika na janga hili. Licha ya juhudhi ya Serikali na wadau mbalimbali kuchukua juhudhi zinazofanywa na wadau mbalimbali katika kutatua tatizo hili lakini bado tatizo limekuwa kubwa na linaendelea kuharibu au kuwaweka watoto wetu mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke mpango kabambe ambao utawabaini na kuwatangaza hadharani wadau wote wakubwa wanaohusika na mtandao wa madawa ya kulevyo hapa nchini na kisha kuwachukulia hatua za kisheria. Tusipofanya hivi kwa kweli tutaendelea kuliangamiza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia sasa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninavyofahamu, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mwajiri mkubwa wa wafanyakazi wote kwene Serikali za Mitaa na Halmashauri zote za hapa Tanzania Bara. Lakini tunaona sasa hivi kwa muda mrefu hususan Walimu wamekuwa wanachangia katika vyama vyao vyao huko makazini mwao.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni jinsi gani Ofisi inavyosimamia haki ya wafanyakazi pale wanapokuwa wanachangia michango mikubwa katika hivi Vyama vyao Wafanyakazi. Kwa kuwa tumesikia, basi kwanza nataka kujua

fedha hizi zinazokatwa kwa Walimu na wafanyakazi wengine zinakaguliwa na nani? Pia kwa nini Serikali haioni haja ya kuletwa Muswada hapa Bungeni ambao utavikagua hivi vyama ambavyo vinawakata wafanyakazi katika sehemu zao za kazi. Ukiuliza unaambiwa wanakatwa fedha, lakini hizi fedha haziwafaidishi wafanyakazi hawa pindi wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu ilisimamie hili na pia uletwe Muswada wa Sheria hapa Bungeni wa kuona jinsi gani hivi Vyama nya Wafanyakazi vitaweza kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi mpaka leo nimekuwa napata shida sana kuona kuwa nchi yetu bado haijajizatiti au haijalpa kipaumbele shughuli au mambo yote yanayohusiana na kukabiliana na maafa. Nalisema hili hata ukifungua ukurasa wa 71 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sijaona mahali ambapo jinsi gani nchi imejitayarisha na kama yametokea maafa jinsi gani tutaweza kukabiliana nayo na watu wetu tumewaandaa vipi na maafa yatakayotokea, lakini pia kurudisha zile hali za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimepata mashaka sana katika suala hili, tumekuwa tukielezwa hapa kwa muda mrefu kwamba, tutaletewa Muswada wa Sheria ya Kukabiliana na Kuratibu Shughuli za Maafa, lakini mpaka leo bado hatujaletewa Muswada huu na sijui tutaletewa kwa muda gani.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, tukitaka tusitake, sasa hivi nchi yetu imekuwa inaendelea sana na maendeleo makubwa. Katika maendeleo yoyote lazima pawe na changamoto zake. Changamoto ndiyo hizo tunazoziona; kunatokea mafuriko ya ajabu sana, watu wanapoteza uhai katika sehemu mbalimbali na mambo mengi ambayo kwa kweli nchi sasa hivi lazima ikubaliane na maafa.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia juzi tu lilipoporomoka Jumba pale Dar es Salaam. Idara ya Zimamoto na Uokoaji kwa kweli ilikuwa haina vifaa. Serikali ijizatiti kuiwezesha Idara hii; Idara pale ilichukua muda wa kuokoa kutockana na ukosefu wa vifaa vilivyokuwepo pale. Tushukuru wamekuja wanajeshi na watu wengine ambaao waliweza kutusaidia katika kuokoa au kulidhibiti lile janga, lakini kwa kweli inatisha.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali sasa hivi iwekeze leo kwa ajili ya usalama wa kesho. Tusione tabu kununua vifaa ambavyo tutaiwezesha hii Idara ya Zimamoto na Uokoaji ili linapotokezea janga lolote uokozi uweze kufanyika kwa salama na kwa haraka zaidi. Lakini pia hata ukiangalia Idara yenewe ya kuratibu maafa, sielewi kwa kweli kama ina uwezo mkubwa wa kufanya shughuli za kushughullikia maafa kiutendaji, ujuzi wa wafanyakazi wake, lakini pia hata kama wana vifaa ambavyo vitaziwezesha Wizara zinazohusika kufanya kazi kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwanza, tuanzishe *Emergence Operation Centre* ambayo isiwemo pale ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu tunajua tukianzisha kituo hiki kitakuwa na mitambo. Mitambo ile pengine *for security reason* itagongana na mitambo ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hiki kituo tukitoe ndani ya lile jengo. Kituo hiki tukiweke na kiwe na wataalam wote ambaao linapotokezea janga au tatizo lolote; wao watakuwa wa kwanza kupata habari na kutoa habari kwa wanaohusika ili suala lile lishughulikiwe. Tusipofanya kuwekeza hivyo bado tutabakia Idara ya Maafa inangojea kupata habari kutoka vyombo vya habari au kwingineko na sio wao wenyewe. Naomba sana hili lifanyike.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba sana tuanze na utaratibu wa elimu kwa jamii nzima. Kwa sababu inaonekana dhahiri, elimu ya kukabiliana na maafa kwa jamii yetu ni ndogo, yanapotokea maafa wananchi wanayaafuata badala ya kuyakimbia. Hivyo, nashauri sana tuiwezeshe hii Idara iweze kutoa elimu kwa wanajamii na walibakia.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kuwa Idara ya Maafa sasa hivi tayari imeshakuwa na sera na mpango wake wa kukabiliana na maafa. Lakini utaona kuwa sera ile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Meshack Opulukwa, halafu atafuata Mheshimiwa Ally M. Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Mariba.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii illi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza kabisa nianze kujikita kwenye uendelezaji wa *CDA*. Wakati nasoma kabrasha hili ambalo ni orodha ya majedwali iliyoambatanishwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilikuwa najaribu kuangalia ile kasima namba 1001, nikaona kwamba hakuna hata fedha moja iliyotengwa ya uendelezaji wa Makao Makuu ambayo ni *CDA Dodoma*.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kufahamu, kwa sababu hata leo asubuhi kama siyo jana Naibu Waziri wa Uchukuzi anasema kwamba, Serikali inajipanga na iko mbioni kuhakikisha kwamba uendelezaji wa Makao Makuu (*CDA*) yanakamilika kwa wakati na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara. Katika bajeti hii ya Waziri Mkuu, hakuna mkakati wowote wa makusudi ambao Serikali imeazimia.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua pamoja na Watanzania wengine kama Serikali imesitisha mpango huu ambao ulikuwa ni mpango mzuri wa kufanya Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma kwa kuendeleza *CDA*

yameshindikana au mkakati bado unaendelea kwa sababu haionekani kama kuna jitihada zozote zile za makusudi za kuweza kulifanikisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala la mafunzo ya JKT. Mimi ni mdau, mionganoni mwa Wabunge ambaao tulikwenda kwenye mafunzo ya JKT na Kambi yangu ilikuwa pale Msange 823 KJ na jina langu naitwa ni Afande Service Man 0591 Meshack Opulukwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yameonekana ni mafunzo ambayo ni mazuri na mafunzo ya maana na hasa kwa watumishi pamoja na watendaji mbalimbali wa Serikali pamoja na Idara nyingine. Napendekeza na nashauri ili kuweza kurudisha heshima pamoja na uzalendo wa Watanzania ambaao umepotea kutokana na mafunzo ya JKT kwa muda mrefu; sasa badala ya mafunzo haya ambaao Wabunge tulikuwa tunachukua kwa muda wa wiki tatu, sasa yafanyike kwa muda wa miezi mitatu kwa sababu ni ya maana sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ningeomba kwa Wabunge wote ambaao hawajapitia JKT sasa iwe ni lazima waende JKT kulitumikia Taifa ili kuweza kuona jinsi gani ya kulikomboa Taifa letu, ambalo sasa hivi linaandamwa na mambo mengi ambayo nadhani kama tutaendelea hivi, tutakwenda sehemu ambayo siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Mkoa wangu wa Simiyu, nilikuwa naangalia kasima ya kilimo kwenye Wilaya yangu ya Meatu. Hakuna hata shilingi moja iliyotengwa kutokana na ambavyo nilikuwa nikisoma bajeti ya Waziri Mkuu kuhusu kuendeleza kilimo kwenye Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu, pamoja na kwamba, Wilaya ya Meatu katika Mkoa wote wa Simiyu, ndiyo Wilaya ambayo ni kame kuliko Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana hakuna jitihada zozote ambazo Serikali imeziweka kwa makusudi ili kuwakwamua watu hawa ili kuweza kuondokana na suala

la kuleta chakula cha msaada kila mwaka, kitu ambacho nadhani hakina tija kwa watu wetu wa Meatu.

Mheshimiwa Spika, naomba, kupitia Wizara ya Kilimo, kuna maeneo ambayo Serikali ilikuwa imeanisha ya umwagiliaji. Eneo mojawapo liko kwenye sehemu mojawapo ya bonde kubwa sana la Mto Semu, kwenye Kijiji cha Mwagila. Kuna fedha ambayo ilikuwa imetengwa, lakini miaka miwili imepita sasa mradi huo haujaanza na ile fedha haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, naomba, ili kuonesha kwamba wana Meatu nao wako katika ramani ya kilimo cha Tanzania, Mto huu na bonde hili ambalo ni muhimu sana kwa kilimo cha umwagiliaji liweze kufanyiwa kazi na watu waweze kujikwamua na upungufu wa chakula kutokana na umwagiliaji unaotokana na maji ya Mto Semu.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa niongelee suala lingine ambalo ni eneo la uwekezaji. Mwezi uliopita Wizara ya Maliasili iliamua kuwarudishia wananchi wa Loliondo eneo la takriban asilimia sitini ili iweze kulitumia kwa mambo yao wenyewe kutokana na mgogoro ambao umekuwa ukiendelea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi Tanzania imekuwa ikiendelea mara kwa mara na hii inatokana na wawekezaji kuwa na maeneo mengi na maeneo makubwa ambayo wameshindwa kuyafanya kazi na badala yake migogoro katika nchi imeendelea kuwasumbua wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sasa Wizara inayohusika kwa eneo letu ambalo limekuwa na mgogoro kwa muda mrefu kwenye Pori la Akiba la Makao ambao ni *WMA*, ni eneo la hekta 19,000 lakini unakuta mwekezaji anataka kupewa lile eneo kwa jumla ya shilingi milioni sitini tu kwa mwaka, fedha ambazo hata wafugaji wenyewe wangechangia shilingi 5,000/- kwa mfugaji mmoja wa Wilaya ya Meatu

wangeweza kupata zaidi ya *billions of money* kuliko kumpatia mwekezaji kwa shilingi milioni sitini na watu wetu wanazidi kuhangaika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kwa eneo hili la Pori la Akiba katika nchi hii, Serikali sasa imefika muda muafaka wa kuwarudishia wananchi maeneo haya wayafanyie kazi badala ya kuwa kwenye mikono ambayo siyo sahihi sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la *SACCOS*, *SACCOS* zimekuwa na matatizo mengi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Naomba nitoe mfano mmoja mzuri sana kwenye Mkoa wa Simiyu kwenye Wilaya ya Meatu. Kuna *SACCOS* ya vijana ambayo ilianza kwa shilingi milioni mia moja na sitini na mbili kama miaka mitano iliyopita. Leo hii viongozi wa *SACCOS* hii wamejikopesha pesa ile yote na mpaka sasa hakuna mwanachama ye yote ambaye anaweza kwenda kukopa fedha katika *SACCOS* ile kwa sababu fedha zile hazipo.

Mheshimiwa Spika, tulikaa katika Baraza la Madiwani tukiwa na Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wetu tukakubaliana wale wote ambao na hili lilikuwa ni azimio la Baraza la Madiwani ambao wamefuja pesa hii, wameitumia kwa faida yao wenyewe, watu hawa wafikishwe Mahakamani kuanzia mwezi wa pili tarehe 18. Mpaka tunavyoongea hivi wananchi wa Meatu, wamekatishwa tamaa kabisa na masuala ya ushirika, wamekatishwa tamaa kabisa na masuala ya *SACCOS* hii ni kwa sababu ya kutokuwa na umakini katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba TAKUKURU pamoja na Jeshi la Polisi, liweze kuifanya kazi *SACCOs* hii ya Meatu, ili kujua ni akinanani wameyafanya haya na zile fedha zimekwenda wapi? Wanaodai amana yao waweze kurudishiwa ili angalau imani kwa watu wetu iweze kurudi kwa *SACCOS* yao pamoja na Serikali yetu nzima.

Mheshimiwa Spika, sipendi kugongewa kengele, nashukuru sana kwa nafasi, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Mariba, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii fupi ya dakika kumi, lakini nyingi sana kwangu. Kwanza napata shida sana kujuu nini maana ya bajeti. Tunakaa hapa Wabunge tunapanga bajeti kwa kutegemea pesa za wafadhili, wafadhili hawaweki pesa, wafadhili wenyewe wanafilisika kule Cyprus, Ugiriki na Italia, sisi tunakaa tunazozana hapa bajeti, bajeti, pesa hatuna. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tujitahidi tukusanye pesa sisi wenyewe, vyanzo tunavyo! Tunakuja hapa tunakaa siku themanini, siku tisini kupiga kelele ya bajeti, kwenda kule Halmashauri hakuna kitu, Wazungu hawaajaleta pesa, mpaka lini tutegeme Wazungu? Hatukudai Uhuru nchi yetu hii mama, kutegemea wakoloni waliotoka. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa nachangia kidogo kuhusu hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ukurasa wa kumi na mbili. Anasema wanaadhibu Halmashauri ambazo zinapata hati chafu; wananchi wanapata matatizo kwa ajili ya watendaji wabovu, wanachakachua pesa, baadaye wanaadhibiwa wananchi wetu sisi, wanakosa barabara, wanakosa madawa kwa ajili ya watumishi amba wanahamishwa Wilaya hadi Wilaya na wanalindwa. Hii haikubaliki hata kidogo na haitakubalika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, waaajiriwa wenu wenyewe kule Wilayani hatujui mlikowataoa, wanaiba pesa, leo mnaadhibu wananchi wetu, hiyo haikubaliki!

Mheshimiwa Spika, pesa za RADA, mwanzo kabisa mkatuambia zitajenga mashule, madawati, nyumba za Walimu na madarasa, leo mnatuambia vitabu, nani

kaidhinisha hilo. Tena vitabu hivyo mkachapishe huko Ulaya hela zirudi Ulaya huko huko, Wabunge tukatae hilo suala, tukatae ndugu zangu Wabunge, tusikubali kuyumbishwa, pesa zenyewe zilikuwa zimeibiwa, sasa zinataka ziibiwe mara ya pili. Hiyo ni *EPA* nyingine, tusikubali kabisa, pesa zote, madawati, kwanza vitabu vikija vitachafuka tu, watoto wamekaa chini. Kaone Korogwe kule hakuna dawati shule nzima, leo unapeleka vitabu, vitakaa wapi, hata ofisi ya kuweka vitabu hakuna. Acheni kutuchazea akili! (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha kilimo, *Power Tiller* 4,000 zimeletwa, zimetoka pesa za kigeni bilioni 38.8. Ndugu zangu, hizi pesa zingeimarisha umwagiliaji, jengeni mabwawa, watu walime hapa hapa. Leo ni aibu Tanzania inaagiza mchele Pakistan, tunawasaidia wakulima wa Thailand hawana soko la kuza chakula, wanatuuzia Tanzania. Sisi tuna mapori kila mtu anashangaa, leo mnashindwa kuimarisha sehemu za umwagiliaji, mnatoa hela uduchu kama kule kwangu mnaita fedha za *Ujutu* kwa watu 3,000, wanataka kumwagilia mashamba kule Kilando lakini pesa hampeleki, mnataka kuwatahirisha wananchi wa kule Thailand na Pakistan, kuagiza mchele wao mbovu. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni aibu kuagiza chakula kwa nchi hii nje ya Tanzania!

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege, nimesoma hapa Sumbawanga haikutengewa pesa, yaani Uwanja wa Songwe ndiyo uwe Uwanja wa Sumbawanga? Mtueleze hapa. Leo Sumbawanga wanalipa nauzi kama nauzi ya kwenda Dubai. Ni aibu, hakuna uwanja Sumbawanga, wala kutengewa pesa Sumbawanga, kwa vipi? Wenyeewe siyo binadamu? Wanatenga Viwanja vidogo vidogo, Sumbawanga hakuna.

Mheshimiwa Spika, hili ni la kuangalia sana na Sumbawanga ni moja ya Mikoa Tanzania, tunataka uwanja wa ndege, hatukubali! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, barabara ya Sumbawanga-Kanazi, Kanazi-Kibaoni ni kama changa la macho, barabara imekaa walitwambia miezi 30, leo imefika miezi 36. Wachina wanabaki wanaiza kokoto, wanalima michicha, hawana kazi wanayofanya. Barabara ina thamani ya bilioni 76 mpaka iishe itakuwa bilioni mia moja arobaini. Serikali tunakwenda wapi? Leo hakuna kinachofanyika katika ile barabara, hakuna Wachina wamesimama, wanaiza changarawe ndiyo wanaishi, wanaiza mchicha ni aibu! Pelekeni pesa kule wananchi waone kama kweli inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Vijiiji kando ya Ziwa Tanganyika, nilizungumza mara ya kwanza nilipokuwa Bungeni hapa. Wananchi wa kule hawajaona barabara hata ya kupita gari wala bajaji, hakuna! Vijiiji viko chungu nzima kado ya Ziwa Tanganyika hakuna barabara. Kuna Kijiji cha Kalila, Mkombe, Kazovu, Isaba, Chongokatete, Kisambara, Msamba, Nindye, Mwinza, Lusebwa, Lyapinda, Izinga, Tundu na hata barabara ya Itindi- Kibaoni. Hii barabara ya Kala-Wampembe siyo barabara, hazipitiki kabisa, ni jina la barabara tu. Tumeomba hapa kila siku, barabara ziende *TANROAD* wanatuambia fungu hakuna, lakini kwingine wanaomba barabara za lami, mnawapa!

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na maneno mengi sana, lakini naiomba Serikali izingatie haya machache nillyosema ambayo yana umuhimu. Kuhusu maji, katika nchi yetu kila Kijiji kina matatizo ya maji. Tuna miaka hamsini, nilizungumza mapema sana hapa, wakati wa Rais wa Awamu ya Kwanza tulikuwa na maji yanamwagika, leo Awamu ya Nne ndugu zangu maji hakuna, sijui yamekwenda wapi. Serikali inakaa inatazama wananchi wanagombania maji, miaka hamsini ya uhuru mtu anagombania maji!

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine tupo, kama mimi Mbunge nimekaa siku tatu siogi, niliwaambia mapema hapa Namanyere hatuogi, hatuna maji, tuoneeni huruma. Leo mkisikia tunakwenda kupigana na Malawi, anadai kidogo tu baadaye mnapigana, sasa mbona mnaachia kule

kando ya Ziwa Tanganyika hakuna huduma yoyote, DRC Kongo ikiingiza majeshi pande hiyo, ndiyo mtatuletea barabara? Tunaomba barabara kando ya Ziwa Tanganyika, ni wananchi wa nchi hii, walidai Uhuru kama nyie, leo mnataka wakimbilie wapi? Hakuna Mmachinga Mfipa hapa! Dar es Salaam nimetembea, hakuna Mmachinga Mfipa. Sasa wajengeeni miundombinu wasihamie Dar es Salaam, wajengeeni miundombinu wananchi wa Rukwa, leo watu wote Wamachinga sijui wametoka wapi wale? Wamejazana pale wanauza vichupi na visidiria, sasa mnataka wananchi wote wauze vichupi na visidiria Dar es Salaam? Tunawaomba muamke, tunataka haki sawa kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi/Vicheko*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Nyambari Chacha, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdalla Salehe na Mheshimiwa Felix F. Mkosamali.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kuchangia hoja hii, moja kwa moja kwa kusema kwamba, Watanzania kwa kiasi kikubwa wamechoka na suala la rushwa katika Halmashauri zetu. Hili Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba uliangalie kwa makini kwa sababu, nchi inakosa miradi ya maendeleo kwa sababu ya rushwa ambazo zimekithiri katika Halmashauri za Wilaya zetu. Hili jambo tulifikirie na tulizingatie kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika hotuba yake, Waziri Mkuu ameelleza kwamba atajitahidi kadri itakavyowezekana kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo. Hawa wachimbaji wadogo wadogo wanaotaka kuendelezwa, nataka kuwafahamu ni akina nani? Kwa sababu nina ushahidi katika Jimbo langu la Tarime wachimbaji wadogo wadogo kila siku naahidiwa wataendelezwa, lakini ukiangalia wachimbaji wadogo wadogo wanaotaka kuendelezwa ni watu ambao wana maeneo makubwa, ambao wameingia mikataba na wawekezaji. Hao ndiyo mnataka kuwaendeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali tuwe *serious* katika kuhakikisha kwamba wale wachimbaji wa chini ambao hawana eneo lolote lile wapewe maeneo ya kuchimba kama ni dhahabu au mtakavyoangalia, lakini nashauri utafiti wa kutosha ufanyike.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swalii moja, tuna rasilimali nydingi za Taifa letu; tuna mito, bahari, dhahabu, gesi na vitu vingine chungu nzima. Maliasili kama vile wanyama, misitu, lakini suala la umaskini katika nchi yetu ndilo ambalo nataka kuuliza, hivi linatokana na nini? Naomba tufanye mjadala wa Kitaifa. Hebu tutafute watu wanaoweza kukaa na kufikiri, maana katika historia tunasoma kwamba kuna nchi ambazo zilikuwa zinatuma watu, wanakaa wanafikiri, wakishafikiri wanapendekeza njia mbadala na njia sahihi za kuweza kupata maendeleo. Naomba tujaribu kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuongelea suala la fedha za rada. Wabunge waliotangulia wameongelea. Kwa kweli hili suala linasikitisha sana kwa sababu tulikaa sisi wenyewe tukapitia na kukubaliana kwamba hizi fedha zitanunua vitabu, zitajenga baadhi ya nyumba za walimu na madarasa. Sasa jana tumesikia tena mnasema kwamba zitanunua vitabu vya shule za msingi na fedha za madawati zitakwenda katika Halmashauri Nane tu.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mgawanyo bora wa rasilimali za Taifa au inakuwaje? Hizo Halmashauri nane zina nini cha ziada na ukiangalia kwamba tatizo la madawati katika nchi ya Tanzania lipo katika kila Halmashauri, hata Makao Makuu ya nchi tu hapa Dodoma na miji mikubwa kama Dar es Salaam ni tatizo kubwa sana, sasa kwa nini fedha za madawati ziende katika Halmashauri nane tu? Ina maana Halmashauri nydingine hazihitaji madawati? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hilo kwa kweli hatutakubaliana nalo, hivyo naomba mlirekebishe. Hata hivyo vitabu vinavyotaka kwenda kuchapishwa, tunajianaa kwamba tubadilishe sera ya elimu, sasa tukibadilisha sera ya elimu hivyo vitabu vitatumika kwa muda gani? Kwa kweli tuangalie hizo

fedha namna tutakavyozitumia ili ziweze kuendana na hali halisi na mazingira ya Kitanzania, lakini siyo kuonesha sehemu, kama kuvaan kwa upendeleo tu, hilo hatutakubali kwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hotuba ya mwaka jana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba, atajitahidi sana kuhakikisha kwamba anapunguza matumizi ya Serikali hasa suala la mashangingi. Sasa hivi utakuta mashangingi ni mengi na ndio yanazidi kununuliwa na kutumika tu. Kwa nini tusitumie magari ambayo kwa kweli siyo mashangingi na ambayo yanatumia mafuta kidogo? Katika hilo naona kwa kweli, tunatumia matumizi makubwa sana pasipokuwa na ulazima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo vile vile napendekeza kwamba mfumo wa elimu katika nchi yetu ya Tanzania urekebishwe; Vyuo vyote vya VETA viwe chini ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia kwa maana ya kwamba kule VETA tunafundisha mambo ya ufundi ambayo ni *application of technology*, kwa nini sasa viwe chini ya Wizara ya Elimu?

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la amani, suala la udini, naomba Serikali isimamie na ilinde watu wake. Sasa hivi kuna chokochoko za udini, kesho au keshokutwa tutaanza ukabila, hii nchi haitakuwa kisiwa cha amani tena.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niongelee suala la Mto Mara ambao uko katika Wilaya za Tarime, Serengeti na Ranya. Huo Mto unakufa na siyo kwamba unakufa tu, bali unameza baadhi ya vijiji kwa sababu tope limejaa ndani ya Ziwa Viktoria, maji ya Ziwa hilo yamefurika katika huo Mto na baadhi ya Vijiji kwa mfano Kongoto, Ghuta, Nyamakanga na Wegilo na Kijiji cha Ikongo kimekwishamezwa kabisa lakini Serikali kila siku tukipiga kelele, tukiwaambia watendaji kutoka Halmashauri, Wakuu wa Wilaya sijui kama hawaoni hilo tatizo. Naomba hilo jambo na lenyewe lifikiriwe kuangalia namna gani Serikali itakavyoweza kunusuru ule Mto Mara.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala ilisitisiza kwamba hebu Wabunge wajengewe ofisi zao Majimboni kwa sababu Mbunge unapata hifadhi ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya au Ofisi ya Mkurugenzi. Hao ndiyo wanakuhifadhi, siku akiamua au ukienda kinyume naye anakufukuza. Hii ni aibu, tunaomba Wabunge kwa kweli wajengewe ofisi zao katika Majimbo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la maji katika Wilaya ya Tarime. Mwaka jana nilipiga kelele na sasa hivi nalisema kwamba, Wilaya ya Tarime tangu tupate uhuru, haina maji safi na salama kwa ajili ya afya ya watu wa Tarime. Naomba suala hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie. Mwaka jana wakati wa Wizara ya Maji nilisema, nikaahidiwa kwamba, maji yanafanyiwa upembuzi yakinifu, sijui nini na nini na kila kitu. Hebu naomba sasa hivi muwaambie wananchi wa Tarime kwamba ni lini watapata maji safi na salama kutoka Ziwa Viktoria au Mto Mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la barabara katika Wilaya ya Tarime naomba nimalize nalo, kwa kusema kwamba, utakuta baadhi ya Wilaya zina barabara za lami kila sehemu, lakini unapoongea na Waziri anayehusika anasema kwamba, hizo barabara siyo za Kitaifa, au ni za Halmashauri. Lakini ukiuliza kwamba hizi Wilaya zingine zimepataje barabara za lami? Wanakwambia kwamba, *TANROADS* wamejenga.

Mheshimiwa Spika, naomba mgawanyo wa rasilimali katika nchi yetu uwe sambamba na vilevile tuhakikishe kabisa kwamba tunasaidia Wilaya zilizoko pembezoni kama Tarime ili ziweze kupata maendeleo kwa sababu ni aibu. Unapoongia katika nchi ya Kenya utakuta kuna barabara za lami kila sehemu mpaka vijijini, umeme kila sehemu mpaka vijijini, lakini ukija Tanzania giza tu, matope matupu, inakuwa ni aibu.

Mheshimiwa Spika, naomba tuzingatie na tuhakikishe kabisa kwamba, katika kufanikisha hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie barabara alizotuahidi kule Tarime. Kwa mfano,

kuna barabara kutoka Mangucha - Kibaso kwamba inakuwa chini ya *TANROADS* na itawekewa lami, naomba hiyo ahadi yake itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilisema Mheshimiwa Mkosamali atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa siyo mimi?

**SPIKA:** Nani, Mheshimiwa Masoud! Aah, samahani nimechanganya. Kweli ni Mheshimiwa Masoud kwanza, atafuatiwa Mheshimiwa Mkosamali halafu atakuja Mheshimiwa Abeid.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nimekusamehe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya njema hadi nikijadili hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika kurasa zote 82 za hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hajaonesha sehemu yoyote jinsi ya nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, ametuomba sh. Trilioni 4.2, lakini kwa kuwa hakuna eneo hata moja ambalo ameonesha jinsi ya nidhamu ya matumizi ya fedha hizo. Kwa kuwa mwaka jana alituomba sh. Trilioni 3.8 na tukampatia, napata mashaka juu ya watendaji wake katika Ofisi za Mikoa na Halmashauri za Wilaya, ambako kumebainika ubadhirifu, wizi na ujisadi mkubwa katika maeneo hayo. Mheshimiwa Waziri Mkuu tukimpatia fedha hizo, je, ana mikakati gani ya ziada kuhakikisha watendaji waliobainika na ujisadi na wizi huo atawea kuwashughulikia kama ifuatavyo, hilo la kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika hali nyingine ningeomba niseme kwamba, ukurasa wa 66 katika hotuba ya mwaka jana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonesha anakerwa sana na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati akizindua Bunge hili Mwezi Novemba, 2010 alisema: "Wizi, ubadhirifu na ujisadi hautavumiliwa." Akasema, tutakuwa wakali sana kukemea maovu haya na kudhibiti jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kumbe wengine ni wakali wa kuiba, napata mashaka makubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa hotuba yake haioneshi hata kidogo kukerwa na jambo hili, je mara hii amepata kigugumizi gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ukurasa wa 31 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu unaosema mwenendo wa bei za mazao na maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alieleza kwamba, kuporomoka kwa bei za baadhi ya bidhaa kunatokana na kukosekana au kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia. Lakini vile vile Serikali hapa inaonekana imejisahau yenye, mikakati yake ambayo ni hafifu katika kuweza kuthaminisha bei za bidhaa katika maeneo mbalimbali. Moja, katika kazi za kuthaminisha ni kujenga viwanda. Vile viwanda ambavyo vilijengwa lakini bahati mbaya vilikuwa au vilikuwa kwa misingi mingine kwa aina yoyote vilikuwa vifufuliwe. Kuna viwanda ambavyo vilikuwa, lakini Serikali hadi sasa wameweza kuvibinafsisha kwa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja hapa kufanya majumuisho, naomba anieleze ni kwa sababu zipyi viwanda vya korosho vya Mikoa ya Mtwara na Lindi vimeuzwa kwa bei ndogo kwa vigogo wa Serikali ambao nyie mnawajua, lakini hadi wakati wa Bunge lililopita Waziri wa Viwanda na Biashara tulipotaka kumwambia atupe maelezo kwa nini haviendelezwi, alisema atawaita. Je,

Mheshimiwa Waziri Mkuu Kiwanda cha Korosho cha Mtwara Mjini aliyemilikishwa ni nani?

Mheshimiwa Spika, naomba kuelewa kwamba Kiwanda cha Newala *One* nani ni mmiliki wake? Ni mkakati gani ambao mmeuandaa kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinafufuliwa. Masasi nako vile vile, Nachingwea, Mtama, Likombe, Lindi Mjini, Kibaha, viwanda hivi vyote wamepewa vigogo wa Serikali na mnawajua. Ni sababu zipi za msingi zinafanya mpaka leo viwanda hivi hamuwezi kuviiingiza katika mkakati wa kuboresha maisha ya Watanzania? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo halikubaliki na si zuri. Naomba kwa vyovyote iwavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifanya majumuisho atwambie mwaka 1970 hadi 1980 Serikali ilikopa dola za Marekani milioni 20, lakini viwanda hivi vimeuzwa kwa bei ndogo na wanaochukua ni viongozi wakubwa wa Serikali. Kama hamuwezi kuwaita basi mtwambie ni kwa nini mnalindana? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 60 - 61 una suala zima la elimu ya Sekondari. Matokeo ya hivi karibuni ya kidato cha nne yanaonesha kwamba idadi ya waliofaulu ni kidogo sana, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema tusitafute mchawi, tusilaumiane. Naomba Watanzania mnaonisikiliza muandike, mchawi nambari moja ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyokataa kuwasikiliza Walimu.

Mheshimiwa Spika, Walimu wana matatizo mengi lakini Serikali haiwasikilizi. Fedha zao za mishahara ni tatizo kwani hazipatikani vizuri. Fedha za madaraja wakipandishwa hazipatikani, hata wakipatiwa *arrears* hakuna. Fedha za likizo vile vile ni tatizo na fedha za mazingira magumu ni tatizo. Sasa mnasema mnatafuta mchawi, mchawi namba moja ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba kazi hii ya ualimu ni ngumu kweli. Niseme kwa haraka haraka maana ya neno UALIMU.

U- maana yake ni usumbufu, A- maana yake ni adha kubwa inayopatikana kwa Walimu, L – maana yake ni lawama, I- maana yake ni inda, kila jina anapewa Mwalimu, M- maana yake mahangaiko na U-maana yake uvumilivu na umaskini umewajaa Walimu. Umaskini unasababishwa na Serikali. Kwa nini Serikali haiandai mazingira mazuri ya kuboresha maslahi ya Walimu? Tatizo ni nini? Jamani muwaonee huruma Walimu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye ukurasa wa 71 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo amezungumzia ukame, amegusia ukame wa kukosa chakula. Hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hajaonesha mahali popote juu ya maafa yanayotokea katika ajali za barabarani pamoja na kwenye maji.

Mheshimiwa Spika, kuna Watanzania wengi wamekufa kwenye maji, katika maziwa pamoja na bahari, lakini inaonekana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili halikuwa la kipaumbele katika maandishi yake. Naomba atakapokuja hapa alieleze Bunge hili, awaeleze Watanzania ni sababu zippi za msingi zilizompelekea asiwatambue hata kwa kuwapa pole wale ambao walikufa katika maji na katika barabara, tatizo ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye maendeleo ya sekta ya uvuvi kwenye ukurasa wa 36. Mambo mengi yamesemwa, mkakati wa uvuvi haramu mtashirikisha ulinzi shirikishi, lakini mna mkakati gani wa kuweza kuboresha wavuvi hawa kwa kuwakopesha fedha za kuwaendeleza na kuwapatia zana? Hakuna katika hotuba hii. Hili nalo ni tatizo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho awaeleze Watanzania ana mikakati gani ya kuweza kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo katika bahari na kwenye maziwa. Hili ni jambo kubwa na wavuvi siku zote ni maskini.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye vitambulisho vya Taifa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza hapa juu ya vitambulisho vya Taifa, lakini pia nataka niseme

kwamba kuna watu ambao si waaminifu. Kuna watu wanaingiza baadhi ya wananchi wa nchi jirani kwa ajili ya kukaa na kwa ajili ya ufugaji. Je, nini mikakati ya Serikali juu ya watendaji wabaya na waovu wanaochukua rushwa mipakani ili kuwaingiza wananchi kutoka nchi jirani ambao wanaendelea kukaa katika nchi hii ya Tanzania? Serikali hili mnalifahamu, je, mna mkakati gani?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho atueleze. Lakinije, kwa nini mnawavulimia au mnataka kuwapa vitambulisho vile vya utaifa ili wapige kura? Kama ndiyo mkakati wenu mwaka 2015 badilisheni umeshatambulika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo siyo ya kawaida, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mambo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Ngoja nimwite Mheshimiwa Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, kisha atafuatiwa na Mheshimiwa Kange Lugola na Mheshimiwa Sylvester Mabumba ajiandae.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuchangia kuhusu mchakato wa Katiba namna gani unadorora na unaharibiwa na Tume na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza haya kama alivyoeleza vizuri Kiongozi wa Upinzani Bungeni kama hayatabadilishwa maana yake tunapitisha fedha ambazo zinakwenda kuharibika tu, maana Katiba mpya haitapita. Watu wamechaguliwa na wananchi lakini wanachakachuliwa na viongozi wa Chama cha Mapinduzi huko kwenye mikoa. Sasa Waziri Mkuu wakati anahitimisha ili mchakato wetu uweze

kwisha salama, tunaomba atwambie na asitishe zoezi linaloendelea, mtu akichaguliwa anakwenda moja kwa moja kwenye Mabaraza ya Katiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kwenye mchakato huu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tulimtembelea Mheshimiwa Jaji Warioba, tunamheshimu, lakini alizungumza kwamba, hata tukimuita sisi Kamati hatakuja kwa sababu Tume yake iko huru kwa sababu ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, si Tume yake tu ambayo iko huru, wala ile haiondoi Bunge kufanya kazi yake ya *oversight*, hatuwezi kuacha mambo yaende hovyo hovyo, tupitishe bajeti ambayo tunajua mwisho wa siku Katiba mpya haitapatikana kwamba tusimuite wala tusimhoji kwenye Kamati, hicho kitu hakipo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka pia kuhoji kwenye mchakato huu wa Katiba, fedha za Bunge la Katiba ziko wapi? Mmetwambia kutakuwa na Bunge la Katiba, *Vote* yake iko wapi? Tumeoji kwenye Kamati, lakini hatukupewa majibu yanayoeleweka. Fedha za Bunge la Katiba ziko wapi? Ni shilingi ngapi? Wabunge hao watalipwa nini? Nitaomba nipewe majibu na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo kwenye mchakato wa Katiba naomba nizungumzie Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tumeshasema kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi haitaweza kusimamia kura ya maoni, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ameomba fedha ya kwenda kuboresha Daftari la Wapiga Kura ambalo litatumika kwenye kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, hilo halikubaliki hata kidogo, tunachotaka sheria iletwe. Hawa wanakwenda kubadilisha daftari lipi ambalo linatumika kwenye mchakato wa Katiba? Sheria inasema ni *two third* (2/3) Zanzibar na Bara, tunaipata vipi hiyo *two third* (2/3)? Kuna Watanganyika ambao wapo

Zanzibar ambao hawatambuliki kwenye sheria ya ZEC ya Zanzibar, unaboresha hilo daftari kwa ajili ya mchakato wa Katiba ili iweje?

Mheshimiwa Spika, kuna Watanganyika ambao hawapigi kura hata za kuchagua Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, kuna Wazanzibari ambao wako huku Bara ambao na wao wanatakiwa wapige kura ya *two third*, sasa hiyo sheria mnailetea lini? Mnawapa fedha wakaboreshe daftari lipi ambalo halitasaidia mchakato huu kukamilika. Tunataka sheria ili fedha hizi mnazokwenda kuwapa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha daftari ziende kufanya kazi ambayo inaeleweka kutokana na mchakato huu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache ya Katiba, naomba nije kuzungumzia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Fedha ambazo zimekuwa zinapitishwa kwa ajili ya Fungu la Msajili wa Vyama vya Siasa, nyangi ni kwa ajili ya ruzuku za Vyama, lakini CAG amekuwa hakagui fedha hizi. Sasa hivi Msajili wa Vyama anaomba bilioni 19, sasa tunataka Msajili awe anakagua fedha, pia tujue Vyama gani vinapata hati safi na Vyama gani vinapata hati chafu. Hatuwezi kuwa tunapitisha mabilioni ya fedha, halafu hayakaguliwi, tunapitisha pitisha, mnaogopa nini kukaguliwa? Mnaogopa nini? Tunaomba fedha hizi zinazopitishwa kwa ajili ya ruzuku za Vyama vya Siasa zianze kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, ndio maana kwenye randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeona kuna fedha nyingine zinatoka kwenda kuchapisha vitabu kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa Ilani ya CCM. Sasa tumewapitishia fedha kwenye ruzuku kwa ajili ya Chama chenu, bado mnakwenda tena Ofisi ya Waziri Mkuu mnachukua fedha kwenda kuchapisha vitabu kwa ajili ya kuangalia Ilani yenu sijui mmefanya vitu gani na nini na mmeshindwa namna gani au mmefanikiwa vipi? Sasa tunachotaka fedha hizi zikaguliwe kama fedha zinazokwenda sehemu zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la Kitaifa kabla sijarudi Jimboni kwangu, nizungumzie vitambulisho vya Kitaifa,

nina kitambulisho ambacho nimepewa, Wabunge tumepewa hiki kitambulisho, huhitaji kwenda nchi za mbali sana ku-*compare*, nime-*compare* tu na kitambulisho cha Zanzibar. Hivi vitambulisho tunavyopewa, maana mnatenga fedha ili mwendelee kutoa vitambulisho, sasa sijui ni vitambulisho au nini sijaelewa. Kwa sababu kinaandikwa jina, Felix Francis Mkosamali na jinsia na namba ya kitambulisho na mwisho wa kutumika; hakioneshi huyo Mkosamali anaishi wapi, anakaa wapi, anwani yake ipi, anafanya kazi gani, ni raia wa wapi, vinazidiwa hata na vitambulisho vya kupigia kura.

Msiende mbali, angalia kitambulisho cha Zanzibar hiki hapa ninacho, vitambulisho vya Wazanzibari vina jina, mahali mtu alipozaliwa, Jimbo lake wapi, kinakwisha lini, mnaletaje hivi vitambulisho, ndiyo mnataka kuchukua fedha kuandika jina la mtu na jinsia, hivi! Yaani ni jina na jinsia basi, ndiyo kitambulisho cha Utaifa! Sasa tunatafuta vitambulisho vya nini, vioneshe nini, kwa sababu sisi tuli-*expect* kwamba vitambulisho hivi vitatumika katika maeneo mengi, kupigiwa kura kwenye maeneo ya Kimataifa. Sasa vitambulisho vya namna hii, ovyo kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nirudi Jimboni kwangu, baada ya kuzungumza mambo hayo ya Kitaifa. Nianze na kilimo, pembejeo ambazo zimekuwa zinaletwa kwenye baadhi ya Wilaya zetu hazifai kabisa. Sasa naomba nimweleze jirani yangu Waziri kwamba, mkituletea mbolea kama za mwaka jana Minjingu na zile ambazo hazitumiki kwenye udongo wa Kibondo, hatutumii tena na wala hatutaki mbolea za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, mbolea ambazo tulishazikataa miaka yote ndiyo mnazotuletea, hatuhitaji mbolea ambazo hazifai kwenye udongo wetu ule. Tunawaambia hivyo na mnaendelea kutuleta tu na zinakuja kila siku kwa kuchelewa mwezi Desemba sisi tulishapanda zamani. Sasa naomba hivi kama mmeshindwa hizo fedha za kutuletea ruzuku mtupe tufanyie shughuli zingine, lakini kutuletea mbolea ambayo haitumiki, mnatunanihi.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba nichangie kuhusu Idara hii ya Maafa na Majanga. Nilivyofundishwa kwenye Sheria maafa au majanga ni kitu ambacho hujaki-overseeni *unforeseeable thing*. Sasa hivi tumesambaza umeme kwenye Wilaya nyingi sana ikiwemo Wilaya ya Kibondo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge naona kengele ya pili.

**MHE.FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza.

**SPIKA:** Ni ya pili.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Ni ya kwanza.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Sasa hizi Wilaya hazina magari ya zimamoto, majanga yakitokea maana yake zinaweza zikaungua hata nyumba 100, umeme umefika lakini magari ya zimamoto hakuna. Lakini jambo la ajabu ambalo nimekuwa nikilionia, kuna Idara ya Zimamoto inapita huko kwenye Majimbo yetu, hata mwaka huu imepita inatoza watu fedha 30,000 au 40,000 kwa ajili ya Zimamoto hakuna gari. Hizo fedha mnazowatoza watu ni za nini? Gari lipo Kigoma Mjini, Kibondo ni kilomita 300 kutoka Kibondo Mjini, mnatutoza fedha za nini, hakuna magari, kama siyo uchakachuaji na ujisadi ni nini? Mnatoza fedha za nini wakati hakuna huduma ambayo tunaipata kwa hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba wananchi wetu wasiendelee kutozwa fedha, lakini Serikali ihakikishe kila Wilaya yenye umeme inapelekewa gari la zimamoto ili kuepuka majanga ambayo yanaweza kusababisha hasara kubwa, tukaanza kulaumiana ooh sijui waokoaji na nini, *we have to oversee things before things happened.*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba niwashauri mkusanye kodi kama walivyoeleza Kamati ya TAMISEMI, *Service Levy* kwa watu wanaochukua tenda na shughuli

nyingine kwenye Halmashauri, Serikali itoe mwongozo kwenye Halmashauri zote nchini, lakini pia ikusanye kodi ya majengo (*property tax*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba niishe hapo, hayo ni maeneo ambayo nilijiandaa.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Kange Lugola na Mheshimiwa Sylvester Mabumba ajiandae.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia. Lakini katika Bunge la Bajeti liliopita nilimwomba Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, lakini maombi yangu naona mpaka leo hayajatekelezwa. Kwa hiyo, kwanza nataka nilikazie hoja yangu ile ili iweze kutekelezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, najua yeye akimwelekeza ataaelekea.

Mheshimiwa Spika, nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, Ofisi ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kule Zanzibar, upande wa pili wa Muungano, Ofisi ile ipo katika maeneo ya Ikulu na nikaiomba sana Serikali iweze kutenga fedha kwa bajeti ile iliyopita ili ofisi ile iondoke kule maeneo ya Ikulu iwe nje ili wananchi wanapotaka taarifa mbalimbali za kuhusu Ushirikiano wa Afrika Mashariki hasa kwenye mtengamano ule wa Afrika Mashariki maeneo hayo ya ushirikiano wa biashara waweze kuelewa vizuri au wakitaka taarifa hizi waweze kuzipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, lakini hadi sasa ofisi ile bado ipo kule kule na wala sijaona dalili yoyote ile ya kuondoka katika maeneo yale ya Ikulu. Naomba Waziri Mkuu alichukue hili ili Wazanzibari na wao wa upande wa pili wa Muungano waweze kufaidika na masuala haya ya mtengamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye kitabu hiki cha Waziri Mkuu, ukurasa wa 43, hali ya ajira nchini. Ni kweli vijana

wengi wasomi wapo mitaani na mwaka hadi mwaka tunaendelea kuzalisha vijana wengi wasomi ambao hawana ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia katika Wizara mbalimbali, Mashirika ya Umma na Halmashauri zetu, pale tunapofanya kazi za Kamati tunagundua kwamba kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu utakuta wanaokaimu ni wengi sio kwamba mfanyakazi yule hayupo ndiyo mwingine anakaimu hapana, unakuta kaimu juu ya kaimu na unakuta tunafanya kazi na makaimu wengi. Kwa hiyo, hii ni dhahiri kwamba wafanyakazi wamepungua sana katika maeneo mbalimbali ndani ya Wizara, Mashirika na hata kwenye Halmashauri. Wakati mwingine utakuta vitengo muhimu kama vya Wakaguzi wa Ndani, vina upungufu mkubwa wa wafanyakazi hata wakati mwingine tunasema kwamba ndiyo inasababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye hii hali ya ajira nchini Mheshimiwa Waziri pia ameweka hapa EPZ, EPZ wanahitaji fedha nydingi za kununua maeneo kwa ajili ya wawekezaji. Lakini mimi niiombe Serikali EPZ watenge fedha za ndani wasitengewe fedha za wafadhili ili waweze kupatiwa kiurahisi na maeneo haya yakipatikana kwa wawekezaji, ninavyoona ajira kwa vijana zinaweza zikapatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, lingine nasema hivi, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Tumeshuhudia hapa upotevu wa fedha za Serikali, CAG anatueleza kila mwaka wa bajeti jinsi upotevu wa fedha za Serikali, lakini nadhani Serikali bado haijalipanga vizuri na nasema mtoto umleavyo ndivyoakuavyo. Kwa sababu tumezoea kuwalea bila kuwachukulia hatua kali za kisheria, ndiyo maana upotevu huu unaendelea wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ilione suala hili na sasa liwe basi, tuna

vijana wengi wanahitaji ajira, kama mtu amechukua hela nyingi za Serikali, afunguliwe mashtaka na azilipe, lakini pia afukuzwe kazi, vijana wengi wa kuziba mapengo wapo. Naona hili liwe mwisho kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na vijana wengi watapata ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwa leo hayo yanatosha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kange Lugola atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba, nafikiri na Mheshimiwa Dkt. Mrema anaweza kufikiwa.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa CCM siungi mkono kabisa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Siungi mkono kwa sababu nina hoja mbili kuhusu mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme mwenye macho haambiwi tazama, wale wanaosema Serikali ya CCM haijafanya kitu kama hawaoni nitawapeleka wawe wanapapasa, watapapasa lami na vitu vingine. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge mnataka pesa zifurike kwenye Majimbo yenu kwa ajili ya maendeleo, lazima tupambane na vitu viwili vikubwa katika nchi yetu na ni vitu viwili vinavyohujumu uchumi wa nchi hii; vitendo vya rushwa na vitendo vya madawa ya kulevyia ndugu zangu ndivyo vinavyoangamiza Taifa letu na ndivyo vinavyosababisha tusipate fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nianze na madawa ya kulevyia na mnisikilize vizuri. Hotuba ya Waziri Mkuu imebaki tu kusema kwamba, kuna vita dhidi ya madawa ya kulevyia, sikubaliani nayo, hakuna vita hata kidogo vya kupambana na madawa ya kulevyia. Nilisoma kwenye gazeti moja Kamishna wa Tume ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevyia, Christopher Kyondo anasema wanawafahamu kwa majina wanaohusika na

madawa ya kulevya, lakini wameshindwa kuwakamata kwa sababu ya mbinu walizonazo. Maana yake ni nini? Maana yake kama siyo rushwa zinazosababisha wasiwakamate, ni watendaji wa Serikali na hata wakiwemo baadhi ya Mawaziri, ndiyo wanahusika na madawa ya kulevya. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hata Mheshimiwa Rais mwenyewe aliwahi kutamka kwamba, kuna viongozi wa dini na kwa majina wanaohusika na madawa ya kulevya. Kwa nini watu hawa na hao ambao Kyondo anawafahamu wasikamatwe na kutajwa kwa Watanzania ili wachukuliwe hatua. Ndugu zangu tusipodhibiti vitendo vinavyohujumu uchumi wa nchi hii tutaendelea kuwa na sungura mdogo, hatutapata maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la rushwa na nimesema siungi mkono. Vita ya kupambana na rushwa, manati lini ikampiga tembo au ndovu. Huwezi kupambana na rushwa ndugu zangu bila kuwekeza fedha kwa ajili ya kupambana na rushwa haiwezekani mahali popote pale. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwenye hotuba yake kwamba, kuna mianya ya rushwa, nini maana ya mianya ya rushwa? Nichukue mfano kwenye Jeshi la Polisi, kila siku wanaandamwa, Jeshi la Polisi wala rushwa, wanafanya tafiti; matokeo, Jeshi la Polisi ni namba moja kupokea rushwa, huku ni kuwapakazia Jeshi la Polisi katika kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, mianya ya kupokea ndani ya Jeshi la Polisi, mimi nimekuwa Askari wa Jeshi la Polisi. Cha kwanza ambacho ni mwanya, Jeshi la Polisi mishahara yao ni midogo, huo ndiyo mwanya wa kuziba. Askari ambaye mshahara wake ni mdogo anapokea 250,000, wakati huo huo analala kwenye jengo ambalo ni *godown*, mimi mwenyewe nimelala kwenye *godown* nikiwa ndani ya Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Mtwara pale kuna *godown* moja linaitwa *Canadian Spirit*, ile ilikuwa ni meli moja inahudumia kati ya Dar es Salaam na Mtwara. Halafu kuna jengo lingine pale linaitwa MS Mtwara, meli moja ina-serve

kati ya Dar es Salaam na Mtwara. Usiku ukitaka hata kujiburudisha na mke wako inabidi utoke uende *guest house* kwa sababu kila mmoja atakusikia vitendo unavyofanya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake Askari wanalazimika kutafuta fedha za ziada kwa njia ya rushwa ili waweze kujikimu, waweze kujenga nyumba uraiani waondoke na adha hii. Lakini Serikali haitaki kujenga nyumba za Jeshi la Polisi na haitaki kuwapa mishahara.

Mheshimiwa Spika, *TRA* walipokuwa wanakusanya kodi kidogo, mlisema kwamba ili wakusanye lazima tuwape mishahara minono na posho ili waondokane na kuomba rushwa na mkafanya hivyo. Kuna kigugumizi gani kwa hawa mnaowatuhumu namba moja kwamba, wanapokea rushwa. Huko ni kupambana gani na rushwa ndani ya nchi hii. Hakuna dhamira ya dhati.

Mheshimiwa Spika, kama sitapata majibu yanayozungumzia kuanzisha Mfuko Maalum ndani ya Jeshi la Polisi, utakaoboresha mishahara yao, posho zao pamoja na kujenga nyumba watoke kwenye ma-*godown*, watoke kwenye ma-*box*. Haya mambo ya akina Jerry Muro, sijui wamepiga picha Askari anapokea rushwa, huko ndiko kupambana na rushwa ndani ya Jeshi la Polisi! Lazima tuweke pesa kwenye vyombo vinavyotuhumiwa na rushwa ili wawe na maslahi, wasipokee rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kukubali mambo ya namna hii, kila siku nyimbo ni zilezile nchi inaangamia madawa, rushwa na vitendo hivi vinafanywa ndani ya Serikali yetu ninayoiamini ya CCM. Maisha magumu kwa Watanzania yanatokana na uchumi kuwa mbovu halafu leo tunataka kufumbafumba macho, tunawaonea huruma; haiwezekani hata kidogo. Siungi mkono hoja hii mpaka nipate majibu ya dhamira ya dhati.

Mheshimiwa Spika, niende Mwibara pale. Humu ndani wanaandika sijui maafa, kuna Kitengo cha Maafa; huu ni

ulaji mtupu ndani ya Serikali ya CCM. Umeandika humu kwamba kuna ukame, ukame unasababisha maafa, maana yake watu wasipate chakula. Pale Mwibara tumezungukwa na maji ya Ziwa Victoria, tunachohitaji ni miundombinu ya umwagiliaji kutoka Kabainya mpaka Igundi mpaka Ilamba ili wakati wote tuwe na chakula. Mnaona mkitupa miundombinu ya umwagiliaji hiyo, kete yenu ya Kakitengo ka Maafa katakuwa na hamtapata ulaji. Hatuwezi tukakubali hata kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, chakula kinapelekwa kule, unakuta wananchi wamejipanga wanapata *amboni* moja. *Amboni* moja ni sawa na kilo nne, tunawaambia mini wananchi hawa? Eti tunakuja kuwasaidia. Hatuwezi kukubali. Siungi mkono hoja; tunataka majibu ambayo kwa kweli ni ya dhati. Humu ndani sijui mnaweka shilingi bilioni moja, mazishi ya viongozi. Mazishi gani ya viongozi mnatenga shilingi billioni moja mnatenga kwa ajili ya nchi hii? Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali, huu ni wizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwibara wanakufa njaa, tunakosa skimu za umwagiliaji, mnatenga *one billion* kwa mwaka kwa ajili ya mazishi ya viongozi. Kama kwa mwaka hatujafiwa na viongozi hao, hatujawahi kuletewa *feedback report* kwamba ile pesa sasa imefanya kazi fulani. Wizi mtupu ndani ya Serikali. Mimi nimechoka, sikubaliani na bajeti ya namna hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tulizungumza hapa kuhusu mazao makuu katika nchi hii; korosho, pamba na kahawa, ni lazima tuwe na Mfuko Maalum pale ambapo bei inatetereka wakulima hawa ili wasikate tamaa na ndiyo mazao ambayo yanaendesha uchumi wa nchi hii. Leo Waziri Mkuu humu ananiwekea maandishi na nimeshindwa hata kumwelewa. Ooh Serikali imeshaongea maoni na wadau; hivi hao wadau wanakaa Ujerumani au Ufaransa? Ooh, sasa tunakaa na watalaam, watushauri juu ya maoni ya wadau. Wataalam wa wapi tena wanaoshauri juu ya wadau? Nawaambia ndugu zangu Wabunge tusikubali maneno matamu ya namna hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tusikubaliane na Bajeti ya namna hii. Tunataka Serikali ije na majibu katika Bajeti hii, kwamba, tayari Mfuko Maalum kwa ajili ya wakulima wetu. Mwibara kule wanaanza kukata tamaa kulima pamba. Nimepata tabu sana mimi na Mkuu wa Wilaya kuhamasisha watu walime pamba, wanasema wamechoka. Sasa kabla hawajakata tama, kuna mzee mmoja pale anaitwa Mafiri Mnyaga aliniambia nikirudi kule kama hakuna Mfuko Maalum wa ku-stabilize bei, yeye ndiye atakuwa mtu wa kwanza kukata tamaa na ataitisha maandamano kwa wakulima wote wasilime pamba. Wasipolima pamba, humu sote tutavaa nini? Si kila mmoja atakimbia huku ameshika huku mbele? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu na timu yake aje na majibu juu ya mambo haya matatu, vinginevyo nitashawishi Wabunge wenzangu wote, tusikubaliane maneno matamu ya kila mwaka kwenye Bajeti. Uchumi unahujumiwa halafu tunakuja hapa tunapakwa asali kwenye mdomo, hatutakubaliana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Serikali ya CCM ndiyo inayotufanya hata humu ndani tunacheke kwa furaha. Serikali ya CCM ndiyo inayotufanya hata humu ndani tunakuwa na ubaridi wakati wa joto. Sasa kama yote haya inayafanya na tunapata furaha hii, kwa nini Serikali hiyo hiyo inashindwa kutufurahisha kwenye maeneo mengine? Huko kwenye maeneo mengine kuna nini? Vitu vya wazi hivi tunavyoviona mnatufurahisha, vingine huko kuna nini?

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Bunge la Bajeti na nitaomba Wabunge wenzangu mniunge mkono, nitakuja na orodha ya watendaji wa Serikalini, wanaopokea rushwa na madawa yanaendelea na wanaojihuisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu hatamwambia Shekiondo wale aliowasema kwamba wanafahamika ila tu mbinu ndiyo wanawazidi, hatakuwa amewajibishwa. Huwezi kuwafahamu watu halafu

usiwakamate? Kwa nini kule mtu anaiba kuku hata kama upelelezi bado, anakamatwa anapelekwa Mahakamani? Kwa nini hawa wanafahamika, Shekiondo asiwakamate akawapeleka Mahakamani? Kama sio rushwa ni nini? Awajibishwe kwa sababu amekiri kwamba wanawafahamu lakini wameshindwa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini hajajakuomba pesa humu tuidhinishe walete *FBI* kama wamezidiwa mbinu? Mbona juzi Zanzibar kwenye mauaji ya Askofu tayari *FBI* wamekuja pale? Nitaomba Wabunge wenzangu mnisaide.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, siungu mkono hoja mpaka hayo niliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu ayafanyie kazi. (*Kicheko*)

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi nitajielekeza katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, nitazungumzia kidogo kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ambao upo kwenye ukurasa wa nne wa muhtasari wa matumizi; mapato ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametenga bilioni 114/-.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Mbunge sasa mwaka wa tatu, Jimbo langu linatengewa kwa mwaka sh. 24,200,000/- na Majimbo mengine vile vile nahisi yanapata mchango mdogo sana. Fedha hizi zinatumika katika masuala ya elimu, maji, afya na barabara. Naomba Serikali yetu kupitia Bunge hili Sheria ilioanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo iletwe hapa tuipitie ili turekebishe kwa sababu fedha hizi hazitoshii na kwa sababu tunajenga nyumba moja, naomba pia hata Wabunge wa Viti Maalum waruhusiwe kupata fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunajenga nyumba moja, hakuna haja ya kupigania fito. Kila mmoja atatimiza wajibu wake, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali atakuja kukagua hesabu zetu na hivyo kama mmoja wetu atakuwa

amekiuka Sheria ya Mfuko ule, basi Sheria ichukue mkondo wake. Lakini naomba Sheria ile iletwe hapa, ili Mfuko uongezwe na watu wote wapate haki yao wa Viti Maalum na sisi wa Majimbo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, naomba nizungumzie hali ya elimu nchini, lakini hasa nijielekeze kwenye elimu ya juu. Pamoja na juhudzi zote ambazo Serikali inafanya za kuboresha elimu ya msingi na sekondari. Lakini pia naomba Serikali yetu iangalie vyuo vikuu vya umma nchini. Hakuna anayesimama na kuzungumzia habari ya elimu ya juu, vyuo vikuu vya umma, ambavyo ukiangalia bajeti ya maendeleo haitoshi na wakati mwingine haipelekwi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, bajeti yake ya maendeleo ni ndogo sana na vyuo vikuu vingine. Huku tunahamasisha vijana wengi waendelee na elimu ya juu wakati hatupanui vyuo vikuu vya umma nchini. Baada ya kufaulu *form six*, wataendelea kusoma chuo kipi kama hatuweki bajeti ya kutosha katika vyuo vikuu vya umma hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, naomba nizungumzie pia taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa kuhusu hali ya uchumi. Tumeambiwa hapa hali ya uchumi imeboreka hasa kwa vigezo vya kushuka kwa mfumko wa bei kutoka asilimia 19.4 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 10.4, Februari, 2013, lakini pia tukaambiwa ukuaji wa uchumi umeongezeka kutoka asilimia 6.4 mwaka 2011 na kufikia asilimia 6.9 mwaka huu. Takwimu hizi ziwe na tafsiri nzuri kwa wananchi wetu. Hali za maisha ya wananchi wetu si nzuri.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi hazina maana kama hali halisi ya maisha ya watu wetu haiwezi kuwa sambamba na ukuaji huu ambao tunaambiwa. Ukiangalia hali ya chakula wananchi wetu hawamudu kula milo mitatu kama dira inavyosema na kama MKUKUTA unavyosema. Vile vile ukiangalia hali ya hospitali zetu, dawa hazifiki mwisho wa

mwezi, wananchi wetu wakienda kupata huduma ya afya, wanaandikiwa karatasi na Madaktari, lakini dawa hawazipati.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata ubora wa elimu yetu ambayo wote tunasema hapa kwamba, watoto wetu wamefeli sana. Sasa tunapoambiwa hali ya uchumi imekuwa, naomba pawe na tafsiri sahihi, takwimu hizi hazitusaidii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu hapa nchini. Miradi mingi ya maendeleo hapa nchini, bajeti ya maendeleo ni ndogo sana kwa sababu tumekuwa tukitegemea sana mchango wa wahisani. Kama wasemaji waliopita walivyosema, hali hii haitatusaidia sana na kama vile taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI illiyoyeleza, na mimi nikwiwa ni Mjumbe wa Kamati hiyo, naomba sana Serikali sasa ihakikishe kwamba inapunguza utegemeaji wa fedha za wahisani kwa sababu ameonesha kutokuwa na mwenendo mzuri kwani miradi mingi imefeli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukitenga fedha nyingi za ndani, nina imani kwamba, tutatia nguvu katika kukusanya mapato yetu ya ndani ili fedha hizo sasa ziweze kutumika kuleta maendeleo katika miradi hiyo. Mwalimu Nyerere katika hotuba yake ya mwaka 1964 aliwahi kusema: "Bahati mbaya sana mfanyakazi wa Serikali hawezi kuwa tajiri isipokuwa wafanyabiashara wanaweza kuwa matajiri".

Mheshimiwa Spika, sasa cha ajabu ni kwamba, baadhi ya wafanyakazi wa umma si waadilifu sana, fedha zetu ambazo zinakusanya na Halmashauri zetu wanazitia mifukoni mwao. Naomba tujenge utamaduni wa kuwawajibisha watu kama hawa, tusiangularie ngazi ya mtendaji. Tena tujenge utamaduni kama kule nchi za magharibi, ukishatuhumiwa jambo lolote, basi uchukue hatua ya kuwajibika kupisha uchunguzi dhidi yako, kuliko kusema siwezi kuijuzulu, ni bora kufariki kuliko kuijuzulu sasa tabia hiyo sio nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumze kwa ufupi sana kuhusus habari za udini. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuambia kwamba, ni bahati mbaya hali hii sasa inanyemelea Taifa letu. Naiomba Serikali yetu Katiba ya sasa bado ina meno na inasema kwamba Serikali haina dini isipokuwa Watanzania wana dini zao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali moyo huu wananchi waendelee kuufahamu na tena iwachukulie hatua kali sana wale ambao wanajaribu kupenyeza siasa zao au nia zao kwa kuingiza udini. Taifa hili ni moja na sisi humu ndani sote ni wamoja. Humu ndani sote ni ndugu na hata tunapotoka nje haiwezekani Fatuma amkute Sylvester amepata ajali amwache. Kwa hiyo, ni ajenda ya watu wachache, Serikali iwashughulikie ipasavyo, iwe na meno yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tusipokemea udini, hatuna Taifa, kwa sababu ndani ya CCM kuna watu wa imani tofauti, ndani ya CHADEMA kuna watu wa imani tofauti. Sasa tutagawanyika sana na hata kwenye majeshi yetu, Serikali ikemee, sasa tuseme mwisho yatosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ya Kanuni zetu.

“Bila ya kuathiri masharti ya lbara ya 100 yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.”

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Kangi Lugola akitoa mchango wake alisema, baadhi ya Mawaziri

wanahuksika na madawa ya kulevya. Sasa ingekuwa vizuri sana angetoa majina ya baadhi ya Mawaziri wanaohusika ama ningemwomba atoe kauli hiyo kwa sababu sisi wote Mawaziri hapa tutakapotoka mmoja ataangalia ni nani ambaye anahuksika na biashara hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kangi Lugola ama afute kauli yake au awaseme hao wanaohusika na biashara hiyo ya madawa ya kulevya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola, umesikia hiyo, ama unafuta usemi wako au unataja hayo majina, kusudi kila mtu asianze labda ni huyu au ni huyu, aseme tu ni huyu na huyu.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri alinisikiliza vizuri, siwezi kufuta kauli hiyo, kama alinisikiliza vizuri. Kwa sababu kauli yangu na anachoeleza Mheshimiwa Waziri ni tofauti kwa sababu mimi nili-*justify* kwa mambo ama rushwa wanachukua au wanahuksika kwa sababu hao watu walishatuambia kwamba wanawafahamu wapo.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira ambayo mtu unasema unamfahamu, halafu hutaki kumtaja basi tuna-*draw inference* kwamba, wewe ambaye unawafahamu, lakini hutaki kuwachukulia hatua au kuwataja, aidha, wewe mwenyewe unahuksika au unakula rushwa. Kwa hiyo, ni lazima tu-*draw inference* na hawa ndiyo Mawaziri na Taasisi za Serikali ndiyo wamemteua hayo Christopher Shekiondo na wakati anayasema hayo hakuna hatua walizomchukulia. Sasa kama hakuna hatua walizomchukulia inamaanisha nini; kama sio kumaanisha kwamba, aidha, baadhi ya Mawaziri, ndiyo sababu nimesema baadhi ya Mawaziri? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kama alinisikiliza vizuri sioni kama nina sababu ya mimi kufuta kauli yangu. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa sababu hatuna *Hansard* kuona jinsi alivyosema, basi mimi nasema ngoja tupate *Hansard* tutajua kilichosemwa. Inawezekana pia namna ya kuongea, unajua lugha ziko tofauti; lakini masikio yangu yalinituma kwamba wamo Mawaziri. Kwa hiyo, tutaaingalia *Hansard* yenye kesho.

Enhe, Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kuuliza; Mheshimiwa Waziri aliposimama alikuwa anaomba nini? Alikuwa anaomba Mwongozo wa Spika, ilikuwa ni kuhusu utaratibu, alikuwa anatoa taarifa au alikuwa anafanya nini? Kwa sababu kama kuhusu utaratibu Mheshimiwa Kangi Lugola amekosea Mheshimiwa Waziri alitakiwa asimame wakati Mbunge bado anasema kama inavyosema Kanuni ya 68(1):

"Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno 'kuhusu utaratibu' ambapo Mbunge yoyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza".

Sasa Waziri alikuwa anaomba nini? Sikumsikia akisema 'Mwongozo wa Spika', hakusema 'Kuhusu Utaratibu,' hakusema 'Taarifa'. Amejiamkia tu, tufuate Kanuni. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kuna maneno unaweza ukasema wewe ni mtoto au wewe una miaka miwili, yote yanamaana hiyo hiyo. Mheshimiwa Waziri alisimama mara baada ya Mheshimiwa Lugola kunyamaza. Mimi nikamwambia nilimtaja mtu ili achangie vizuri, ningependa muda wangu utumie vizuri kwa kumwacha azungumze, kwa hiyo nitakupa nafasi utoe mwongozo wako. Kwa hiyo, ninachokisema ni sahihi na ndivyo ilivyokuwa.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kujaribu utaratibu wetu tuliokulaliana, naona mmefanya kazi nzuri sana. Kwa sababu katika muda wa dakika 165 tulizokuwa nazojioni hii wachangiaji wamekuwa 17. Kwa hiyo, tumefanya vizuri na nadhani tutaendelea kufanya vizuri zaidi siku zinazofuata za kuchangia hotuba hii. Kwa sababu hiyo, tumesikiliza hotuba nyingi sana leo na sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 12, Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)